ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nane - Tarehe 19 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, Wajumbe, kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi tuliyoyafanya mwishoni mwa mwaka 2016, Kanuni ya 40(4) inahitaji maswali ya nyongeza yanayojibiwa kwa maandishi, yawasilishwe mbele ya Baraza kupitia Taarifa ya Spika. Madhumuni ya Kanuni hii ni kuwawezesha wananchi kufahamu majibu ya maswali hayo yanayoulizwa kwa niaba ya wananchi wanaowakilishwa kwenye chombo hiki.

Waheshimiwa, Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 10 Mei, 2017, Mheshimiwa Nadir Abdullatif Yussuf Alwardy aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Fedha na Mipango na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni hiyo ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi.

Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuwasomea majibu hayo kwenu Waheshimiwa Wajumbe na kwa wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Nadir Abdullatif Yussuf Alwardy alitaka kujua idadi ya maeneo huru '*free zone'* yaliyotolewa kwa Wawekezaji na majibu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

" Kwa mujibu wa sheria ya uwekezaji ya mwaka 2004 kifungu nambari 24 na 27 kuna jumla ya maeneo huru matano (5) ambayo ni maeneo huru ya Amani, Maruhubi, Fumba Micheweni na *Airport*.

Hakuna eneo hata moja kati ya maeneo huru niliyoyataja hapo juu lililotolewa kwa mwekezaji. Maeneno yote hayo yapo chini ya Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (ZIPA) kwa mujibu wa kifungu nambari 4(3) cha sheria ya Uwekezaji. Jukumu la uendelezaji wa maeneo hayo ni la Serikali.

Aidha, Mheshimiwa Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf Alwardy alitaka kujua idadi ya maeneo ambayo hayajaendelezwa hadi hivi sasa majibu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

*"*Hadi hivi sasa maeneo mawili ya Micheweni na *Airport* bado hayajaendelezwa.

Maeneo ya Fumba, Amani na Maruhubi yanaendelezwa kadri ya hali ya fedha itakavyoruhusu".

Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwasilisha.

Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe taarifa kwamba leo hatutakuwa na Maswali kwa sababu tu wachangiaji wa hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora bado inaendelea na wachangiaji ni wengi, kwa hivyo tumeona kuwa tuwape nafasi nyinyi Waheshimiwa Wajumbe kwa kujadili hutuba ile tuendelee nayo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa namuiita Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni, akifuatiwa na Mhe. Zulfa Mmaka na Mhe. Hamad Abdalla Gerei ajitayarishe.

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana jana wakati tunaahirisha Baraza nafikiri nilikuwa nichangie mimi na mpaka anamaliza kufunga akawatangaza wachangiaji wa mwanzo atakuwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani, ningeomba sana tuwe tunaangalia hivyo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo nilikuwa sijaliona kimakosa, kibahati mbaya. Kwa hivyo hilo halina tatizo kwa vile nimeshamtaja Mheshimiwa mwache aendelee baada ya yeye utafuata wewe.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya hapo nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Wizara hii mwalimu wangu Mhe. Haoroun Ali Suleiman kwa uwasilishaji na umahiri sana kwa hotuba hii muhimu na taasisi zake, lakini vile vile nimpongeze Mhe. Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa utendaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Wanu Hafish Ameir kwa uwasilishaji wake mzuri wa ile ripoti ya Kamati ya Sheria ambayo imesheheni mambo mbali mbali, lakini nimpongeze vile vile Makamo Mwenyekiti wa PAC kwa ripoti yake ambayo amewasilisha na niwapongeze wajumbe wote walionitangulia kwa michango yao.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii au wizara hii au Ofisi hii ina taasisi 22 ni ofisi muhimu sana yenye majukumu mengi ya kitaifa nichukue fursa hii ya kuwapongeza watendaji wote wanaohusika na taasisi hizi 22 kwa utendaji wao. Kabla sijatoa michango yangu ningependa kuzungumzia moja kati ya hichi kitabu cha bajeti, katika hotuba yake Mhe. Waziri jana alituomba radhi katika makoseo kwenye jalada la kitabu hichi kutokana na mwaka ambao umeainishwa hapo na yeye kwa mujibu wa *draft* aliyoipeleka kwenye kiwanda au kwa wakala wa mpigaji chapa.

Lakini nichukue nafasi hii vile vile sijui nimuombe radhi Waziri wangu kwa sababu kitabu hichi kwa sisi wachambuzi wa vitabu na yeye najua mwalimu alikuwa mchambuzi wa vitabu katika kurasa za mwanzo hakuna kurasa za yaliyomo, kwa hivyo hii ni kasoro kubwa sana ambayo inawakosesha wajumbe kuweza kwenda moja kwa moja katika jambo linalokusudiwa. Niwaombe sana wenzetu wakala wa mpigaji chapa wawe makini sana wanapochapa vitabu ambavyo vinaletwa katika Baraza hili tukufu, na huku tukiwa tunajigamba kwamba tunatangaza soko ubora wa kazi ndio ambao utatupatia soko. Lakini hitilafu kama hizi kwa kweli nadhani hazitotujenga, kwa hivyo naomba watendaji wa wakala wawajibike vizuri *editor* awajibike vizuri kwa sababu humu mna wachambuzi wa vitabu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika michango yangu nianze katika ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, kuna *program* hii ya usimamizi wa utekelezaji wa kesi za jinai ukweli usiofichika kwamba kuna malalamiko mengi ya wananchi wetu juu ya ucheleweshwaji wa kesi za jinai na kilio kikubwa sana kipo katika

kesi za uzalilishaji. Lakini hata sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumepiga kelele sana juu ya kesi za madawa ya kulevya. Niipongeze sana ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka kwa kuanzisha mkakati wa kupambana na kesi za udhalilishaji ambao sasa utazihusisha au unazihusisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, Mahakama pamoja na Polisi. Nina imani kwamba mkakati huu kama utasimamiwa vizuri basi malalamiko yale ya wananchi yanaweza kupungua kwa asilimia kubwa.

Lakini vile vile nipongeze ndani ya ripoti hii kwamba wenzetu wameweka takwimu za kijumla juu ya kesi ambazo zimefunguliwa zilizotolewa maamuzi na zile ambazo zinaendelea niwapongeze sana, ombi langu unajua kutokana na unyeti wa mambo haya matatu udhalilishaji, madawa ya kulevya na vitendo vya rushwa na wahujumu wa uchumi, kitabu hichi kingependeza sana kama tungepata takwimu za kina kabisa juu ya kesi za udhalilishaji peke yake, kesi zinazohusiana na madawa ya kulevya peke yake na kesi za uhujumu wa uchumi peke yake. Kwa sababu takwimu hizi zingeweza kuwasaidia wajumbe wa Baraza hili kuona uzito wa kila moja ya haya ambayo nimeyataja.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii bila ya kuchambua kesi za udhalilishaji za nyuma ngapi, zilizopokelewa ngapi ndani ya mwaka huu 2017 na ambazo zimepata hukumu hii itawafaya wajumbe wasiweze kuona uzito wa tatizo hili na peke yake data hizi ndio ambazo zitaweaza kuleta ile picha halisi ya uzito na mataizo ambayo yanajitokeza. Kwa hivyo niiombe sana ofisi hii hususan Mhe. Waziri, atakapokuja tupate kwa maandishi takwimu zinazohusiana na kesi za udhalilishaji, madawa ya kulevya, kesi za rushwa na wajuhumu wa uchumi.

Lakini vile vile kuna tatizo kubwa sana la talaka katika ndoa tungependa tupate takwimu juu ya kesi mbali mbali zilizopokelewa ndani ya mwaka huu za ndoa na talaka, kwa sababu tatizo hili limekuwa kubwa sana katika jamii yetu. Hii itatufanya sisi wajumbe kuweza kuona uzito wa matatizo haya na jinsi gani yanavyoshughulikiwa na vyombo hivi vya sheria.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije Mamlaka ya kuzuia rushwa na wahujumu wa uchumi kuna *program* ya uzuiaji wa vitendo vya rushwa na wahujumu wa uchumi. Mamlaka hii ni mamlaka moja muhimu sana na lengo lwa kuanzishwa kwa mahakama hii ni kuweza kuzuia lakini hatimae kuondosha kabisa kwa vitendo vya rushwa na wahujumu wa uchumi, vitendo hivi bado vinaendelea katika nchi yetu. Lakini niwapongeze wenzetu kwa juhudi kubwa wanazochukua katika kuelimisha jamii, kwa kupitia kwenye maeneo wanayoishi lakini vile ile kwa vipindi mbali mbali katika vyombo vya habari, niwapongeze sana wanachukua juhudi kubwa sana.

Lakini kama nilivyotangulia kusema takwimu ambazo wametuonyesha wenzetu hapa ni takwimu za tuhuma 17 na kuna kesi 4 tu ambazo zimefunguliwa majalada katika mwaka huu, lakini hakuna takwimu inayotuonyesha kwamba kuna kesi iliyopata ufumbuzi. Ukweli Mhe. Mwenyekiti mamlaka hii tokea ianzishwe sijui kama kuna kesi ambayo ilipata ufumbuzi. Na kuna kesi nyingi sana ambazo ndani ya vyombo vya habari utasikia mtu kategewa mtego na kakamatwa *red handed* akitoa rushwa. Sasa inakuwaje kesi hii ikae miaka mitatu au minne iwe haijapata ufumbuzi. Mimi nafikiri bado kuna tatizo aidha kwa watendaji wa mamlaka hii, au kuna tatizo katika ofisi ya DPP lakini tuweze kuyasoma matatizo ambayo yapo ili suala hili la rushwa na wahujumu wa uchumi liweze kuchukuliwa hatua kwa sababu linaendelea siku hadi sikue hata katika taasisi zetu hizi za Serikali. Kama kweli tunataka nchi hii iwe na utawala bora basi haki iweze kutendeka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika fungu lile la GO 8 Kamisheni ya Utumishi wa Umma juu ya takwimu katika kiambatanisho No. 3 ya hotuba hii ya Mhe. Waziri, hususan katika takwimu za wale wafanyakazi waliochukua likizo bila ya malipo. Mhe. Mwenyekiti, inashangaza kidogo najua Mhe. Waziri ni mwalimu na yeye alikuwa mwalimu wa hisabati alikuwa mwalimu mzuri sana, lakini tukitizama takwimu ya wafanyakazi waliochukua likizo bila ya malipo tukitizama katika mwaka wa bajeti iliyopita takwimu inaonesha walikuwa wanne. Lakini la kushangaza sana Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hichi ambacho tumekisoma kuna wafanyakazi wanne tu ambao wametajwa kwamba ndio waliochukua likizo bila ya malipo katika Serikali nzima hii inashangaza sana. Inawezekana kuna takwimu ambazo zina matatizo ningependa sana Mhe. Waziri akae na watendaji wake waweze kuzi-*review* takwimu hizi ili watuletee takwimu zenye usahihi.

Mhe. Mwenyekiti, kama tutawasimamisha wafanyakazi waliomo Baraza hili waliochukua likizo bila ya malipo wanafika 12 haiwezekani takwimu ya Serikali nzima wafanyakazi waliochukua likizo wawe 4 haiwezekani, wenzetu watendaji wakakae upya watuletee takwimu zenye uhakika. Baraza hili hivi saa lina wachambuzi wakubwa sana, takwimu hizi ambazo zinatia mashaka hizi takwimu hazina nafasi tukisimama hapa wafanyakazi waliochukua likizo ndani ya Baraza hili wanazidi kumi. Sasa haya ndio yanayotufanya baadae tuwe na wafanyakazi hewa. Tumechukua likizo bila ya malipo mishahara yetu pengine inakwenda Mawizarani hatuwezi kufika kwa kupokea takwimu hizi lazima taasisi inayohusika ikae na Mawizara kuweza kuona kwamba inapata takwimu sahihi kabisa za waliostaafu, waliofukuzwa kazi na wale ambao wamechukua likizo bila ya malipo umakini unahitajika sana.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika Ofisi ya Mufti ofisi hii ni muhimu sana katika mustakbala mzima wa masuala ya kidini katika nchi yetu na hususan dini ya Kiislamu. Niwapongeze sana wenzetu kwa kazi kubwa sana wanayoichukua katika kutoa fatwa mbali mbali. Vile vile niwapongeze katika kutoa miongozo ya kidini, kuhamasisha suala la amani na utulivu. Wenzetu wamejitahidi sana na niwapongeze sana chini ya Katibu Mtendaji Maali Soroga, wamejitahidi sana katika suala zima la kusimamia amani na utulivu katika nchi yetu, nawaendelee na najua wanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyotangulia kusema ripoti ya Kamati au wenzetu wanahitaji sana wapewe fungu lao maalum ambalo linajitegemea ili waweze kupunguza changamoto mbali mbali ambazo zinawakabili na yale malengo ambayo yamekusudiwa ndani ya Afisi hii yaweze kufikiwa kwa ufanisi mkubwa. Wenzetu hawa niwaombe washirikiane na Afisi inayohusika ili watuletee takwimu zile ambazo mmeziomba. Kwa sababu suala la ndoa na talaka ni suala ambalo hivi sasa lina migogoro mingi lakini hakuna takwimu ambayo inatupa picha hasa ya uzito wa tatizo hili. Nimuombe sana Katibu Mtendaji katika Afisi hii kuweza kuipata takwimu hizo kwa kushirikiana na Afisi zinazohusika na mambo ya sheria hususan Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana wenzetu wa Afisi ya Mufti pamoja na juhudi kubwa sana wanazochukua katika kusuluhisha migogoro, hususan katika misikiti yetu ambayo migogoro inazuka siku hadi siku, sijui chanzo chake ni nini zamani Misikiti ilikuwa haina migogoro, lakini siku hizi kila Msikiti unaojengwa basi panakuwa na migogoro. Sijui kwa sababu misikiti inakuwa na maduka na vyanzo vingi vya mapato, sijui tutafika wapi. Ningemuomba sana Muhusika Mkuu wa kitengo hichi kuweza kufatilia Msikiti Shurba pale Kidongochekundu. Vyombo vya habari juzi vilitoa habari ya unyanyaswaji wa wanafunzi katika madrasa ya pale, hili linasikitisha sana. Ningeomba sana Afisi ya Mufti ifuatilie suala hili ili vijana wetu ambao wanasoma madrasa waweze kutendewa haki na waweze kusoma katika mazingira ya salama.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nikushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii na niwaombe Wajumbe wenzangu waendelee kupitia hotuba hii na hatimaye waipitishe hotuba hii bila ya kikwazo chochote. Mimi niseme naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Lakini yale niliyoyaomba naomba sana mwalimu wangu ayafanyie kazi kwa sababu lengo ni kuweza kuisaidia serikali. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi, sasa namuomba Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Hamad Abdalla Gerey ajitayarishe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia kuwa mtu wa pili nashukuru sana. Awali ya yote niungane na mwenzangu aliyetoa shukurani, pole na pongezi. Pongezi zangu za dhati kabisa kutoka ndani ya sakafu ya moyo wangu zinakwenda kwa Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa namna alivyoweza kuwafurahisha watumishi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba Rais amekuwa ana uchungu na watu wake anaowaongoza ni Rais wa kupigiwa mfano sana. Aliahidi katekeleza na leo hii Maalim Haroun anapata sifa na pongezi kwa kile ambacho alichotendewa na Mhe. Rais, nampongeza sana katika hilo. Kwa kweli Rais tumepata zawadi kutoka kwa Mungu ni tofauti pengine na Rais wengine. Mhe. Rais, wetu huyu kama binaadamu basi asilimia 99.9 anayo hiyo moja tumuachie mwenyewe *Subhana llahu Wataallah*. Tulikuwa tunamaraisi hapa walipewa mpaka majina, wengine wanaitwa hapa pangu kwa kunyang'anya vya watu. Lakini huyu Mhe. Shein hata sisimizi wa mtu ahajawahi kuchukua, namsifu sana na kumpongeza sana Mhe. Rais kwa moyo wake kama huo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika mchango wangu aya ya 37 kuna masuala ya nyaraka za serikali. Sitosema sana, nitaiomba tu Wizara ya Mhe. Haroun, imekuwa kilio cha muda mrefu. Basi angalau atakapokuja atueleze tumefikia wapi? Tuliambiwa kuna ripoti imepelekwa, hatujaipata mpaka leo. Tunaomba atwambie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu na lini ile nyumba ya jirani ya Afisi ya Nyaraka haileti picha nzuri. Ni lini wale watu wataweze ku-*compensation* waondoke na lile eneo lote limilikiwe na Afisi ya nyaraka. Ile sehemu ni nyeti na nzuri, haiwezekani wanapita watu mbali mbali na wageni mbali mbali kutoka kwenye lango kuu la kuingia mlango wa nyaraka kuingia kwenye nyumba ambayo anaishi mtu. Tukitilia maanani kwamba hii serikali ni yetu, ardhi ni yetu, kwa nini hatufanyi *compensation* na wale watu tukaweza kuwaondoa likawa lile eneo likawa katika hali ya usalama. Kwa sababu kama unampata mtu muhalifu maeneo kama yale anaweza akahamia nyumba ya pili akachimba siku ya pili anakuja kuibukia katika jengo lako la nyaraka akachukua nyaraka muhimu. Limesemwa sana huko nyuma na mimi nalikazia kidogo tu Mhe. Waziri katika suala hili nitakuomba sana. Lazima upitishe maamuzi magumu tuone haraka iwezekana lile eneo linakuwa la salama na amani.

Mhe. Mwenyekiti, niende aya ya 49, Afisi ya Mufti. Mwakilishi mwenzangu kwa sababu tumepakana mipaka alizungumza kadhia nzima juu ya Msikiti wetu wa Shurba au Masjidi Arafa. Mimi ni shahidi Mhe. Waziri nishafika na ujumbe wangu wa Kamati nzima ya watu wa Jang'ombe kwenda kwenye Ofisi yake juu ya kadhia ya Msikiti ule pale. Umekuwa ule msikiti mwenye punda anawekwa mkiani. Ule Msikiti umejengwa badala ya matatizo yaliyotokea katika Msikiti Hidaya ambao ni Mshelishelini. Ule Msikiti, kuna watu walishughulika sana kuanzia mwanzo Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe Mhe. Said Bakari Jecha alikuwepo pale, wakaja kina Chengo, wakaja kina Nyanga, kuona mustakbali wa Msikiti ule pale unapatikana ufumbuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, nina ma-*document* mbali mbali haya ni ushahidi Mhe. Waziri nimeshampelekea Afisi kwake, kwamba kwa nini kadhia ya Msikiti ule haiwezi kumalizika. Naomba sana Mheshimiwa, Wananchi wa Jang'ombe wananyanyasika kwa msikiti ule. Mimi kama msemaji wao siko tayari kuona kwamba kile kilio chao katika serikali hi hakisikilizwi, nitakuomba sana Mhe. Waziri suala la Msikiti wetu wa Jang'ombe ulichukulie kidhati *lillahi* haraka upatikane ufumbuzi.

Leo hii imefika *time* watoto wanafungiwa wasisome ndani ya msikiti, wanakaa kichochoroni tu pana tope hapo hapo, pana mambo machafu watoto ndio wanasoma. Watoto wale ni watoto wa Jang'ombe. Kwa sababu wanasema kwamba hawatoki Makunduchi unafumbia macho, fahuwa. Ingekuwa wanatoka Makunduchi ungefanya utafiti. Tunakuomba sana Mheshimiwa katika hili mimi siko tayari kuona vijana wangu wa jang'ombe wananyanyasika kwa kitu ambacho kimejengwa kwa mustakbali na manufaa ya watu wa jang'ombe. Kadhia ya Msikiti nakuomba sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna barua mbali mbali hapa kutoka Afisi ya Mufti kukabidhiwa, kuna sijui ongezeko la eneo, barua nyingi ambazo zote hizi ni shahidi unazo kwenye meza yako kwa sababu nimekuletea mimi mwenyewe kwa mkono wangu. Nitakuomba sana Mwenyekiti, suala la Msikiti, sana tena Mhe. Waziri nipate ufumbuzi wake *at least* watu wa Jang'ombe wapate faraja na Msikiti wao.

Msikiti ule wa Jang'ombe lakini vereje leo wanatoka watu Darajabovu ndio wawe maimamu wa pale. Imefika hatua mpaka Imamu wa Msikiti wa Hidaya aliyokabidhiwa alishushwa kwenye Membar na hizo taarifa mnazo, nitakuomba sana linaniudhi sana hili jambo kwenye nafsi yangu. Mimi kama kiongozi wa Jang'ombe ninalisemea silinyamazii hata dakika moja kuona mustakbali wa Msikiti ule unapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wakfu na Mali ya Amana, ni kweli wenzetu wanajitahidi kwa namna moja. Lakini hivi juzi imetokewa kadhia nzima juu ya madeni zinazodaiwa taasisi za kusafirisha Mahujaji na kuwatia hofu Mahujaji wetu wanataka kwenda Makka. Je, tatizo ni nini? Watu wanajiandaa na safari za Makka lakini mara wanaambiwa Mahujaji wa Tanzania hawatopokelewa, hawatosafiri wanadaiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hili suala Ofisi yako imeliratibu vipi. Bajeti iliyopita nimelizungumza hili na leo nalizungumza tena nini tatizo mpaka kupelekea mahujaji wetu wakakosa amani juu ya suala la safari zao za kwenda Makka kutokana na madeni wanazodaiwa taasisi zinazosafirisha Mahujaji. Nitakuomba sana Mheshimiwa utakapokuja hilo uniwekee wazi kwa sababu sasa hivi watu wapo katika maandalizi na Kampuni mbali mbali zipo lakini bado hawajui mustakbali wa safari zao zile kwa sababu ni safari ya ibada, nakuomba sana Mhe. Waziri unisaidie katika suala hilo.

Niende katika Chuo cha IPA aya ya 76, ni kweli Chuo kinahitimisha wanafunzi wa kada mbali mbali katika chuo kile, Hongereni sana na wanahitimisha wanafunzi wa *human resources* pale. Lakini bado kumekuwa na tatizo kwamba baadhi ya kada hizo ambazo zinaletwa pale kila mwaka zinatoka wanafunzi wengi zile nafasi za kazi zinachukuliwa na wageni kutoka nje ya nchi hii, kulikoni?

Je, chuo hakina uwezo wa kutoa wanafunzi bora ambao wenye uwezo wa kufanya kazi, kama wanao kwa nini zile nafasi ambazo wanapaswa wafanye kazi hata *human resources (HR)* , atoke nje ya Zanzibar au nje ya Tanzania, ushahidi nnao. Taasisi mbali mbali kuna *human resources* kutoka nje ya Tanzania Wakenya wapo pale, Waganda, inakuwaje wana vigezo gani, kazi ambayo wanaweza kufanya Wazanzibari waliosomeshwa na wazee wao wengine na serikali hii, lakini nafasi zile hawazipati, tatizo liko wapi. Nitakuomba sana juu ya usimamizi wa Chuo chao hichi kuona tatizo hili kwamba angalau lipungue, kumalizika kabisa tatizo, basi angalau lipungue ili tuone kwamba wale waliosomea kada ile wanapata nafasi katika zile sehemu zinazohusika.

Leo hii ukenda upande wa Kaskazini Unguja asilimia 98 au 97 yote HR ni wageni. Lakini wakati pale kila siku tunahitimisha watu wa kada hii. Je, tatizo ni nini, nitakuomba na hilo uje unambie vizuri ili niweze kupitisha bajeti tu, kwa sababu bajeti haina shida sana.

Niende kwenye suala la Haki Miliki, vijana wetu wengi wa upande wa wasanii wamesema bado halijakaa sawa. Japo ulikuwa na vipindi katika redio la televisheni sasa hivi naona na vile vipindi vimesita havipo. Angalau ilikuwa vinaelimisha watu kupitia vipindi vile kuona namna gani hawa wasanii wetu katika suala zima la haki miliki wanavyofaidika na kazi zao. Imekuwa kazi zao zinarudufiwa ovyo, watu wanaziuza bila ya wao wenyewe wavuja jasho kuweza kujipatia kipato. Nitakuomba sana kwa sababu hii taasisi unayo mwenyewe katika Wizara yako, uliangalie kwa kina kabisa hili suala *at least* wale wavuja jasho wetu wafaidike. Tusiwatumie tu kwa baadhi ya mambo lakini baadhi mambo juu ya maslahi yao yakawa hayatekelezwi, itakuwa hatuwetendei haki. Naomba sana serikali sikivu, Waziri msikivu, ni mwalimu ambaye unahuruma na watu wako katika hilo nitakuomba sana uzidishe huruma tuone wale watu namna gani wanafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika G04 Mkurugenzi wa Mashtaka. Pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na taasisi hii lakini bado malalamiko yapo. Malalamiko yaliyokuwepo pale juu ya kadhia nzima ya upelekwaji wa majalada katika Mahakama zetu kwenda kufunguliwa zile kesi. Polisi kazi yake kukamata na kupeleleza anapeleka pale lakini pale inachukua muda mwingi sana. Inafikia *time* hata inahatarisha hata ile imani kwa wananchi wetu kuondoka. Nakumbuka mimi nilikuwa nadhaa ndogo kwenye jimbo langu pale nafikiri kama sio kupata nguvu kwa kwenda mimi mwenyewe kuifatilia ingefika miaka bila ya kupelekwa Mahakamani.

Lakini mara baada ya kwenda pale wiki iliyofuatia tu ile kadhia ikapelekwa Mahakamani. Nyinyi nyote mashahidi mnafahamu ile kadhia iliyomkuta kijana wetu kule jang'ombe kwa Mpendae na nashukuru baada ya kwenda pale nikauliza tatizo nini, nikafahamishwa na nikaona baada ya muda mdogo kupelekwa Mahakamani ni kazi yao. Lakini tusikae tukasubiri kama mtu hana uwezo wa kufika pale ikawa yale mambo hayafiki Mahakamani. Yanakawia sana, kuna mrundiko mkubwa sana wa kesi pale ambazo Polisi wameshazipeleka lakini bado tatizo la kwenda Mahakamani. Nitaomba kujua pale kuna muda gani ambayo kupokea jalada, kujiridhisha na uchunguzi ili kesi iende Mahakamani ni siku ngapi, mwezi, miezi miwili, siku moja au siku mbili, nitaomba sana hilo linilipata ili kuweza kuangalia dhana nzima ya kuondoa matatizo ya mrundikano wa DPP kupeleka kesi zetu mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sio hivyo tu Afisi ya DPP bado inafanya kazi kama 79, 78, kwa sababu hata vyombo vya kuhifadhia zile data zao bado tunatumia mabuku. Ifike *time* sasa hivi dunia inatumia teknolojia, pana uhaba wa vitendea kazi pale. Imekuwa Makarani wa pale mpaka dakika hii kesi zile wana-*file*

katika mabuku na ma-*file* ambayo sio taratibu nzuri kwa muda huu kutokana ulimwengu unavyotupeleka. Lazima tupate vitendea kazi kwa ajili ya kuweka *data* zetu na kesi iwe rahisi kuweza kuendelea na shughuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, hata tatizo la usafiri kwa upande wa DPP nzima Ofisi ya Zanzibar pale Unguja ina gari tano (5) ina mahakama tano. Ukiondoa gari tano hizo gari moja anapanda Mkurugenzi, nyengine Msaidizi Mkurugenzi, gari tatu ndio za kuwasambaza ma-DPP wetu katika Mahakama Zanzibar, tuangalie umbali wa mahakama kuna Mahakama ya Makunduchi kuna Mahakama Mfenesini, Mahakama Mwera, Mahakama ya Mwanakwerekwe na Mjini kwa gari tano, bado vitendea kazi mmewaminya. Ningeomba sana Mhe. Waziri katika bajeti yako hii angalau basi wale watu uwaridhishe wapate usafiri ili iwe rahisi kufanya kazi kuweza kufika sehemu zao za kazi kiurahisi. Tatizo hilo lipo nimeona niliseme hapa kwa sababu hapa ndio pahali pekee ambapo penye kupitisha bajeti za matumizi katika taasisi mbali mbali za serikali.

Mhe. Mweneyekiti, nikiendelea mbele naomba nizungumzie suala zima la Tume ya Kurekebisha Sheria, nimsifu sana Mkurugenzi Mhe. Mshibe anafanya kazi nzuri sana ya kurekebisha sheria za nchi hii. Lakini bado kuna ukakasi wa Mwanasheria Mkuu kutuletea yale mabadiliko ya sheria. Kuna sheria sasa hivi zimepitwa na wakati. Kwa mfano sheria za mikataba hizi ni lazima zirekebishwe katika Baraza la Wawakilishi ili ziendane sambamba na mahitaji yaliyokuwepo sasa. Kuna sheria ya Ushahidi, kuna sheria ya *criminal procedures* ambazo hizi sheria tunaomba haraka iwezekanavyo zibadilishwe na ziletwe Barazani ili ziweze kuendana na mustakbali wa sasa katika suala zima la muelekeo au maendeleo ya mabadiliko ya nchi yetu.

Ningeomba sana sheria zipo nzuri, tuzisimamie ipasavyo inakuwa zogo lote hili litaweza kuondoka. Ningekuomba sana Mhe. Mwanasheria katika haya ufanye haraka iwezekanavyo ulete *amendment* za sheria hizi ili tuweze kuzibadilisha tuzipe nguvu zaidi kutokana na hali ilivyo kwa sasa. Ningekuomba sana hili suala ulichukue na iwe moja katika ajenda ya kuhakikisha kwamba hizi sheria tunazifanyia marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, ni-*declare my interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC, pale ilivyokuja kusomwa kuna kipengele ndio kwanza nikisikie jana kwamba kuwatambua wajumbe waliopitia Bajeti. Nathubutu kutamka kwamba mimi sikupitia bajeti na kwa sababu ya misimamo yangu ya kusimamia Kanuni ya Baraza la Wawakilishi. Nilisimamia Kanuni ya 96(3) iliyonipasa nipate mambo ndani ya muda wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Diwani, nakuomba sana ujadili hotuba iliyokuwepo mezani na kilichokuwepo hapa mezani masuala ya hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Suala la Kamati ya PAC ambayo imeleta ripoti wewe hukuwemo hilo suala itakuwa wewe na Mwenyekiti wako wa Kamati mtashirikiana pamoja na Spika ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. Kwa hivyo kwa hapa Mheshimiwa si pahala pake. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, napokewa busara zako lakini ikumbukwe kwamba tupo katika Baraza la Wawakilishi na kinachotuongoza ni Kanuni ya Baraza la Wawakilishi. Sipendelei kurudia huko lakini *message* imefika.

Niendelee katika suala la Mahakama niipongeze sana Mahakama inafanya kazi vizuri lakini bado kuna matatizo kwenye Mahakama zetu. Ukitilia maanani sasa hivi Mahakama inatanua matawi yake kuna Mahakama sasa hivi tunaambiwa Mahonda Mahakama ya Watoto, Mahakama ya Biashara, lakini bado kuna tatizo zima la Bajeti yao, kazi zinaongezeka lakini bajeti inapungua ....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Diwani una dakika tatu zilizobaki kwa hivyo nakuomba sana umalizie.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana naomba na dakika yangu moja uliyozungumza unilindie. Kuna kadhia hii ya bajeti yao kutokidhi haja. Mahakama imetanuka sasa imeongezeka *branch* nyingi sana, matawi mengi sana lakini bado bajeti inashushwa. Ningeomba sana Mhe. Waziri katika hilo. Si hilo tu, hata katika kada zetu zile za Mahakimu kuna Mahakimu wa Mwanzo, kuna Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mkoa. Naelezea zaidi juu ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo maslahi yao bado hayaendani sambamba, tofauti ni kubwa sana pamoja na pongezi za kuongezwa mishahara lakini nafikiri miaka miwili iliyopita iliongezewa mshahara lakini kwa kada hii ya Mahkama za Mwanzo bado. Ningeomba sana basi wafanyiwe kidogo uangalie angalau kwa jicho huruma tuone na angalau na hawa Mahakimu wa Mahkama ya Mwanzo wanawiyanawiyana na Mahkama ya Wilaya au kwa sababu viwango wa elimu takriban vinakaribiana *degree* lakini bado kidogo hawa Mahkama ya mwanzo yako chini yale maslahi yao, ningeomba sana Mhe. Waziri na hili ulichukuwe ili na wale wenzetu waweze kutenda haki vizuri.

Nende katika Tume ya Rushwa naipongeza inafanya kazi vizuri tunasikia ina kamata lakini bado rushwa bado nchi hii haijamalizika kuna mambo

yanafanyika mpaka utowe rushwa ndio uendelee juu ya suala kadhia nzima ya kupata tenda katika sehemu mbali mbali. Ni shahidi wa hilo nimekutana na Mkurugenzi wa Rushwa kwa mambo ya masuala haya na kaniruhusu nende na nataka kwenda kumpelekea vigezo vizima jinsi gani tenda katika taasisi zetu zinavyochukuliwa kama hujatoa mlungula huwezi kupata tenda zile ukafanya kazi zako. Ningeomba sana Mahkama ya Rushwa iwe na meno makali katika hili na wanapopata taarifa dakika wafatilie kufanikisha ili kuweza kufanikisha kuona namna gani watu wetu wanafarijika.

Najua wataka kunambia nimalize nashukuru sana kwa muda huu niliotumia, siungi hoja mkono moja kwa moja nasubiri majibu ya Mhe. Waziri yatakaponirisha nitaunga mkono hoja. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdulla Diwani kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Zulfa Mmaka nafasi wa wanawake akifuatiwa na Mhe. Hamad Abdalla Gerey na Mhe. Simai ajitayarishe.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa wetu Mwalimu Haroun.

Mheshimiwa mimi nianze katika sehemu ya hizi sheria nimuombe sana Mhe. Waziri kipindi kilichopita hapa tulikuja na hoja zetu binafsi kuhusu masuala ya udhalilishaji lakini sasa hapo hapo ambapo tulileta malalamiko yale Mheshimiwa tunatoa malalamiko mingi lakini tukienda ndani tunakuta kwamba sheria hizi ambazo zinahusiana na makosa haya zimepitiwa na wakati.

Mheshimiwa pale kuna sheria namba 6 ya Sheria ya Adhabu, Mheshimiwa kwa kweli sheria ile imetungwa tokea mwaka 2004 kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri sheria ile imeshapitwa na wakati pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sheria namba 7.

Mheshimiwa alitupa ahadi kwamba sheria zile atazileta hapa lakini hadi leo sheria zile hazijaletwwa hapa kwa ajili ya kuzibadilisha. Nimuombe sana Mhe. Waziri sheria hizi azilete kwa sababu unakuta kwamba kuna makosa mengi sana ambayo yanatendeka mwisho wa siku unakuta adhabu zake ni ndogo sana. Unakuta mtu kabakwa lakini sheria inasema afungwe miaka saba au miaka mitano kwa kweli sheria hizi zinatukandamiza sana, kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili alingalie na atuambie ni lini sheria hizi atazileta katika Baraza hili ili tuweze kuzirekebisha ziendane na wakati uliopo. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa tukienda hapo hapo juzi moja nilisikiliza redio unakuta kwamba sisi tunalaumu katika hizi sheria tunasema kwamba wale wahusika wa udhalilishaji wasipewe dhamana lakini sheria inawataka kwamba wale watu wapewe dhamana. Kwa hivyo sasa inakuwa kwamba tunalaumu lakini kulaumu kwake ni bure kwa sababu sheria hazijaletwa, kwa hivyo nimuombe sana Mheshimiwa kwa kweli naamini kwamba suala la udhalilishaji yeye mwenyewe pia binafsi halitaki lakini pale ambapo atakaa chini na kuletea katika Baraza hili ili tuzibadilishe ndio ule msemo wa kwamba hazitaki ndio tutamuamini kuliko kukaa na zile sheria katika vitabu na zikaendelea kufuatwa vile vile na wanasheria wetu katika kutoa hukumu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Ofisi ya DPP Mheshimiwa mimi katika Ofisi ya DPP na maswali machache ambayo nataka niyazungumzie. Mheshimiwa katika Ofisi ya DPP nianze la daraja ambalo Mheshimiwa pale katika ofisi ya DPP kuna wanasheria ambao wanafanyakazi zao tafauti, wanasheria wale katika ofisi ile wako katika madaraja tofauti na kila ambapo wanapanda madaraja stahiki zao na posho zao zinabadilika. Mhe. Waziri pale pana wanasheria ambao tayari wameshabadilishiwa kada moja kutoka *Junior* kwenda *Senior* au kutoka daraja moja kwenda ya pili mpaka tatu lakini la kushangaza hadi leo wanasheria wale posho za bado hazijabadilishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa kwa kweli wanasheria wanafanya kazi nzito ambayo na lawama juu tunawapa, Mheshimiwa wanasheria wanahitaji kubadilishiwa posho zao zile ili kujikimu na makosa ya kesi zile nzito na kazi zile nzito ambazo wanazifanya. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri aniambie ni sababu zipi zilizopelekea wanasheria wale wakawa hawajabadilishiwa posho zao zile na pia nimuombe Mhe. Waziri aniambie ni lini posho zao zile zitabadilishwa na zikisha kubadilishwa je, kuna utaratibu gani wa kulipwa *area* zao za posho zile ambazo kwa kipindi kirefu hawajapewa.

Mheshimiwa mimi hapa naomba uniletee jibu zuri sina nia ya kupiga buti lakini nina nia ya kupunguza hichi kifungu ili nipate majibu yangu yanavyoenda. Nikienda hapo hapo katika suala la DPP. Mhe. Waziri kwa kweli Ofisi ya DPP Pemba ina matatizo mengi sana. Tukianza tatizo la jengo Mheshimiwa pale walikuwa na jengo moja ambalo walikuwa wana kodi kutokana na pesa zao nadhani sio nyingi ki hivyo wakashindwa kukaa katika jengo lile Mheshimiwa na sasa hivi wamehamia katika nyumba sio ofisi.

DPP ni ofisi ya heshima ni ofisi kubwa ambayo sisi sote tunaiangalia kwa macho mengine kesi zetu zote zinapelekwa pale lakini unakuta kwamba watu

wale wakaa katika nyumba siyo ofisi nyumba ile iko finyu, haistahiki kuwa ni ofisi na bado wako pale. Kwa hivyo, nikuombe Mheshimiwa wale wana kiwanja chao kwa nini katika bajeti hii na wao usiwafikirie kuwajengea kila kiwanja chao na amini katika majibu unaweza kuja kunambia lile jengo ambalo linajengwa kule Gombani na wao wataingizwa mule.

Lakini Mheshimiwa nikwambie kwamba hilo eneo ambalo kwamba kupewa hata wakaingizwa hao DPP itakuwa bado tunawaonea kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa kiwanja wale watu wanaocho wapangie basi bajeti yao na wazo wajengewe jengo lao '*mcheza kwao hutunzwa'* kazi wanazozifanya ni nzito, tuwape sehemu salama watakapokaa kufanya kazi zao kwa ufanisi. *(Makofi)*

Nikitoka hapo niende suala la DPP pia Pemba suala la usafiri. Mheshimiwa DPP wana gari mbili mbovu wale wana mahakama nyingi wanakwenda Chake Chake, Mkoani, Wete. Mheshimiwa unamkuta kwamba mtu ambaye anakwenda mahakama ya Mkoani anakwenda kwa vespa kwa kweli wale wanasheria wanakuwa watu wengi sana hasa hawa ambao wanakuwa mabalaa balaa wanakuwa wanawachukia hivi Mheshimiwa vespa mtu wa DPP anakwenda na vespa kabeba majadala kabeba na mambo mengine jee watu wakiamua kumhujumu mtu kama yule na kumuumiza lawama tutampelekea nani.

Tukimaliza hapo Mheshimiwa hizo gari mbili ambazo wako nazo ni mbovu kwenda leo tukasema tunaenda kuzitizama Mheshimiwa kupewa *lift* unaona tabu gari zile zishatoka pele, gari zile kila siku gereji hebu Mheshimiwa nikuombe sana suala la usafiri hebu waangalie na wao unakuta kama mwisho watumia usafiri wao kwa ajili ya kwenda mahakamani na sehemu nyengine. Kwa hivyo nikuombe sana katika bajeti yako uangalie na wao wale watu uwapatiwe vipando uwanunulie gari ambayo inaenda na wakati, kwa sababu tukiangalia hata hapa Unguja wana kibasi kimoja wanapanda humo humo kwa kweli hatuwatendei haki wanasheria wetu katika Ofisi ya DPP. Kwa hivyo nikuombe sana Mheshimiwa hii Ofisi ya DPP tunaitegemea kwa ajili ya kutufanyia kazi zetu kwa hiyo kwa kuwapa motisha Mheshimiwa suala la posho wabadilishie na suala lao la usafiri wawekee sawa kidogo ili waweze kufanya kazi zetu bila la kupokea rushwa nje.

Waheshimiwa nikitoa hapo niende katika Tume hii ya Utumishi masuala ya uajiri, Mheshimwa kwa kweli sisi vijana wawakilishi wa vijana tunapata tabu sana kwa wapiga kura wetu inapotokea nafasi za ajira. Mheshimiwa Tume hii siye hatuna imani yao kwa sababu ajira zinatangawa tu redioni lakini mimi niseme kwamba kutangazwa redioni ni kupoteza pesa za Serikali kwasababu

ajira zile zinapotangazwa redioni inakuwa tayari washatafuta watu wao wa kuwaajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa sasa kuna haja gani ya kutangaza redioni Mhe. Waziri mimi nina uhakika kwamba nafasi zile wanazitangaza kwa utashi lakini siyo sheria ambayo imepangwa, tunakuta Wizara nyingi sana tu. Mhe. Waziri kama wewe huna wizara ambayo watu wana wanaishuku mimi naomba uje unifate tukae chini nikwambie kuna Wizara fulani wameajiri watu wao ambao pale walitoa ajiria kama nne, tano pale kajiriwa mtoto wa Afisa utumishi, pale kaajiriwa sijui mtoto wa Afisa Mdhamini, kaajiriwa sijui mtu wa nani hasa kwa hiyo sisi tutakuwa hatuna imani ya kupeleka hizo barua tunapoteza muda wetu. *(Makofi)*

Na kilio hiki kila siku tunakwambia kwa hivyo tunakuomba tunakuomba tena Mheshimiwa sasa hivi kuna ajira zishatangazwa lakini vijana hawapeleki barua kwa sababu hata wakipeleka barua ni kazi bure. Mheshimiwa kwa kweli Tume sijui inafanya kazi gani inatutafutia siye matatizo na wapiga kura wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tume yako inatutafutia siye hapa tusirudi tena lakini sawa ila hatutokubali. Kwa hivyo nikuombe sana Mheshimiwa hii Tume kaa nayo chini kwa sababu nahisi kama wanapelekeshwa na hawa watu wa mawizara, wanatoa ajira lakini mtu anakwambia mimi napendekeza mtu wangu huyu na huyu na huyu, jamani wale walala hoi wataajiriwa lini? Wakwezi na Wakulima kwa kweli watabakia kula vumbi tu kwa sheria hii ambayo tunaifata. *(Makofi)*

Nikitoka hapo niende katika suala la utengenezaji wa Mahakama nimpongeze sana Mhe. Rais anazipenda Mahakama na Mhe. Waziri ulipendekeza ile Mahakama ya Chake kufanyiwa marekebisho makubwa. Lakini Mheshimiwa niulize, hivi ile Mahakama ya Chake ni Mkandarasi gani ambaye amepewa kazi ya kurekebisha lile jengo? Kwa kweli Mheshimiwa mimi niende moja kwa moja niseme kwamba lile jengo ni *failure*.

Lile jengo limetumiza pesa nyingi kurekebishwa lakini sasa kilichofanyika ni sawasawa na kuchukua kidonda ukenda kukipiga dawa juu au plasta juu ukasema kwamba kimepoa ni uongo tunajidanganya. Mheshimiwa lile jengo tokea lifunguliwe hata mwaka bado haujatimia lakini sasa hivi nakuomba utoke uende kuliangalia jengo lile lina pele, lina keya, lina kila njia chafu. Mheshimiwa keshokutwa jengo lile tukienda tayari limefanya *chipping* na jengo lile halikutiwa *chipping* limetiwa rangi kilichofanyika pale ni kutia *gypsum* juu na rangi, kwa kweli pesa za Serikali Mheshimiwa tunazitumia vibaya. *(Makofi)*

Lengo la jengo lile ni kutengenezwa sio kuficha watu machoni tu kujificha mgongo wazi. Kwa hivyo nikuombe sana Mheshimiwa unieleza jengo lile ni Mkandarasi ambaye mumempa kazi ile ya kulitengeneza jengo lile na kuliharibu na pia unambie kama ni kweli jengo limeharibiwa ni adhabu gani ambaye utaitoa kwa Mkandarasi huyu ambaye katuchukulia pesa zetu bila ya kufanya kazi ile ambayo tumemtuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa mimi ninung'unike sana kwenye suala hili la uajiri wanatufanyia vibaya na watatupotezea sifa zetu sisi Umoja wa Vijana ambao tumekuja hapa tunawatafutia ajira moja mbili, ni bora hizi ajira ziwe hazipo moja kwa moja kuliko kuletwa halafu zikawa na mambo mengine, kwanini Mheshimiwa hawafuatwi watu wengine.

Mimi Mheshimiwa hapa hapa nimsifu DPP Mheshimiwa DPP anapelekewa nafasi za ajira lakini DPP nafasi zile za ajira anazitoa zitakiwavyo, mimi naamini pale anaajiri watu kutokana na sifa za kwa nini na wao wasiende kwa huyu DPP wakenda kujifunza jinsi ya kuajiri watu. Kwa kweli Mheshimiwa mimi sina nia kuharibia hii hotuba yako napenda sana ipite kwa ajili ikipita hii na pesa humu ambazo umezitaja naamini wanasheria wetu watanufaika na wakinufaika na wao katika Baraza hili kuna na watu na wao watanufaika napenda sana. *(Makofi)*

Ila kwa kukaa kitako nakuomba sana Mheshimiwa masuala ambayo tumeyazunguza yaangalie sana ili tupate kukupitisha vifungu vyako hivi vya pesa tupate kwenda kujipongeza.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. sana Mhe. Zulfa kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Hamad Abdalla Gerey akifuatiwa na Mhe. Simai na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajitayarishe.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii adhimu kabisa katika Baraza lako Tukufu kuchangia hotuba hii ya Mhe. Haroun Ali Suleiman Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao kwa kweli wametupa kitabu ambacho kina maandiko mazuri yaliyopangika hasa ukitilia maanani na sisi kazi yetu ni kutilia nyama ili kuhamasisha na kufanikisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja kwanza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa naipongeza wizara kuanzisha Mamlaka hii ambayo kwa kweli inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha katika nchi yetu rushwa inaondoka kabisa na kwa kiasi kikubwa imeweza kupungua tokea ilipoanza kuundwa Mamlaka hii.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka hii na kama ilivyoainishwa katika kwenye kitabu hiki imeweza kuokoa hata fedha kwenye meli yetu mpya ya MV Mapinduzi mimi naipongeza sana. Lakini napenda kuitanabahisha hii Mamlaka kwa sababu mara nyingi inafanya kazi kwa kusikiliza watu na imeonekana zaidi kwamba mara nyengine kuna hali ya chuki tu mtu kwa mtu anaichomekea hii Mamlaka ya Rushwa na anaweza kukamatwa yule mtu kwa sababu ya shindikizo la mtu. Ningependa kuishauri Mamlaka iwe makini katika kufanya kazi zake hizi kwa sababu imeshatokezea kwa sababu ya chuki ya mtu anamsingizia mwenziwe na Mamlaka inakuwa rahisi kutoa fedha zake za mitego mtu yule akakamatwa kumbe kile kitendo si cha kweli kabisa ni chuki ya mtu tu.

Napenda kumshutua Mhe. Waziri kwamba awe makini na hii Mamlaka tusikubali kushawishiwa kufanya kazi kwa kushawishiwa tufanye kazi kwa uhakikia na kuthibitisha hasa kwamba yule mtu sio kasingiziwaa rushwa kwa maana ya chuki ya mtu, lakini iwe kweli kathibitika na kuchukua rushwa hasa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kazi yake kubwa ambayo katika kitabu imeeleza hata imeweza kuokoa fedha za Kombe la Mapinduzi Cup na niipongeze Mamlaka lakini nirudie tu kuitanabahisha kwamba isiwe tayari kufanya kazi kwa kusingiziwa ifanye kazi kwa nguvu yake na uwezo wake hasa na mafunzo waliyoyapata ili kuepusha watendaji wetu wazuri pengine wengine wakatiwa doa, viongozi wetu wazuri wakatiwa madoa isikubali kurahisha jambo hilo, ipeleleze vizuri na waweze kuthibitisha na pale watakapo amua kumpeleka mtu kwenye vyombo vya sheria basi iwe ni kweli yule mtu kahusika na lile jambo linalohusika.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Chuo cha Watumishi wa Umma kwanza nipongeze Wizara, hiki Chuo kimeleta muamko mkubwa na wanyakazi pamoja na wasomi wameweza kujiunga na Chuo hiki katika kuhakikisha kwamba wanapata elimu ya kutosha katika kuleta ufanisi wa kazi zao kwenye maofisi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti niseme tu Chuo kina tawi lake Pemba na bahati nzuri kimo ndani ya Jimbo langu nampongeza Waziri Chuo kile kukileta kwenye Jimbo langu lakini niseme tu kile Chuo humu ndani mimi sijaona fungu lake la

kutengewa kile Chuo hususan Tawi la Pemba. Kwa kweli kile Chuo Mhe. Waziri pale Pemba kiko Wawi kabisa ndani kule na sasa hivi kina jengo la kuazima tu, yaani ni sawasawa kusema wanadandia dandia kwa sababu siyo mara ya kwanza kuhama, ningependa kumuomba Mhe. Waziri kile Chuo wasikiweke kama mtoto wa kambo ni Chuo kizuri wananchi kule Pemba na wafanyakazi wamekiunga mkono na wanajiuinga kwa wingi na juzi juzi tu walinialika katika mahafali yao. Nimeona lakini kuna matatizo mengi Mhe. Waziri, kunamatatizo ya njia ambayo toka ipite hii dhahma ya mvua ile njia sasa ndio imechafuka hasa mpaka Mwakilishi wa Jimbo lile naomba basi tushirikiane mimi na Wizara yako na Wizara ya Usafirishaji na Ujenzi ile njia tuipitie tuifanyie maekebisho kidogo, ili wanafunzi wetu wale waende kule kwa raha kwa sababu lengo lao ni kupata elimu ambayo itaongeza ufanisi wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nije upande wa takwimu sasa ambazo Mhe. Waziri katika kitabu chake amezileta ambazo wenzangu huko nyuma walishaanza kuzitilia mashaka takwimu zile. Na mimi nitilie mkazo tu kwamba zile takwimu zinaonesha dhahiri kwamba si za uhakika, na kama alivyoomba mwenzangu ni vyema basi Mhe. Waziri na watendaji wake wangekaa kitako wakatupa takwimu za uhakika. Na mfano mwengine ukiondoa ule ambao amepewa mwenzangu kitabu ni kizuri, kimepangwa vizuri kwenye ukurasa wa 70 kuna vipengele pale ambapo vinaonesha wazi kila wizara kuna wafanyakazi ambao wathibitishwa kazini, wenye nyongeza ya muda wa kazi, uajiri wa mkataba, kustaafu kwa maradhi, kustaafu kwa lazima, kustaafu kwa hiari, likizo bila ya malipo, kubadilishwa kada, kuacha kazi na kufukuzwa kazi. Napenda nimwambie Mhe. Waziri ingekuwa vizuri basi kikaongezwa kipengele kingine pale waliosimamishwa kazi, mimi najua wapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa huu hakipo kile kipengele, wapo waliosimamishwa kazi ambao bado wanasubiri kesi zao ziendelee, lakini hapa hawakuwekwa. Ningependa kumwambia Mhe. Waziri arudie tena kama alivyosema mwenzangu wakae vizuri na watupe takwimu nzuri na za uhakika ili tuweze kuelewa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye tofauti sasa ya mishahara ya wafanyakazi wetu. Kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa nyongeza ambayo kwa nia njema kabisa kaamua kuwaongeza wafanyakazi wa kima cha chini ili kuleta ufanisi kwa wafanyakazi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nyongeza hii kidogo ina utata utata kwa wafanyakazi wengine wa juu ukiondoa wale wa kima cha chini. Na inaonesha dhahiri kwamba kuna marekebisho madogo madogo ambayo watendaji bado hawajayaweka sawa. Namshukuru Mhe. Waziri kuna maelekezo wafanyakazi wetu wamepewa kwamba yule ambaye anahisi nyongeza yake haiko vizuri basi aende kwa Afisa wake wa Utumishi ili apatiwe marekebisho. Jambo hili nalipongeza sana na ningeomba wafanyakazi wote wa nchi yetu wasinung'unike pembeni kwani serikali haina nia yakuwanyanyasa au kutokuwalipa mshahara mzuri, Rais kwa moyo wake kaongeza nyongeza ile lakini kama kuna matatizo basi warudi kwa watumishi kama ilivyoagizwa na serikali waende wakaeleze wazi matatizo yao ili na wao warekebishiwe. Wasivunjike moyo kutaka kuacha kufanya kazi au kutokufanya kazi kwa nia njema, hapana kwani bado serikali ina nia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika kitabu hiki, narudia tena kumpongeza na watendaji wake bado ofisi hii ina matumaini makubwa kwa wafanyakazi wake na kwa serikali hii. Mhe. Waziri kuna matatizo madogo madogo juu ya Mahakamani kama aliyoyasema mwenzangu aliyetangulia ambayo yanahitaji usimamizi mzuri na ufatiliaji ili kuondoa zile kasoro ndogo ndogo. Na kuondoa kasoro zile kama alivyosema mwenzangu ni mwanzo wa kupata mafanikio ya wananchi wetu na sisi wenyewe pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya hayo niipongeze hotuba ya Mhe. Waziri na naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamad Abdalla Rashid sasa namuomba Mhe. Simai Mohammed Said akifuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo na mimi kuwa mmoja katika wachangiaji hawa. Lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii leo tukiwa hai na uzima wa afya kufika hapa Barazani kuweza kutimiza majukumu yangu, kwa niaba ya wananchi ambao mimi ninawawakilisha hapa katika jimbo letu la Tunguu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kweli Mhe. Rais hajafanya makosa, hajakosea Mhe. Ahmada ni mwana CCM, amekuwa mtetezi wa Chama chetu cha Mapinduzi Wazungu wanasema *this is the man who can take a bullet for you,* yaani kama unataka kupigwa

risasi basi anakuwa yuko mbele yuko tayari kupigwa akae mbele kukilinda chama kwa maslahi yote. Na Mhe. Ahmada tuliwahi kufanya kazi wote katika Kamati ya Kujenga ule ukumbi wa Mkoa wa Mjini pale Amani na leo mkiona yale mabati yote juu yalivyoekezwa basi ni utaalamu. Kwa hivyo, nimpongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mhe. Ahmada ambae tuko nae hapa, naomba sasa nimpongeze pia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya suala zima la kuazinsha pensheni kwa ajili ya wazee, lakini pia kuongeza mshahara wa kima cha chini kwa watendaji wetu kufikia hicho kiwango ambacho kilichotajwa na kinazungumzwa. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mchango huu umekuwa unazungumziwa na Mataifa mengi sasa hivi ndani ya Bara la Afrika, lakini pia na maeneo mengi watu wanafurahia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo sasa naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu nitaanza na Jaji Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia katika kitabu cha bajeti suala zima la fedha na mafungu yalivyopangwa. Naomba sana nishauri kwa fedha ambazo zitakuwa zinatumika kwa ajili ya maslahi hasa kwenye mambo tofauti hasa safari basi kama itawezekana Jaji Mkuu nae apelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali akiwa yeye pia ni alama ya muhimili kama Spika wetu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Rais mwenyewe.

Lakini pia nimejaribu kusikiliza katika michango tofauti ya wajumbe tangu Baraza hili na huko nyuma. Mhe. Mwenyekiti, hakuna jambo limekuwa linazungumzwa sana juu ya maadili ya Wazanzibari kuporomoka kwa maadili yetu na kujaribu kufanya au kutanganua kuangalia ni yapi ambayo yanasababisha. Mhe. Mwenyekiti, suala la maadili kwanza itambulike kwamba maadili au malezi ya watoto ni *parental guidance* ni wazee ndio wenye *responsibility* au jukumu ya kulea watoto wao. Sasa Zanzibar tunapokea wageni wengi, kuna wageni wanakuja kibiashara, kazi na pia kuna wageni wanakuja hapa ni watalii. Wakati mwengine watu huzungumzia kwamba kuunganisha maadili yetu pamoja na sekta hii muhimu au sekta mama ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, nikuhakikishie na pamoja na Baraza lako tukufu kwamba wageni wanapotaka kuja Zanzibar wanakuja hapa ili kwa kupenda visiwa vyetu na kujifunza na kuona yale ambayo tuliyokuwa nayo sisi kama historia yetu. Sasa unapomkuta leo kijana anaendesha hivi vi-*vespa* au *passola* ana miaka 14 je, mwenye makosa ni mtalii au mlezi wa yule mtoto? Unapomkuta mtoto anatembea usiku mwenye umri chini ya miaka 18 au 21 kwenye saa 3:00

mpaka saa 5:00 za usiku je, ni mtalii au ni mlezi wa mtoto mwenye jukumu la malezi na yule mtoto? Unapomkuta mwanafunzi mwenye umri chini ya miaka 15 anatumia simu hizi za kisasa ambazo umaarufu wake ni *smartphones* ambazo zinakupa *access* na taarifa za kila aina. Je, tatizo ni mlezi au mtalii? Sasa Mhe. Mwenyekiti, tuwe makini sana katika suala hili zima, tujaribu kutofautisha juu ya malezi yetu na watoto wetu na katika mawasiliano na mambo ambayo dunia imezidi kuwa sasa karibu. Kama wanavyozungumza sasa dunia ni kijiji taarifa zote ziko hapo hapo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi natumia hiki kidubwasho kinaitwa *iPad* humu ndani unaweza ku-*access* mpaka mtu alipokuwa sasa hivi maeneo tofauti anatembea ukamuona. Mimi marehemu mzee wangu alikwenda kutembea Urusi mwaka 1977 akaingizwa kwenye chumba hicho kimoja, alipoingia mule ndani na hii *story* alinihadithia mzee wetu nitamtaja kwa jina, sina tabia ya kutaja watu majina lakini alinihadithia mzee wangu mmoja. Akaniambia akachukuliwa ndani akaoneshwa angalia, anaangalia kwenye *screen* kubwa anaoneshwa Zanzibar, Rais wa Zanzibar anatoka Ikulu anakwenda zake kwenye mapumziko. Ma-*satellite* juu yamekaa yanagongana sasa hivi juu huko kuna uchafu kibao, ukienda kwenye *space*. Taarifa sasa hivi kuzipata mkononi ni rahisi *access to information*.

Mhe. Mwenyekiti, simu hii zamani ulikuwa mtu ukitaka kupiga picha inabidi uwe na *camera*, siku hizi simu moja unapigia picha, unarikodi sauti, unaandika *notice* zako zote ambapo zamani tukiandika kwenye *filofax*, unaweza wewe kurikodi chochote, kuna taarifa za kila aina una-*access apps* kibao dunia yote iko pale pale. Leo kijana ambaye anatumia hii simu anaweza ku-*access* taarifa ambazo hatakiwi kuziona kutokana na umri wake. Sasa mwenye makosa ni nani? Mimi naomba sana Mhe. Waziri utapokuja utilie mkazo masuala ya malezi ya watoto na umuhimu wake na sisi sote humu ndani ni wazazi tuweze kuchukua jukumu la kuhamasisha watoto wetu na wananchi wetu katika jamii kufata yale ambayo yanayostahiki. Na hili ukiangalia linatakiwa liende sambamba na wizara ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kule kwa Mhe. Maudline Cyrus Castico.

Mhe. Mwenyekiti, na tusipokuwa makini tutajikuta tumekaa kati kati ya uwanja tunapigana mabao tunanyoosheana vidole hatujui tulipotoka. Leo *phonograph* watoto wa skuli wanaiangalia unatafiri wanaangalia mpira mechi ya Simba na Yanga, tuweni wakweli. Sasa anayeruhusu mtu kuangalia hizi *website* ni nani? Kwa hiyo, tunapokaa hapa tunalaumu kuhusu taarifa watoto wanaangalia mambo ambayo yasiyostahiki, wale ambao mnatumia *DSTV* ambayo ni *digital satellite television* pale juu kama kuna sinema usiku inaandikwa *PG8*, maana

yake *Parental Guidance8*. Unapoangalia mchezo unawekwa juu *PG15* maana yake mtoto mwenye umri chini ya miaka 15 hafai kuangalia.

Kwa hiyo, masaa ya watoto huwezi kumlinda uhuru wake mtu, lakini ni vizuri watoto ambao mnatoa vipindi katika *TV*, majarida ambayo mnayatoa muhamasishe wazee kwamba nyakati za jioni na haya mambo yanayotokezea watoto wawe wameshafika nyumbani. Mimi nilipokuwa na miaka 10 ikilia honi niko juu ya meza nafanya *homework* yangu, leo mtoto ana miaka 10 yuko nje mpaka baada ya Sala ya Isha anafanya nini, na kwa nini, na wazee wake wapi, masheha na majirani wako wapi mbona hawakemei haya. Sasa katika malezi ya watoto turudi nyuma tuchukue jukumu letu sisi na tusikae tukanyoosheana vidole.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka nizungumze suala dogo juu ya mikataba ya Kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe tahadhari na utaalamu ambao Zanzibar uko nao juu ya suala zima la sheria, na hasa katika sekta ya mafuta na gesi. Najua serikali ina siri zake, serikali ina mikataba yake lakini naomba sana hasa Mwanasheria Mkuu na *Chambers* wote kama wanahitaji kujifunza utaalamu zaidi kupitia mikataba yetu hasa juu ya mafuta na gesi, basi wasichoke kwenda pahala kuuliza unajifunza kwenda kusoma na kutafuta zaidi hiyo elimu ambayo inayohitajika. Tusije tukaingia katika mikataba baadae tukajikuta tuko pahala na migogoro.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mafuta na gesi suala hili ni kwa ajili ya kuhakisha rasilimali hii tutailinda kwa nguvu zote sisi kama viongozi hapa wa kutunga sheria pamoja na serikali na Mahakama kuhakikisha kwamba kwa ajili ya vizazi vijavyo hii rasilimali kama tutaipata Zanzibar maana yake bado hatuna uhakika kama tunayo, lakini habari inasemekana kwamba tuna nafasi nzuri ikaonekana, na siku ambapo Mhe. Waziri wa Nishati na Maji na Ardhi atakapokuja aje pia na taarifa kutueleza kila hatua awaeleweshe Wazanzibari na Watanzania tuko wapi. Na yote haya ni kwa ajili ya *transparence* wananchi wafahamu mikataba iko hivi, lakini kwa yale ambayo tunayostahiki sisi kufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la mkonga wa Taifa (*fiber optic*) mwaka jana nilizungumza sana suala hili, nilizungumza nikapigwa danedane katika wizara tatu. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, nikazungumza kwenye suala Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara hii ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma. Sijui Mhe. Mwenyekiti, waziri mwaka huu ataniambiaje kwenye suala zima la mtandao wa mawasiliano la *E-government component* yake bado ipo, fedha alizotumia ni nyingi. Kwa

hvyo, Mhe. Waziri utakapokuja hapa ujitayarishe vizuri na unipe taarifa ambayo ili wananchi wangu na Wazanzibari wakuelewa juu ya serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la *CAG*. Mhe. Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mbili ziliungana mwaka 1964 zile *publics* mbili tuliungana ya Tanganyika na Zanzibar kufanya *republic* moja. Mikutano ya Kimataifa ambayo *CAG* wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Tanzania Bara anayoshiriki kuna kila sababu na sisi *CAG* wa Zanzibar nae pia akawa anapata hadhi yake na kuweza kushiriki katika mikutano hiyo ikiwa ni Afrika, ikiwa na maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kwenye suala la *CAG* nataka nifahamu pia katika wale vijana ambao wanatumika na makampuni binafsi kwenda kufanya *auditing* katika taasisi za serikali ni vijana wangapi sasa tumeweza kuwajengea vipaji na utaalamu ili waweze sasa kufanya masuala yote haya ya auditing katika taasisi za serikali kwa pamoja. Nimeona katika buku lako Mhe. Waziri umezungumza suala la *Case Management System ambayo* ni CMS. Sasa nataka nifahamu kwenye suala la hii *CMS* pamoja na *E-government* unataka kuiunganisha vipi huko miaka ya mbele ili Wazanzibari kesi zao ziweze kwenda kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niulize suala moja, suala la Mahakama Kuu ambayo inatarajiwa kujengwa katika Jimbo langu la Tunguu. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika bajeti utakuta kule kulitengwa milioni 100, milioni 100 ambayo imekwenda wizarani moja kwa moja. Sasa je hii fedha tayari wameshakabidhiwa Mahakama kwa ajili ya kuanza ujenzi na mambo ya matayarisho ya awali? Na kwa nini fedha hizi zinapitia wizarani, hakuna fungu lake la kwenda kwenye Mahakama moja kwa moja?

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nimuombe sana Mhe. Waziri anakuja kuleta ujenzi mpya katika Jimbo la Tunguu nimesema jana hapa Jimbo la Tunguu pale katika Tunguu Mji Mpya tuna vyuo vikuu na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo nyumba yake pale ya makaazi yake, tuna Bunge, kuna Ofisi ya Mambo ya Ndani Uhamiaji, tuna Ofisi ya Mkoa, Makao Makuu ya Polisi ya Mkoa eneo hilo hilo na leo tunaletewa Mahakama. Lakini Mhe. Mwenyekiti, barabara zetu mule ndani bado haziridhishi, haiwezekani Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano anapofungua dirisha lake kuangalia mbele anaona tope tupu, njia mbovu haipendezi.

Kwa hivyo, mimi niombe sana Mhe. Waziri vinapokuja vipaumbele katika maeneo ya kuyapeleka nina kila sababu ya jimbo langu la Tunguu kwenye

barabara za ndani hasa katika Tunguu Mji Mpya ili wapate nafasi hizi basi njia zitengenezwe. Hizi njia zitengenezwe kwa mujibu wa taratibu na vipaumbele vya serikali, viongozi wanakaa, wananchi wanakaa na utumiaji wewe Mahakama yako itakapokuja pale mazingira yake yasije yakafanana kama niliyokuwa nayo sasa hivi. Tope tupu kwa upande ukipita huku mbele unaona jengo zuri lakini ukiangalia nyuma maji hakuna, tope nyingi huelewi wapi tunapokwenda, na mitaa pia ianze kutambulikana kabisa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri utaona kama nakugusa pale pasipo lakini najenga hoja ya msingi juu ya ujenzi wa Tunguu Mji Mpya.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie katika…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohammed Said naomba umalizie una dakika tatu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ukienda kwenye programu kuu ya PG0107 juu ya uimarishaji wa mawasiliano, nimeigusia juu juu nitapenda hii kidogo igusie. Nyengine ni programu kuu ya 0104 juu ya usimamizi wa masuala ya dini. Mhe. Mwenyekiti, nitaomba sana hapa nifahamike.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar sio nchi ya Kiislamu lakini Zanzibar ni nchi ambayo watu wake ni Waislamu tena wanaipenda dini yao na wamepitia pia katika malezi ya dini ya Kiislamu. Lakini ukiangalia katika PG0104 unazungumzia katika suala ya dini moja, ukienda katika historia yetu Zanzibar pale Mkunazini pana Kanisa sasa hivi pale *Anglican Church*, pale ukienda katika historia miaka 300 nyuma pamejengwa lile kanisa kwa sababu watumwa ndio walikuwa wanacharazwa pale halafu wanakuja kuuzwa ndio lilikuwa soko pale, unauzwa katika lile soko unapigwa halafu unapandishwa kwenye jahazi unapelekwa maeneo mengine. Hiyo ni historia yetu, lakini leo hao waliopita huko ambao wakoloni waliamua kuutokomeza ukoloni na wakapajenga sehemu ya nyumba katika dini ambayo tunaijua ni ya Wakristo. Kwa hiyo, *minority* au wachache Zanzibar wanastahiki kuwa na heshima yao, kutambuliwa kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sio nchi ya Kiislamu, zipo nchi ndani ya Bara la Afrika wanatumia *monarchy* ambao ni Swaziland, Lesotho pamoja na Morocco ni falme hizo, lakini sisi ni *United Republic of Tanzania*. Kwa hivyo, niseme kwamba hili tuliangalie sana na tuwe nalo vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie la mwisho naomba sana Mhe. Waziri suala la Utumishi wa Umma ndani ya serikali kwa wananchi ambao hasa ni wenye hali duni wanapokwenda katika mawizara husika wanashindwa kuwatambua nani ni

mtumishi wa umma na nani pale amekuja kufuata huduma ndani ya serikali. Naanza na wizara yako ambayo iko hapo Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, ukiingia ndani huwezi kutofautisha katika watu panapokuwa na msongamano baina ya mtumishi na nani pale amefuata huduma, ni vizuri watendaji wa serikali wakawa na *uniform* au kama itawezekana wawe wanavaa na *badge* kama Ikulu. Leo ukienda Ikulu Ofisi ya Rais unamuona kabisa mtu amevaa *badge* yake na jina lake, *badge* zipo za bei nafuu unapoingia katika hizi wizara ambapo wananchi wengi hasa masikini wanapokuja wenye hali duni, walemavu, watu wanahitaji msaada ili kupata taarifa basi ni vizuri anapomuona mtumishi wa umma aweze kutambulika, haiwezekani wanaingia pale wanapata tabu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa mawazo yangu kwa niaba ya wananchi wangu najishukuru sana mimi mwenyewe lakini pia nikushukuru wewe, nashukuru Baraza lako naunga mkono hoja asilimia 90 nitahitaji taarifa kumi. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed sasa namuomba Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Ali Suleiman Shihata, Mhe. Ali Khamis Bakari Doholo ajitayarishe.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie japo kidogo katika hotuba ya wizara hii. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kunirudishia pumzi bila ya malipo na mimi nikawa niko hai, lakini kunipa afya njema nikaweza kuhutubia katika Baraza lako hili.

Mhe. Mwenyekiti, natanguliza shukurani pia kwa kiongozi wetu wa wizara hii ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa hotuba yake hii iliyojaa mambo mengi mazuri, lakini miongoni mwake yanahitaji ufafanuzi ikiwa ni jambo la kawaida. Lakini pia nitoe pole kwa wananchi wote wa Zanzibar waliofikwa na majanga haya yaliyotokana na mvua kali zilizotufikia nchini, lakini hasa nisiwasahau wananchi wa Jimbo langu la Mgogoni ambao wameathirika na mvua hizi. Tusichukie hii ni kudura ya Mwenyezi Mungu na tuipokee kama alivyoileta na yeye Mwenyezi Mungu atatuletea wepesi kama alivyopanga mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki mimi naomba nichangie katika ukurasa wa 22 wa hotuba hii yanapozungumzwa masuala ya dini, usimamizi wa masuala ya dini. Hiki ni chombo muhimu sana katika nchi yetu ya Zanzibar

hasa kwa vile tunasema kwamba asilimia 99 ni Waisilamu. Kwa hivyo, wananchi wa Zanzibar walio mbali mbali katika nchi hii wamo ambao wana uwezo wa masuala mazima ya zakka. Nchi yetu katika hali tuliyonayo hivi sasa kwa kweli lazima tumshukuru Mwenyezi Mungu watu wengi wamejaaliwa na kipato cha juu sana, lakini tunashindwa kuitumia fursa ambayo Mwenyezi Mungu ametuwekea kutoa zakka ambayo itaweza kuhalalisha ile mali yetu ambayo tunayo na kuwasaidia wale wanyonge ambao wanastahiki kupewa zakka ile. Kwa hivyo, naishauri sana wizara hii ichukue juhudi za makusudi kwa sababu fedha ina uzito wake kuitoa lakini waratibu mambo ambayo kuwa yataweza kuwafika watu wenye uwezo kuwashajihisha waweze kutoa zakka na zakka ile ihifadhiwe vizuri na kupewa wale ambao wanastahiki, itasaidia sana ile omba omba ya nchi yetu ambayo imejitokeza.

Vile vile kwa sababu ni chombo cha dini nawashauri sana wizara hii katika masuala mazima ya mirathi. Hapa penye mirathi pana mtihani mwengine kwa sababu imeonekana kwamba kuna taratibu ambazo hazifuati sheria kutokana na kwamba mirathi inacheleweshwa, lakini pia wanaostahiki haki zao hawapewi wanapewa wengine kwa utashi wao. Chombo hiki jamani naomba sana kijitahidi, masuala ya mirathi yametajwa hata athari yake katika Qur-ani kula mali ya mayatima, mayatima ambao kuwa hawajui haki yao wewe ndiye unayestahiki kuichunga haki yao na kumpatia kila anayestahiki. Kwa hivyo, tuwe makini katika suala zima la mirathi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 37 unaozungumzia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika bajeti iliyopita niliwahi kusimama katika suala zima la kuwaombea idara hii suala zima la ajira, bado ina malalamiko ya ajira kwa watumishi na hiki ni chombo muhimu sana kwa nchi yetu, tunakitegemea kwa kuchunguza na kudhibiti hesabu za serikali. Pia na kutathmini thamani ya fedha katika matumizi ya serikali. Kwa hivyo, hapa kama tutakuwa hatukipi haki ya kuweza kupata ajira namna hiyo ambayo kuwa wanahitaji itakuwa yale malengo yetu hayafikii.

Kwa mfano, leo wananchi wanastaafu kazi mwananchi hawezi kupata haki yake ya kustaafu kama hesabu hajafanywa ipasavyo. Kama watumishi ni kidogo utakuta kuna mlundikano wa mafaili utaambiwa hayajafanyiwa mahesabu, mtu anaweza akakaa mwaka mzima lakini kama ajira hii itakuwa ipo na watu hawa wanapewa elimu kama hapa niliona elimu mbali mbali inatolewa lakini watu wenyewe ni kidogo, kama itakuwa idara hii inapewa kama inavyostahiki pamoja na uchache wetu wa fedha katika serikali, lakini suala hili la kupewa kipaumbele katika idara hii nayo ina nafasi yake, waweze kupewa nafasi ili waajiri watu waweze kutekeleza haya majukumu ambayo

yako mbele yao. Suala zima la kutengeneza viinua mgongo, kwa sababu kama hivi sasa watu 547 wameoneshwa, idadi ya watu ambao wameoneshwa hapa tayari wameshastaafishwa kazi, hawa kama idara hii haina watu wa kufanya kazi wa kutosha matokeo yake wataweza kuchelewa kupata haki zao za kiinua mgongo. Kwa hivyo, ni vyema na naomba sana katika kupanga bajeti yao nao wapewe kipaumbele ili waweze kuajiri watu wa namna hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 42 kunazungumza suala la utumishi serikalini. Ni vyema katika mpango wake aliyojiwekea huu wa kipaumbele 2017/2018, wamesema watasimamia usimamizi wa ajira, haki na nidhamu kwa watumishi serikalini. Hapa naomba nizungumzie suala zima la uajibikaji. Nimshukuru sana Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutekeleza ahadi yake na ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama alivyopanga. Kwa kweli ni muungwana na amefanya kama inavyostahiki.

Sasa na sisi tuoneshe kwamba tunajali kile ambacho tumefanyiwa, kwa sababu haki na wajibu ni watoto pacha hawa, leo wajibu tumeshapewa bado haki na sisi tuifanyie serikali. Kwa hivyo, watumishi katika taasisi mbali mbali nchini na wao wasimamie uwajibikaji, haingekuwa vyema kwamba tunadai maslahi, maslahi tumepewa lakini tukiangalia utendaji wa kazi bado upo pale pale. Ni imani yangu kwamba utendaji wa kazi nao ubadilike wasimamizi wasimamie kila mmoja nafasi yake tusifanye kazi kwa mazowea kama ilivyokuwa na Rais wetu amepiga kelele suala zima tuendelee kufanya kazi kitaalamu lakini pia kwa kuwajibika.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili wananchi wanastahiki na wao kuonesha kwamba wanajali hiki kilichopelekwa katika kurekebishiwa maslahi yao. Kwa hivyo, ni vyema tukarudisha shukurani hizi.

Sasa niende kwenye suala zima la uajiri. Pamoja na ajira zote ambazo zimepangwa katika mwaka 2017/2018 na kwa kuwa kama tuna nia nzima ya kutaka kunyanyua kiwango cha elimu nchini mwetu, basi Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri katika ajira yake aangalie katika sekta ya elimu kuwaajiri walimu wastaafu. Walimu wastaafu miongoni mwao tunaweza tukachukua mule tukawarudisha katika ajira ya muda. Mimi nina imani kubwa sana na walimu wa zamani wale wakirudi skuli ndio watasaidia kunyanyua elimu, bado nawaamini pamoja na kwamba wao hawakufikia *master* wala *degree* lakini elimu zao bado ni nzuri, hekima ya ufundishaji ni nzuri, mbinu ambazo wanazitumia za ufundishaji ni nzuri. Hivi sasa mbinu za ufundishaji zimepotea anakuja mwalimu darasani ana *master* lakini kwa kweli namna anavyowachukua wanafunzi na kuwafundisha utakuta hakuna matokeo mazuri.

Lakini walimu wetu hawa wastaafu kama tutawarudisha baadhi yao tukiwaona ambao wana sifa nzuri nashauri sana tuwarudishe walimu hawa jap kwa ajira ya muda.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee katika ukurasa huu wa 42 kifungu 141 panapozungumza masuala ya ajira. Wanasema hadi Machi, 2017 ajira 348 zimetangazwa kutolewa kibali cha ajira, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie ni ajira ngapi mpaka sasa zimesimamishwa katika hizo 348 Unguja na Pemba. Haya malalamiko aliyosema malalamiko mawili yalitatuliwa yalikuwa ya aina gani, ya kitu gani, atuwekee wazi hapo. Lakini atumishi 15 wameongezwa muda wa utumishi. Mimi hapa nataka nipate maelekezo na maelezo zaidi wameongezwa muda hawa wana umuhimu gani hata wakaongezwa. Kwa sababu nimeona baadhi yao kwa sababu na mimi natokea katika ajira hizo hizo, mtu anaomba aongezwe muda lakini ukimuona katika ile taasisi hakuna anachozalisha, kama ni mwalimu *okay* nakubaliana naye au ni daktari au sekta nyengine muhimu ziko, lakini kuna watu hapa watu wanatumia mbinu ya kuusogeza muda wa maisha kwa hivyo hii nafasi isitumike vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri na atakapokuja anieleze hawa watumishi 577 ambao wameshastaafishwa kazi je, mafao yao yana mwelekeo gani katika kuyapata kwa haraka. Kwa sababu miongoni mwao humu mtu akistaafu anajipangia mimi Mwenyezi Mungu akinijaalia nikiaafu nataka niende Makka na humu nina hakika wamo ambao wameshajipangia. Kwa hivyo, kama hawajapata haki zao hawa watu nawaombea sana wapewe kipaumbele, watu ambao wamestaafu na wamejipangia mwaka huu kwamba nao waende wakatekeleze nguzo hii ya tano ya Kiislamu kwenda kuhiji. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana waziri alichukue hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile bado napingana na mimi katika takwimu hii ya watu wanne kwamba ndio likizo bila ya malipo, au atueleze hii watu wanne walioelezwa humu katika hotuba yake ni aliomo ndani ya ofisi yake au ndio nchi nzima? Kwa sababu mimi mwenyewe niko likizo bila ya malipo, kama alivyosema Mjumbe mwenzangu humu 12 au 20 unaweza ukawakuta humu, leo anatupa takwimu ya watu wanne kwamba ndio wako likizo bila ya malipo. Hapa panaweza pakachezwa mchezo mchafu.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunatokea katika taasisi mbali mbali huku, hapa utasikia mtu yuko likizo bila ya malipo lakini anazunguka anatiliwa fedha katika *account* yake. Haya yanatokea fedha za serikali zinapotea, tunasema matumizi makubwa kumbe ni matumizi hewa, tuisaidie serikali katika hilo. Kama tutafanya hivyo tutakuwa tunaisaidia sana serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sitaki nichangie mengi hayo yanatosha, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja lakini atakapokuja anieleze katika masuala ambayo nimetaka ufafanuzi. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako, sasa namuomba Mhe. Ali Suleiman Shihata na Mhe. Ali Khamis Bakari na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote nichukue fursa hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora; kila kitu kimeungana humu.

Pili, nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea nazo katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma za jamii hasa zaidi kwenye sheria na mambo ya dini, ili waishi vizuri katika mwelekeo wetu ambao unatufaa.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein hasa nikizingatia kwamba Mhe. Rais aliwahi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria katika mwaka 2000 hadi kifo cha Marehemu Dkt. Omar Ali Juma alipoteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, wizara hii naamini ni wizara nzito na inatakiwa busara na hekima ili kuendeleza yale mema yote yanayotakiwa kwa maslahi ya wananchi wetu.

Aidha, niseme tu kwamba hivi sasa tuna mambo mengi ya maendeleo katika nchi yetu kutokana na mikakati mbali mbali inayopangwa ya kisheria na mambo mengineyo, lolote la kisheria litakusaidia na ukilidharau litakupoteza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa mchangiaji wa muda mfupi sana kutokana na mazingira ambayo ninayo leo, nimeomba ruhusa hii kidogo halafu niondoke. Kwanza kabisa ukurasa wa 30 Mahkama Kuu. Niishukuru serikali kwa kuendeleza mahkama zetu juu ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wenye matatizo mbali mbali wanapata fursa ya kupata uamuzi wa kimahkama juu ya kesi zao mbali mbali. Lakini naishukuru serikali kwa kuandaa au kuweka Mahkama ya watoto Mahonda. Hili nimelifurahia sana, nasema tu kwamba serikali imezingatia jambo kubwa sana hasa tukizingatia udhalilishaji wa watoto wetu na kinamama unaendelea siku hadi siku. Naipongeza kwa dhati serikali kwa kuliona hili lina umuhimu wake, lakini nigeomba zaidi vyombo

vya sheria viwasaidie watoto hawa kupata haki zao pale wanapopatwa na kadhia hii.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara umefika wakati sasa hivi kupitia vyombo vyetu vya sheria, sheria ya udhalilishaji wa watoto ibadilishwe au irekebishwe. Kwa sababu sheria hii ni ya muda mrefu na matokeo yanazidi siku hadi siku. Leo tumesimama hapa tumesikia kuna mtoto mmoja kabakwa, yaani siku hadi siku, kukipita siku mbili majaaliwa lakini hali hii inatisha katika nchi yetu na ni jambo la aibu sana katika mazingira yetu tuliyokuwanayo Wazanzibari. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri mahkama hii ya sheria za watoto ambapo Mahkama ya Mkoa imepewa uwezo wa kumhukumu muhalifu miaka saba ifutwe, yaani irekebishwe.

Mhe. Mwenyekiti, si vibaya anayefanya kosa la kumuharibu mtoto yoyote yule kifungo cha maisha kinafaa kuliko vyenginevyo, kwa kuwa Zanzibar hatuna utaratibu wa adhabu ya kifo kwa sababu yeye pale anakwenda kama kumuuwa yule mtoto wa watu, basi na mimi napendekeza kwamba sheria hii iletwe na nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii nitalisimamia kwa uwezo wangu wote kuishauri serikali kuhakikiasha kwamba wakati umefika kuliondoa janga hili katika mikono yetu na kuliwekea sheria ili watoto wetu wasitirike na wapate usalama wao wanapotembea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya unapojenga leo hufikirii kesho baadhi natoa mfano ulipojenga barabara ya kutoka Kinazini - Bububu wakati ule tulikuwa na gari kama kumi au ishirini hatukifikiria kumbe wakati unabadiliko na tulipopitisha sheria hii na mimi nilikuwemo kati ya miaka 2000 huko tulisema miaka 7 inatosha kumbe ilikuwa kama tunampa mtu fursa ya kufanya lile tendo arudie tena baada ya kutoka jela.

Mimi ombi langu Mheshimiwa naiomba serikali kwa dhati kabisa sheria ya mtoto ya udhalilishaji irekebishwe na ianzie kifungo cha maisha kinatosha kuliko jengine lolote itakuwa mtu unampa nguvu ya kufanya jengine na wengine kurudia mambo kama hayo. Naishauri serikali sana tusiwe n huruma kwa hili huyu ni sawa sawa na muhujumu uchumi wa nchi au huyu ni fisadi wa mwisho katika nchi yetu au ni jambazi wa mwisho katika nchi yetu. Mheshimiwa naliomba sana hilo linagaliwe.

Lakini pia nishukuru tu kwamba Mahamaka hii ya watoto inaendelea na kesi zake vizuri na ndugu yetu dada yetu aliewekwa pale kidogo anakwenda vizuri. Naomba tu bado wapate ushauri wa wasaidizi kwa sababu watoto ni watoto wakati mwengine wanababaika. Lakini kwa kuwa tulipitisha azimo hapa

nafikiri linasaidia kwa sasa hivi. Muhalifu yoyote asipewe ruhusa ya kupata dhamana. Hili Mhe. Mwenyekiti, nafikiri halina mjadala tulipitisha tulitoa azimio hapa hili liendelee na lisaidie, lakini turudie haraka miaka 7 ni kidogo kifungo cha mwanzo kianzie miaka 50 mpaka miaka 100 au maisha yake alale jela.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nitazungumza kwa ufupi Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni chombo ambacho tunakitegemea haya tunayopiga kelele hapa ndio anaebeba sasa. Namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu tunayoyaleta hapa tuyaangalie kwa usalama wa wananchi wetu na nchi yetu kwa jumla. Zanzibar ya leo ina historia mbaya kuliko miaka mia mbili iliyopita huko nyuma. Zamani mwanamke au mtoto anatembea hata saa sita za usiku hana wasi wasi, leo ikifika saa moja na nusu mwanao hajarudi unatetemeka akili yako inasema sijui kuna nini limemtokea Mwenyezi Mungu amnusuru au awanusuru watoto wetu. Kwa hivyo, niombe sana Mhe. Mwenyekiti, kupitia wizara na Afisi ya Mwanasheria haya tunayoyaleta yatizamwe haraka ili yalete manufaa kwa wananchi wetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka mimi nimpongeze Mkurugenzi wetu huyu kwa kazi zake njema anazozifanya lakini pia ningeomba serikali kupitia afisi hii Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka anafanyakazi vyema, tatizo linakuja kwa yale yale tunayoyapigia kelele kila siku wananchi wetu bado waongezewe taalamu ya kuhakikisha kwamba wanakubali kutoa ushahidi pindi linapotokea tatizo kwa kesi yoyote na anapata shida na masikitiko kwa sababu yeye katika kazi zake hana msaada unaopatikana kwa sababu kesi anazo njoo utoe ushahidi hana, watu hawaendi.

Lakini kuna jengine lilosababisha vile vile naiomba sana serikali iangalie mtu anapoacha yake kwenda kutoa ushahidi alipwe maposho yake ya nauli nyengine stahiki zake na hilo watu wengi wanapiga kelele kwamba hawalipati. Mimi naomba hili liangaliwe kwa nanufaa ya nchi na taratibu zetu wa kisheria zinavyokwenda katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nitalolizungmza jengine katika suala zima la kitabu hichi ni Afisi ya Mufti. Mimi nampongeza Mufti wetu, nawapongeza viongozi wote wa ofisi hii kwa kazi njema wanazozifanya na hasa tukizingatia kwamba wanakwenda katika maamuzi mengi ambayo ya maslahi ya nchi yetu na watu wetu.

Nawaomba waongezee bidii na wawe wastahamilivu kwa mengine yanayotokea lakini kwa ile mizozo ambayo iko karibu wa kiiondoa wao basi ni

vyema wafatilie waiondowe, kuna Wajumbe walizungumzia masuala ya misikiti mbali mbali, kuna matatizo mengi yanajitokeza. Lakini matokezeo yale sijui kama watu wanataka uluwa wa uongozi tu au wanataka mambo mengine hatuyajua. Kwa hivyo, wenzetu hawa wasichoke kufatilia ili kuweka kwamba vyombo vya ibada ni vyombo vya kuendeleza dini ni waumini wake kwa salama na amani katika nchi yetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, Wakfu na Maliamana nawapongeza kwa kazi yao nzuri wanayoendelea nayo kila siku. Lakini ningeomba tu sana Wakfu na Maliamana wanafanya kazi nzito lakini malalamiko baadhi ya watu wanasema tu kwamba wanapofika katika Wakfu na Maliamana kwenye kutoa mirathi inakuwa watu wanawakata pesa nyingi kiasi kwamba wanchanganyikiwa. Baba kaacha mali au mama kaacha mali, lakini katika urithi wakati mwengine inakuwa riba kubwa wanavyosema mimi sie riba inakuwa kubwa. Kwa hivyo, kama lipo hili ningetoa nasaha tu kwa sababu hili ni jambo la kisheria la kidini waliangalie na hekma iwepo ili mtu aondoke pale alichopata apate kwa matumizi yao ya maisha yao yanavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa niseme tu kwamba mimi naishukuru wizara hii na tunaitegemea kwa mengi. Lakini kubwa ninalolisema hapa kwamba Mhe. Mwanasheria wananchi waelimishwe kwa mambo mbali mbali tunayokwenda nayo katika nchi yetu na kuna sheria nyingi wanaingia watu makosani kwa kutokuzijua. Mimi hutoa busara kusema kwamba "Elimu kwanza mengine baadae". Kwa hivyo, wananchi wetu wapewe taaluma mbali mbali za kisheria hili linafaa hili halifai ili wasiingie katika mambo ambayo yatakuja kuwakwamisha huko mbele wakapata shida wao na familia zao.

Baada ya hayo machache kabisa Mheshimiwa nazipongeza taasisi zote za wizara hii na sina matatizo nazo, nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wote wa wizara kwa jumla na sina pingamizi naipongeza kwa asilimia mia moja wizara hii na naiunga mkono. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kinipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika bajeti hii ya 2017/18.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kuipongeza wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kuanzia Waziri wake, Naibu Waziri, Wakurugenzi na watendaji wote kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nianze kwa Ofisi ya Wakfu na Maliamana ambayo inakusanya au inafanyakazi kwa mujibu wa sheria ya masuala ya zakka, sadaka pamoja na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa mchango wangu nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri kwa nini hii wizara inakaa kama vile mnara wa *Zantel* kwamba anaetaka ku-*chart* lazima atoke yeye afuate kile kifushi ndio aanze kupata mawasiliano. Kwa nini haibadiliki, Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoona siku zote katika jambo la kheri mwanaadamu anakuwa mgumu wa kulichangia. Kwa nini haiandai matangazo maalum kama vile tunavyoona sehemu za Ijitimai inapotokezea redio zinapiga kelele wanasema kwamba kuna mchango wa Ijitimai aliekuwa na upawa, alie na mwiko, alie na jembe, lakini wao wanakaa kwa nini hawawaelishi hawa watu ambao wanahitaji kutoa zakka au wamefikia kutoa zakka wakaelimisha wakawaambia bwana mali zinahitaji kutolewa zakka na sadaka ili wapate muamko na kuwaelekeza katika mambo mema.

Mimi nilikuwa nasema Mhe. Mwenyekiti, kwamba hii Kamisheni ibadilike sasa na iandae matangazo maalum ili kuwafanya hawa watu ambao wanatakikana watoe sadaka na zakka ili wapate ule ujumbe uwafikie kwa sababu tunaambiwa kwamba tukumbushane kwa hivyo mimi nataka wakumbushwe kila baada ya muda ili kile kinachotakikana kitolewe tusingoje mpaka Mwenyezi Mungu akachukuwa kwa mkone wake, ukasikia aaah! fulani kapoteza kiasi fulani walitakikana hawa wakamatwe na mapema kuwe na sheria maalum au utaratibu maalum wa kupangiwa au wa kuelekezwa kwamba jamani imefikia hatua sasa watu wabadilike na wafanye hivi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka niseme hivyo.

Lakini vile vile hapa hapa nikiendelea sijui niiulize kwamba kuna utaratibu gani wa ugawanyaji wa hizi sadaka na zakka wakati zinapotolewa kwa sababu hapa katika ukurasa wa 23 kuna idadi ya pesa zilizokusanywa kwa idadi ya masuala ya zakka ukurasa wa 23 wasema milioni Tzs. 270,603,955.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nauliza kuna utaratibu gani wa ugawanyaji wa hizi zakka na sadaka kwa sababu sis sote ndani ya majimbo tuanona tunao masikini wetu na masuala mengine. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi naona kwamba hili suala liangaliwe vya kutosha, leo utakuta sadaka zimekuja lakini zinaishia kwa imamu au msoma adhana au mkubwa fulani, kuna misaada inakuja misaada hii utaambiwa kwamba bwana Kondoo mzima kamchukuwa imamu.

Lakini wale watu wanaostahiki ambao wapewe zile sadaka haziwafikii Mhe. Mwenyekiti, tunaangalia kwamba uwezo wa watu wengine unakuwa mkubwa

lakini wale wa kipato cha chini watu wa huko wanaotoa sadaka zao wanatoa kwa mujibu wa kwamba ziwafikie wale wanaokusidiwa. Sasa haziwafikii wengine wananza kugaiana huku juu kule chini masikini ya Mungu pengine Kondoo yule hajawahi kumla anamsikia tu lile jina Kondoo, au kuna vitu vinatolewa kwa mfano kama michele na mambo mengine mtu anasikia tu kuletwa tende misikitini lakini kaenda kusali pengine hata ile kokwa haioni.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana hii misaada inapoletwa katika hii Kamisheni igawanywe inavyotakikana hawa watu waelimishwe waache yale masuala yao waliokuwa nayo kwamba bwana labda wagaiane wale wakubwa tu lakini wale wadogo ikawa haiwafikii. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri yupo anasikia na watendaji wapo wasimame ziadi hili suala la zakka na sadaka. Mimi najua waenda nalo lakini huko chini kuna ukiritimba zile zinapozitoa kuzifikisha Mawilayani au Mikoani kwa ajili ya kupewa watu wetu haziwafikii. Kwa hivyo, hili naliomba sana waliangalie kwa macho mawili.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye suala la Chuo cha Ualimu *IPA* kwanza niwapongeze kwa kazi zao ambazo wanazifanya na juhudi kubwa ambazo wanaendelea nazo na vile vile kutoa elimu juu ya wanafunzi pamoja na walimua ambao wanataka kujiendeleza. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nichangie kidogo Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei) kanifilisi lakini na mimi pia nitakazia kuhusiana na Chuo cha Utumishi kilichopo kule Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mazingira yake ambayo kiko mimi sina mjadala nayo yako mazuri kwa sababu mwanafunzi anapotaka kusoma lazima apate pahali pazuri pa kukaa na utulivu ili kuweze kuya-*cover* yale masomo yake.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, bado suala hili la walimu wanaotokana na sekta hii ya hichi chuo ni kidogo kule Pemba na kwenye Kamati hili tulilizungumza. Mhe. Waziri hii ni mara ya pili au tatu hili suala tunalisema, hebu tuone kwamba bajeti hii inayoelekea kule wanafunzi wameshajitokeza wengi na wanatakikana wapate hii elimu. Kwa hivyo, tusimbebeshe mwalimu mmoja mzigo kila walimu wakiwa wengi ndio ufanisi wa kile chuo unaendela. Lakini Mhe. Hamad Abdalla Rashid hapa alizungumza kuhusiana na kile chuo kwa habari ya barabara. Mimi barabara sitoigusia lakini Mhe. Mwenyekiti, tunapofanya jambo tusijaribu kwa sababu dini yetu inatuelekeza mtu akisema jambo asiseme kama anajaribu, tumeomba Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu kajuaalia tumefungua chuo tukajitangaza wanafunzi wamekuja mbali mbali wakiwemo walimu kwa ajili ya kujipatie elimu kujiendeleza.

Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, tuangalieni na yale mazingira Pemba kuna Mikoa miwili Kusini na Kaskazini kuna watu au wanafunzi ambao wanatoka maeneo ya Konde na kuna wengine wanatokea maeneo ya Mkoani barabara ile wanafikia pale Macho manne wanateremka gari wanataka wende kwenye Chuo lakini inakuwa tabu kufika kwa sababu barabara inayoelekea upande wa Wawi inaendazake Vitongoji Jeshini hailekei maeneo yalioko chuo.

Kwa hiyo, ina maana pale wanafunzi wanaotoka pale kwenda kule inakuwa shida kufika katika Chuo na kuweza kupata yale masomo yao. Sasa inakuwa shida kwa nini Mhe. Waziri hii serikali na wizara yako ni kubwa kwa nini haiandai basi la *staff* ambalo maalum kwa ajili ya ile skuli ili likatoa huduma hata kama wanafunzi wanaweza wakachangia pesa, lakini ikawa ipo hii pesa wanachangia lakini na wao wanaambiwa ikifika saa saba ama saa nane mwanafunzi yoyote awe keshafika Machomane inakuja gari inawachukuwa wanajisikia vizuri na wao.

Kama tunavyoona suala la elimu katika kulitafuta linakuwa gumu hasa kipindi hichi cha mvua inakuwa shida kwa wanafunzi, wengine mwezi mtukufu wa Ramadhani uankuja huo mtu anaondoka pale ikifika saa saba anakimbilia, akitoka pengine magharibi masikini ya Mungu anakimbilia akampikie mumewe uji, lakini hajui atafika vipi barabarani na gari za kwetu Pemba mwisho saa kumi katika mwezi mtukufu wa ramadhani kama mwengine inafika saa kumi na mbili, lakini kuna wengine gari ikifika saa kumi na moja tu hakuna tena kama maeneo ya Kaskazini Pemba.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika bajeti hii kile chuo tumekianzisha kwa nia njema safi ya kusaidia wanafunzi kuweza kupata elimu. Lakini tuwaboresheeni kile chuo ili mradi yale wanayokudia yaweze kupatikana hususan suala hili la usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo mimi nije kwenye masuala ya mishahara. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuitimiza ahadi yake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nataka nizungumze kidogo kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi mpaka leo hususan kwa upande wa Wizara ya Afya huko ndiko kuna uoza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri hii ahadi ni ya muda mrefu mpaka kufikia watu wamefika wakasema aah! jamani huu ni mwezi wa ngapi tuliahidia kuongezwa mishahara lakini hali imekuwa hivi. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo limekaa muda mrefu ni imani yangu kwamba hawa mawaziri na sekta iliyokusudiwa ni kwamba walikwisha kujipanga ili

kuweza kuwatilia mishahara wafanyakazi waliokusudiwa. Lakini mpaka inafika leo ukienda kwenye Wizara ya Elimu na baadhi ya sehemu nyengine wafanyakazi wanalalamika, kuna wengine mishahara yao imenona kuna wengine mishahara yao imenona kuna wengine *account* zao hazina kitu.

Sasa naomba sana najua hapa sijui kama ni Utumishi ya Umma ambao wamelihusu hili suala. Mhe. Mwenyekiti, mimi najua kwamba hizi wizara ni kubwa ni imani yangu kwamba kila wizara ilipewa hili jukumu lake kusimamia watu wake, lakini bado kuna mapungufu ambayo hajakaa sawa wafanyakazi wanalalamika mtu anaambiwa Jumatano njoo tuje kukurekebishia mshahara wake akirudi anaambiwa nenda tena Alhamis njoo tuje tukurekebishie, Ijumaa njoo. Inabidi kile kipesa alichokipata anaanza kukipandia gari njoo, kesho, njoo kesho mpaka kinafika pahala kinamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba sana waliangalie kwa sababu mtu anapoandika jina anaandika Ali Khamis Bakar natoka wapi Skuli ya Tumbe Sekondari. Namba ya simu na saini inakuwepo kwa nini hapigiwi simu tu akajulikana huyu kiwango chake kilichotakikana ni hichi lakini kwa kweli marekebisho yake hajafanyiwa, akarekebishiwa baadae akapigiwa simu akaambiwa tayari. Kwa nini leo anaambiwa njoo na vyeti kesho arudi na hichi ni kipindi cha mvua gari zenyewe kama tunavyoona mtu mara vyeti anavirowesha kesho vinapotea ili mradi mtihani. Kwa hivyo, naomba sana hii wizara inayohusika na masuala haya isimamie hili jukumu kuona kwamba na wao wafanyakazi hawa wanajisikitia *comfortable* katika ile mishahara ambayo imeongezwa isiwe leo kesho anakwenda hapa au hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye masuala ya wastaafu. Mhe. Mwenyekiti, kwenye masuala ya wastaafu najua hii wizara inasimamia na nashukuru sana kwamba wanapata pencheni zao kwa wakati, lakini bado inakuwa kuna malalamiko. Mhe. Mwenyekiti, malalamiko ya kwanza ni kwamba namuomba sana Mhe. Waziri hawa wastaafu ni watu ambao kwa kweli wanaisaidia serikali, kwanza wana uzoefu wa hali ya juu katika zile idara ama sehemu husika walizotoka wameshafanyakazi kwa muda mrefu ndio wakafikia pahali wakastaafu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba Mhe. Waziri na watu hawa na wao tuwe nao karibu ili kuweza kuchota yale mazuri ambayo wamekuwa nayo kwa muda mrefu kupata uzoefu kuelekezana kwa jinsi ya mambo ambayo walikuwa nayo. Lakini tukiwadharau watu hawa ndio pale inakutia unashangaa mtu huyu tulikuwa nae muda mfupi ndio kawa hivi kaingia kwa sehemu nyengine kumbe tuliwadharau. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana

Mhe. Waziri nadhani keshanifahamu kwamba kuhusiana na habari hii hawa wastaafu kwamba tuwe karibu ili nao wao wajisikie na kwamba bado katika serikali wanathaminiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye masuala ya watu hawa wa haki miliki. Katika ziara yetu tuliokwenda ni malalamiko makubwa juu ya watendaji wetu tulioyapata kuhusiana na habari ya majengo yao na bajeti zao.

Mhe. Mwenyekiti, haya mambo ni mazito na wafanyakazi wetu katika maidara yetu tuliyonayo tunaona jinsi ambavyo wanajitolea na kuwasaidia watu wa chini kuweza kuwatatulia matatizo yao. Lakini Mhe. Mwenyekiti, bado kuna malalamiko ya kwamba kuna baadhi ya vitendea kazi katika maofisi yao vinakuwa kidogo. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri katika hizi taasisi zako ambazo zimekuzunguka katika wizara yako uziangalie kwa macho mawili ili yale mapungufu yalioko katika mawizara yaweze kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa kwa sababu mimi ni mwana kamati nilisema niyagusie haya kidogo ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu na yaweze kusikika. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nawashukuru sana watendaji, mawaziri na manaibu mawaziri na watendaji kwa jitihada kubwa waliyoionesha kwa upande wetu katika mzunguko wote wa ziara yetu ya kamati katika kipindi hiki cha bajeti.

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh, na akifuatiwa na Mhe. Zaina Abdalla Mussa. Kabla ya Mhe. Hassan Khamis, Waheshimiwa Wajumbe naomba niwakumbushe leo michango yetu itafikia saa 6:00 kuna wachangiaji wengi waliobaki na wengine wameniomba niwape dakika tano tano. Kwa hivyo, wale ambao sikuwataja katika michango hii naomba wapeleke michango yao kwa maandishi. Ahsante Mhe. Mjumbe endelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika bajeti hii muhimu kwa maendeleo ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua kazi kubwa ya serikali ni kuwatumikia wananchi na kazi ya watunga sheria ni kuwahudumia wananchi. Mhe. Mwenyekiti, naanza kuchangia kwa upande wa mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tunazo mahakama zinafanyakazi nzuri sana, tunazipongeza sana kwa kazi nzuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wanalalamika sana kwamba mahakama makesi yamerundikana na kesi hizo zinakaa kwa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi na hatimaye makesi hayo hufutwa bila ya kupatikana ile haki inayokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande huu wa mahakama nina ombi kwa Mhe. Waziri kwamba atafute utaratibu unaofaa wa kuhakikisha makesi hayarundikani mahakamani na yanapatiwa ufumbuzi kwa haraka, kwa sababu yanapokaa mahakamani kwa muda mwingi yanakaribisha rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu wa pili kwa upande wa mahakama. Kwanza napenda kuwashukuru mahakama wamejenga jengo zuri sana kule Pemba wamelifanyia ukarabati. Lakini mimi nina wasiwasi tumepata simu nyingi, tumelitembelea kwa aina yetu lile jengo la mahakama kazi nzuri imefanyika. Lakini mimi nina wasiwasi baadhi ya Wazanzibari, wakwezi na wakulima wana wasiwasi kwa mujibu wa ukarabati wa lile jengo, aina ya ukarabati uliofanyika, pesa iliyotumika na hali ya jengo lilivyo sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, namtaka Mhe. Waziri aje kuniambia ni kampuni gani iliyofanya ukarabati wa lile jengo la mahakama Pemba na imetumia kiasi gani na wana *guarantee* ya muda gani. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wanalalamika wananchi wametupigia simu lile jengo limekarabatiwa juzi lakini tayari lote limeanza kubanduka, limekuwa bovu na halina viwango. Sasa nina wasiwasi na wenzangu wana Mapinduzi wana wasiwasi kwamba mkandarasi ametupiga changa la macho katika kukarabati jengo letu la mahakama jengo ambalo limetumia mafedha mengi ya wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja katika mchango wangu namba tatu katika Tume ya Kubadilisha sheria. Mhe. Mwenyekiti, tunayo tume ya kubadilsha sheria mwenyekiti wake kama sikosei ni Jaji Mshibe anafanyakazi nzuri, tunamsifu sote lakini kuna malalamiko mengi wanasema sheria nyingi nchi hii zimepitwa na wakati zinataka kubadilishwa, lakini zinakwama kwa Mwanasheria Mkuu ambaye pia ni Mjumbe wa Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, tulipochangia hoja binafsi ya Mhe. Asha Abdalla wa Kiwengwa ya udhalilishaji, Mhe. Waziri alituahidi kwamba ataleta marekebisho ya sheria namba 7, kipengele namba 150 sheria namba 7 ya mwaka 2014 kipengele 150 cha kwamba, mtu anayedhalilisha na yeye pia aingie katika sheria ya makosa isiyokuwa na dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii bado Mhe. Waziri hajaileta kuirekebisha na mpaka leo sheria hii watoto wetu wanaendelea kudhalilishwa na hakuna kinachoendelea. Pia namuomba Mhe. Waziri atuambie ni lini ataileta sheria hii ya udhalilishaji ya watoto iwe ni sheria moja wapo kati ya sheria zisizokuwa na dhamana. Kadhalika Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwa tukichangia tulisema sheria ya utumishi wa umma watu wengi kupewa ajira mkataba imepitwa na wakati. Mhe. Mwenyekiti, tunakubali kuna kada lazima mtu kama daktari na mambo mengine apewe mkataba.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kumuona mfagiaji, mhudumu na sekta nyengine anapewa mkataba wa nchi hii, wakati vijana wengi wapo mitaani hawana ajira. Mhe. Mwenyekiti, vijana ni wengi hawana ajira kwa mujibu wa takwimu za Zanzibar. Leo hii unampa mtu mkataba ambaye muda wake wa miaka 60 umeshafika na hana tena *rear professional* kada maalum, kwa kweli jambo hili mimi linaniudhi na lina nisikitisha kuwaacha vijana kutokuwa na ajira kumuongeza mtu mkataba ameshafanyakazi kwa muda wa miaka 50 eti ajipange, anajipanga nini tena huyu, mimi sioni cha kujipanga. Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri atujibu. Lini ataileta sheria ya utumishi wa umma kuja kubadilisha sheria ile ili ifunge watu kuongezewa mkataba nchi hii ili iweze kutoa fursa kwa vijana zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika Mahakimu wa Mkoa, tunao Mahakimu wa Mkoa ambao kwa mujibu wa sheria kama sikosei Hakimu wa Mkoa mwisho kufunga miaka 7. Mhe. Mwenyekiti, naomba tena naomba sheria namba 7 iliyokuwa *amended* mwaka 2014 kifungu namba 150 ambacho kinatoa fursa mambo mawili tu ndio mambo yasiyokuwa na dhamana, nalo ni *treason*, kwa Kiswahili sijui kitu gani. *What is treason....*

Waheshimiwa Wajumbe: Uhaini.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh : *Yes*. *Treason* ambayo ni uhaini na nyengine mada. Sasa nilikuwa naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu yupo hapa Mhe. Waziri iongezwe mambo mengine mawili, nayo ni udhalilishaji na mtu yeyote anayeshughulika na masuala ya madawa ya kulevya, anayeyaleta, anayeyasambaza pia sheria hii iwe haina dhamana. Baada ya mambo mawili baada ya *treason* na nyengine udhalilishaji iwemo na madawa ya kulevya haya mambo manne. Sasa namuambia Mhe. Waziri lini ataileta sheria hii kuja kuibadilisha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye Tume ya Kuzuia Rushwa. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza serikali kwa kuileta sheria hii ya kuwa

na Tume ya Kuzuia Rushwa, kwa sababu kwenye katiba yetu ya Chama cha Mapinduzi, katika ahadi za mwanachama wa Chama cha Mapinduzi zinasema, inamkataza kwamba rushwa ni adui wa haki sitapokea wala kutoa rushwa, inatukataza sisi wanachama wa Chama cha Mapinduzi ambao nchi hii ndio wengi, hatatoa wala kupokea rushwa. Serikali kwa kuliangalia hilo imeanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa, lakini kinachonisikitisha wala rushwa bado Zanzibar ni wengi, makesi tunaambiwa yako mengi lakini yapo kwa DPP hayafanyiwi kazi tunaambiwa watu wa rushwa wanalalamika, kesi kwa DPP haziendi mbele zimekaa.

Kwa hivyo, mimi naomba kusema hivi kama kweli Serikali ya Zanzibar tunataka kuwaondosha walarushwa basi ije sheria ya ku-*amend*, tutumie ile sheria ya *drug abuse* ya Marekani. Mla rushwa wa nchi hii tusimpeleke kwa *DPP*, tumpeleke moja kwa moja mahakamani, kama ilivyo *drug abuse* ya Marekani, mlarushwa tukishampata tusipite popote tumpeleke kwa *DPP* na hawa wote Mhe. Mwenyekiti, walarushwa, wadhalilishaji na wala unga tuwatie katika kipengele hicho moja kwa moja turuke nao mahakamani, kwa sababu tukiwapeleka kwa *DPP* tukiwapitisha huko inawezekana urasimu ukawa mwingi, ikiapita hiyo rushwa na yakawa mambo mengi tusipate *solution*.

Mhe. Mwenyekiti, njia pekee ya kukomesha vitendo viovu ni kutoa hukumu kali, nchi za wenzetu kama Marekani, Canada na Uingereza ita *file* aliyedhalilisha watoto akishafungwa anakuwa hana pakuka, kwa sababu kila mtu katika mtaa wake hamtaki anakuwa kama mtoto wa paka anakuwa yuko huku na huko.

Mhe. Mwenyekiti, kama kweli tumedhamiria kukomesha mambo haya, lazima watu hawa wawe hawana dhamana, tusiwapeleke kwa *DPP* kwa sababu kwa *DPP* inawezekana zikakaa ushahidi ukawa haujakamilika, ikawa hivi na ikawa hivi. Tuwapeleke moja kwa moja mahakamani tukawahukumu, na mambo haya yapo Marekeni yanatumika na nchi nyingi za duniani tunakokopia hizo sheria mambo haya yanafanyika. Mhe. Mwenyekiti, ukiitiza *drugs abuse* ya Marekeni moja kwa moja haipiti kwa *DPP* inakwenda mahakamani kama kweli tumedhamiria kukomesha rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna *DPP*, kuna Polisi na kuna mahakama. Nampongeza sana *DPP* anafanya kazi nzuri, nawapongeza polisi wanafanyakazi nzuri na nawapongeza mahakama wanafanyakazi nzuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika mahakama, *DPP* na Polisi ni watu wanaolumbana kila siku, kulumbana kwao na kugombana kwao, na kusemana kwao kunaondoa ufanisi katika hukumu za kesi. Naomba kuziomba taasisi hizi tatu za nchi hii

zishirikiane katika kufanyakazi, ili tuweze kukomesha makosa yanayofanyika nchi hii tuwe na nchi iliyokuwa salama na watu waishi salama. Mhe. Mwenyekiti, kama *DPP*, Polisi na mahakama wataendelea kulumbana hapa itashindwa kufanyakazi, nawaomba washirikiane.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar kama sikosei, ambayo ina majukumu mengi sana, lakini moja ni kushughulikia masuala mazima ya Hija. Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tuna mahujaji wengi Zanzibar kwa sababu nchi yetu asilimia 99.9 kwa mujibu wa Mhe. Nadir Abdul-latif ni Waislamu.

Mhe. Mwenyekiti, watu wengi tunakwenda Makka kuhiji, lakini tumekuwa tunapata matatizo kila siku, kwa sababu kwa mujibu wa sheria za Saud Arabia nchi yoyote inayotaka kuwapeleka watu wake kuhiji ni lazima iwe na kitu kinaitwa *beitha*, hiyo *beitha* inatolewa kwa nchi ambayo inafuata sheria za Kiislamu, baadhi yao sio zote, lakini sheria ya kwanza lazima iwe na taasisi inayotambulika kwa sheria ya nchi ile inayoshughulikia mambo ya Kiislamu. Kwa Zanzibar tunayo taasisi hiyo inayoongozwa kama sikosei ndio hii Wakfu na Mali ya Amana, ambayo inaendeshwa na Katibu Mtendaji kama sikosei. Lakini kwa Tanzania hatuna taasisi hii. Lakini huko nje tunajulikana kama Tanzania. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa kuna mgogoro hali ambayo mpaka Makamu wa Pili anaingia, kwamba kumejitokeza mambo mengi kitu ambacho wamewahi kufikia wasiende kuhiji, kwa sababu ya mgogoro baina ya Zanzibar na Tanzania Bara dhidi ya hiki kitu ambacho kinaitwa *beitha.*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri uwezekano upo kwa Zanzibar sasa kuwa na beitha yetu tusitegemee beitha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Najua kesi hii anaijua, lakini nimepata taarifa anakua haishughulikii. Sasa nimeshangaa kwa nini Mhe. Waziri namjua kama hajahiji, basi yuko njiani kwenda kuhiji, kwa nini kesi hii anakuwa haishughulikii mpaka kutaka kufikia mahujaji wetu wanaweza wasiende kuhiji. Nimepata taarifa anazijua na barua ziko kwake, lakini anashindwa kulishughulikia suala hili mpaka analiingilia Makamu wa Pili.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aniambie ni lini ataiombea Zanzibar tuwe na *beitha* yetu ili kuondosha mgogoro wa mahujaji wanapotaka kwenda Makka, kwa sababu mkuu au Rais wa mahujaji wanapokwenda Makka anakuwa ni Sheikh Abdalla Talib, kule wenzetu wa Tanzania Bara taasisi zile zinakataa kumsikiliza, kwa sababu anatoka Zanzibar. Aniambie ni lini ataifanya Zanzibar tuwe na *beitha* yetu, ili mahujaji wetu waweze kwenda Makka bila ya kuwa na matatizo, kesi hii anayo na anaijua.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii pia inaratibu mambo ya Kadhi. Nawapongeza pia Makadhi kwa kada mbali mbali wa Wilaya, Mkoa, Mahakama Kuu, mambo ya kidini. Lakini Mhe. Mwenyekiti, natoa tahadhari, utafiti unaonesha talaka zimekuwa nyingi na talaka hizi kinamama wanakuambia hasa mtu kama humtaki unakwenda tu hapo kwa Sheikh mapenzi, sijui unafanyaje unachukua talaka yako. Sifikirii kama huu ndio utaratibu wa Kiislamu ulivyosema, kwenye aya kwenye msahafu, kwamba akienda tu na pia kuna harufu ya rushwa. Kinachonishangaza ni kwamba Kadhi wa Kiislamu anachukuaje rushwa, lakini ipo harufu ya rushwa tena ipo kubwa kwamba wanapewa rushwa ili atowe talaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kusema tusijione leo tuna uhai, umekubali kuwa Kadhi wa Kiislamu halafu unachukua rushwa, sijui siku ukifa utakaa wapi, sijui utakwenda kuyaona huko huko, lakini hii sio sahihi hata kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri lazima tulishughulikie suala la talaka zimekuwa zinatoka kama njugu, wanakwenda tu kinamama wanapewa talaka kesi haisikilizwi, akienda akisema kalivino kajivino anapewa talaka. Mheshimiwa hii sio sahihi, lazima tufuate kama Uislamu ulivyosema, kama vitabu vya sunna sahihi vilivyosema ili mwanamke apewe talaka kunahitajika nini, lakini sio tunazitoa talaka tu na kunatolewa rushwa. Mhe. Mwenyekiti, mambo haya yapo na mpaka baadhi ya shahidi nyingi zipo, tuwache kabisa kuzitoa talaka kama njugu kwa sababu *outcome* yake ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunao wastaafu. Unapokuwa mstaafu unategemea penye uhai na majaliwa, wengi wetu humu tutakuwa wastaafu na tutapokea pencheni za kustaafu. Mhe. Mwenyekiti, ukiwa mstaafu ni kwamba umeitumikia nchi hii katika hali kubwa sana, wazee wetu ndio waliotupindulia nchi hii, wazee wetu ndio waliotuweka hapa leo. Juzi nilisema hapa kwamba kabla ya Mapinduzi mwaka 1957 mtu wa mwanzo kuingia katika chombo cha kutunga sheria kama hiki mzalendo, mtu mweusi kama mimi alikuwa hayati Ameir Tajo Ameir katika nchi ya Zanzibar, tujuwe kwamba sote kumbe tulikuwa tunadhalilishwa nchi yetu wenyewe lakini kuna watu ndio mabwana walikuwa nchi hii, hata Mzanzibari mtu mweusi kama mimi alikuwa hayupo kwenye chombo cha kutunga sheria. Mtu wa kwanza kuingia ilikuwa mwaka 1957 hayati Ameir Tajo Ameir.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tujuwe umuhimu wa Mapinduzi matukufu ya Januari 1964 yamekuja kutukomboa, yamekuja kutuletea demokrasia. Kwa hivyo, wazee wetu hawa wametutoa mbali, wametutoa gizani, wametuweka kweupeni, leo hii mambo mengi tunayapata kwa sababu ya wazee wetu waliotupindulia nchi, wametuwekea nchi yetu vizuri, na leo tunaishi. Kwa

hivyo, wengine wamestaafu na wengine wametangulia mbele ya haki, wanapata mishahara ya kustaafu mishahara yao haipandi, wanasema iko pale pale wastaafu.

Mhe. Waziri nakujua ni muungwana sana na ni mtu mmoja mstaarabu na mzoefu sana katika kufanyakazi na mwalimu. Ukitizama historia ya Tanzania waliokuwa marais wengi wao ni walimu na sio Tanzania tu ni nchi nyingi duniani, mwalimu ndio mtu wa mwanzo nchi hii kumiliki gari. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri aangalie upya mishahara ya wastaafu wazee wetu. Mhe. Mwenyekiti, aangalie sana pencheni za wazee wetu waliostaafu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli haipendezi wazee hawa kwamba pencheni zao zimekaa pale pale na mishahara ya wafanyakazi inapanda yao wao iko pale pale kwa sababu wamestaafu. Mhe. Mwenyekiti, kwa leo sina mengi zaidi ya kusema. Lakini naomba sana aniambie Mhe. Waziri mambo haya atayafanya lini.

Jambo la mwisho Mhe. Mwenyekiti, Mahakama za Mkoa zimepewa miaka 7 kufunga. Lakini naomba sana kwenye kesi za jinai, kesi ya rushwa, kesi ya udhalilishaji na kesi ya mambo ya unga Mahakimu wa Mkoa tuwape miaka 30 mpaka 40, tuwape uwezo wa kufunga miaka 30 mpaka 40, ili tuweze kuwakomesha hawa wadhalilishaji, wauza unga ili nchi yetu iwe salama. Mhe. Mwenyekiti, naomba haya Mhe. Waziri aje kunijibu kwa kina. Kwa hivyo, naomba kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia 99.9, 00.1 nabakia nayo mpaka Mhe. Waziri aje kunijibu kwa kina. Namuamini ni mwana Mapinduzi na anayatambua Mapinduzi na kuyathamini, lakini naomba sana aje kunijibu.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Sasa naomba nimwite Mhe. Zainabu Abdalla Mussa Mwakilishi wa nafasi za wanawake kupitia kwenye ulemavu, lakini kabla ya Mhe. Zainab naomba niwataje wale wachangaji ambao wameomba niwape dakika tano tano ili na wao wachangie, kwanza nitamtaja Mhe. Said Omar Said wa Jimbo la Wingwi, akifuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri na mwisho kabisa atafuatiwa na Mhe. Said Soud ahsante Mhe. Zainab endelea.

Mhe. Zainab Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa hii adhimu kwa asubuhi hii ya leo na mimi kuweza kuchangia machache

katika Wizara hii ya Rais, Katiba na Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza na mchango wangu kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye aliyetuwezesha kufika sote hapa wazima na kunipa uwezo wa kuweza kuzungumza kuchangia machache kwa asubuhi hii ya leo, pia Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa na mimi leo fursa hii nimeipata tokea ilipoanza mijadala basi kwanza na mimi naomba nimpongeze Mhe. Rais wangu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein katika uamuzi wake kwa ukakamavu katika pando la mishahara……..

Mhe. Mweyekiti: Mhe. Zainab samahani kidogo Waheshimiwa Wajumbe naomba sana mchangiaji aliyesimama ni nafasi maalum za watu wenye ulemavu na sauti yake kidogo ina matatizo, lakini tukianza hivi kuzungumza sifikirii kama kile anachokisema Mhe. Waziri atakipata. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe hasa hasa Mhe. Gavu nawaomba sana waheshimiwa tumsikilize kwa hali yake, nawaomba sana.

Mhe. Zainab Abdalla Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pia niwape pole kwa wale wote waliofikwa na maafa wenzangu nikiwemo na mimi mwenyewe ya masika makubwa kwa mvua zilizonyesha, vile vile kwa wale wenzangu wote ambao tuliopatwa na maafa ya kimbuka kikali cha juzi kilichotokezea pia namuomba Mwenyezi Mungu awape subra waweze kusubiri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na hii Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume hii ya kurekebisha Sheria nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri akae na Tume yake pamoja na Mwanasheria Mkuu irekebishwe sheria au adhabu hii ya wadhalilishaji, ambao matendo haya wanayoyafanya ni matendo ya kikatili na matendo mazito sana, kwa sababu matendo haya yanawasabishia hasa watoto wanakatishwa kizazi au wanakatiwa maisha. Kwa hivyo Mhe. Waziri nilikuwa namuomba sana hii Tume yake irekebishe sheria hii ya adhabu kwa watuhumiwa hawa.

Vile vile nikiendelea mbele naingia katika Kamisheni ya Utumishi, Mhe. Waziri Kamisheni hii kuna baadhi ya taasisi zako nyengine hasa za watu binafsi ambazo hazijaweza kuzingatia kwa wafanyakazi wake kuwa na mikataba pamoja na kuwapatia bima za afya kwa wafanyakazi wao. Sasa nikuulize endapo watu hawa wakibainika sijui ni hatua gani za kisheria ambazo zinazochukuliwa kwa wafanyakazi wao waliokuwa hawakuwawekea mikataba

sahihi ya kuweza kufanya kazi zao vizuri na kujiamini na kupata bima za afya kazini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika Tume ya Utumishi Tume ya Utumishi na hasa sisi watu wenye ulemavu tuliambiwa kwamba tutawekewa vipaumbele katika sehemu hii itakapofika kipindi cha ajira. Lakini Mhe. Waziri naona katika hotuba yako hii haikuonesha hata sehemu moja au kipengele kimoja hususan katika hii tume ya kuona kwamba watu wenye ulemavu wamewekewa kipaumbele gani ambacho kitakachoweza kuwasaidia watu hawa kupatiwa ajira, ajira kwa watu wenye ulemavu ni jambo la msingi kwa binaadamu wa aina yoyote. Mhe. Waziri na sisi ni binaadamu au ni watu tuliokuwa ndani ya nchi kama binaadamu wengine tunahitaji ajira kama wanavyohitaji wenzetu, sasa leo wewe Mwanasheria unayedhibiti Katiba umeshinda kutuwekea hata kipaumbele kimoja cha kuweza kutusaidia. Je hizi Wizara nyengine zitaweza kutuajiri sisi watu wenye ulemavu.

Mhe. Waziri nakuomba sana tena sana naomba utusaidie kwa hii ajira ili na sisi tuweze kupatiwa ajira, kwa sababu ni vijana wengi hivi sasa wanasoma na hili tunalipigia kelele kila siku wanapata elimu ili wapate kuajiriwa na kujikwamua na maisha duni, lakini Mhe. Waziri naona bado hujaweza kutusaidia. Kwanza nimpongeze Makamu wa Pili kwa kutuwekea kipaumbele watu wenye ulemavu ijapokuwa idara yetu imo mule mule katika Ofisi yake, lakini katuwekea kipaumbele kikubwa sana na tumeridhika vizuri sana. Nilikuwa naomba pia na Mawaziri wengine na wizara nyengine nao waweze kutuwekea kipaumbele sisi watu wenye ulemavu, hususan suala la elimu na kupatiwa ajira sisi watu wenye ulemavu ni watu dhalili sana hatuwezi kupata ajira isipokuwa tuweze kusaidiwa.

Mhe. Waziri wa Katiba Sheria, Utumishi wa Umma nakuomba sana tena sana na pia nataka unipe majibu ya ufasaha kuhusiana Tume yako hii huenda, itakuwa itakuwa pengine kuna kipengele nilichokuwa sijakiona umeniwekea kipaumbele ambacho sijakiona. Kwa hivyo ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa mchango wangu huo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Zainab Abdalla Mussa nafasi za wanawake kwa watu wenye ulemavu, sasa naomba niwaite wale Waheshimiwa Wajumbe walioomba dakika tano lakini nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe zile dakika tano ziwe tano kweli kweli zisizidi baada ya hapo. Kwa hivyo naomba Mhe. Said Omar Said wa Jimbo la Wingwi nae dakika tano akifuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Naibu Waziri wa

Elimu Mmanga Mjengo Mjawiri na mwisho kabisa atafuatiwa na Mhe. Said Soud.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru Mwenyezi Mungu Jaalla Subhana Wataalam kwa kuniwezesha kufika katika kikao hichi leo hii Ijumaa, pia nikushukuru wewe pamoja na kwamba umenipa dakika tano tu kwa kunipa nafasi hii ya kuichangia hotuba hii iliyopo mezani saa hivi.

Lakini pia nichukue fursa hii kwa kutoa pole kwa wote waliopata msiba Arusha na Karatu, nimpongeze Mhe. Waziri, nimpongeze Mhe. Makamu Mwenyekiti kwa kuwasilisha, lakini pia nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi anavyoiongoza Zanzibar mpaka kufikia hali ya upendo katika nchi za ng'ambu. Dakika tano sijui nianze wapi lakini haya nianze na Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua kwamba Mahakama ni chombo cha kuwatafutia watu haki zao lakini sio watu tu mpaka wanyama, kwa hivyo Mahakama inahusika na haki za viumbe mimi niseme viumbe kwa sababu hata wanyama wana haki zao si kama Zanzibar ya zamani, Zanzibar ya zamani ilikuwa popote Mzanzibari atakapokwenda nje ya hii Zanzibar anakumbatiwa kwa mikono miwili, anapata heshima kubwa leo Wazanzibari walioko ng'ambo wengi matajiri kwa kuaminiwa kwa sababu anatoka Zanzibar kwa sababu Zanzibar inaonekana ni nchi yenye watu wenye ustaarabu, yenye watu waaminifu, yenye watu waadilifu.

Lakini leo hii akionekana mtu popote pale nje ya hii Tanzania akiulizwa wewe ni nani Mzanzibari watu watakuwa nashaka nae, kwa nini? Sababu leo Zanzibar wimbi kubwa la uhalifu lipo Zanzibar, la uhalifu wa kila aina kumuingilia mtoto ni uhalifu huo, kuvunja nyumba, kuvunja maduka ni uhalifu, ubakaji ni uhalifu huo, wizi ni uhalifu. Sasa haya yanachangiwa na nini na Mahakama ipo, sasa ningeomba Mhe. Waziri akubali mashauri yetu, mimi ningeshauri kama wanavyoshauri wenzangu kwamba hii Mahakama tuifanye sawa sawa na kazi ya nyota, nyota ina kazi tatu zote zina maslahi. Moja ya kutuletea muangaza tukaona, kazi ya pili ya nyota inalinda maadui faida hiyo, lakini la tatu inawaongoza wasafiri wa baharini, saa na Mahakama tuifanye hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, vipi tutaifanya ili ilete faida zaidi tuongeze hukumu katika miaka kifungo, tuongeze hukumu katika faini, leo sio wakati tena huu wa faini shilingi elfu kumi, elfu ishirini mpaka arubaini watu wanazo pesa hizo na ndio

yakashamiri matatizo Zanzibar ka sababu *fund* ile ni ndogo mno. Sasa tukiongeza *fund* ile ya malipo ya shilingi elfu kumi tukaifanya laki moja hanazo atarudi nyuma ataogopa, lakini elfu kumi anazo, shilingi hamsini elfu anazo kutoa. Kwa hivyo tutapoongeza hapa tutapunguza humuma pia tutaongeza pato kwa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti wenzangu wameshatangulia kusema na mimi niendelee kwa sababu mtu akianza kujenga nyumba na ajiri wako kama hiyo aliyojenga yeye husemi huyu kashajenga kajenga nyumba ya ghorofa mbili Mhe. Nadir mie sijengi tena aa na wewe unajenga ile ile. Mhe. Waziri Majaji wetu na Mahakimu wetu ndio ngao yetu hapa sasa hawa ngao huenziwa Mhe. Mwenyekiti, wameanza kutangulia kusema wenzangu na mimi nakubaliana nao kabisa tuwaenzi majaji pamoja na mahakimu kwa maslahi yao na pia kwa makaazi yao. Tuangalie mtu anamfunga mkosaji miaka mitano halafu jaji huyo huyo anakaa kibanda ambacho hakieleweki hapo ulinzi wake uko wapi hatujui yumo ndani ya hatari hapo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ambaye siye jaji siku moja kuna mtu mmoja alinikuta mimi naendesha pikipiki hivi karibuni sehemu ana gari akaja mpaka niliko, akasimama hafla pale akasema Mheshimiwa aaa baada ya leo nisije nikakuona tena unaendesha pikipiki nikija nikikuona unaendesha nitaichana mipira ukanifunge, nikamuuliza kwa nini akaniambia wewe ni Mheshimiwa……

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Karatu naomba umalizie.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kuhusu rushwa hili ni suala ambalo lazima kila siku tulitie midomoni kwa sababu ni janga kubwa, siku moja nilikua nimekaa sehemu ndani mna wanawake wawili…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Karatu

Mhe. Said Omar Said: Naam Mheshimiwa nakuomba dakika mbili tu….

Mhe. Mwenyekiti: Nimeshakuongeza dakika mbili…….

Mhe. Said Omar Said: Namalizia hii …..

Mhe. Mwenyekiti: Ndio maana nikataka umalize wende kwenye hotuba yako umalizie.

Mhe. Said Omar Said: Namalizia. Sasa wanawake hao wakawa wanazungumziana vipi wewe habari ya ajira naona ulikuwa ukihangaika sana, akasema aaa ajira ile mimi sina haja nayo lakini hawanioni mimi, akaulizwa kwa nini, ati aliniambia kwanza ananitaka, sasa nikasema aa siwezi nikafanya jambo la haramu mimi pale nikasema du ingekuwa huyu hajaolewa ningemuozesha mwanangu huyu lakini hawajui kama nipo.

Sasa ningetoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar mwanamke yoyote atakayekwenda kutaka ajira na akapata ajira kwa ajili njia mbaya hiyo ajira yake ni haramu na malipo yake ni haramu hana ibada yoyote atakayoipata.

Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said sasa naomba nimuite Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) akifuatiwa na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri na mwisho kabisa Mhe. Said Soud.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona kwa vile nimepewa dakika tano nitakwenda kwenye *specific issues* na mimi leo nitakwena sana kwenye nyaraka, lakini nyaraka hizi sitaki kusema ni zile zilizoundwa na Tume Maalum ya Kuchunguza nyaraka hapana.

Mhe. Mwenyekiti, nianze tu kuwapongeza Mhe. Waziri mwalimu wangu lakini na naibu wake pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya na tunaona jinsi gani tunavyofunguka sasa. Nimesema nakwenda kwenye nyaraka nataka nieleze umuhimu wa kumbukumbu ambazo zetu hizi za kitaifa ambazo tunazo, umuhimu wa kumbu kumbu hizi tunaweza tukasababisha kufanya tafiti nyingi sana lakini tukizipoteza kumbukumbu hatuna uwezo wa kuweza kufanya tafiti. Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, kumbukumbu zinaeleza wazi kuwa kuna Msweden mmoja wa mwanzo aliyepata maradhi ya malaria akafa hapa lakini wajukuu zake wamekuja wakatafuta kumbu kumbu zake *archives* wakazipata na ndio maana sasa tafiti nyengine zinaweza zikafanyika.

Lakini nyengine ni ndoa za zamani wanafanya utafiti kwa ndoa na *certificate* zile zilizotolewa zamani, lakini jengine kutafuta makaburi yale kama kule Unguja Ukuu kuna makaburi ya Wajerumani wameanza kutafuta sana watu. Lakini nataka kueleza athari ambazo zinaweza kutokea tukipoteza kumbukumbu zetu za taifa, halafu nitakuja na ushauri nini tufanye. Athari zenyewe moja kupotea siri za Serikali lakini nyengine kuvuja siri za Serikali ni athari za kupotea kumbukumbu. Nitaeleza ni kwa nini ninasema hivyo na

ntampa Mhe. Waziri baadhi ya picha ambazo nimezipiga, nimetembea katika Wizara mbali mbali zinavyotupwa kumbukumbu nyingi. Mhe. Mwenyekiti, kumbukumbu zetu hizi zimekuwa hazihifadhiwi ipasavyo na nilizungumza kwenye Ripoti ya Kamati ya mwezi uliopita, kuwa kuna watu wa *strong room* wanahitajika kupimwa afya zao hili Mhe. Waziri akija hapa hebu aweze kuniambia amefikia vipi.

Kwa mfano, tulikuwa tunatafuta vielelezo vya miaka hamsini ya Mapinduzi yetu Matukufu ya Zanzibar, lakini vingi vielelezo tulivikosa kutokana na hakuna utaratibu wa kuweza kuthibiti kumbukumbu zile tulihangaika sana kwenda kuzitafuta. Hapa nakuja kuna hata vielelezo vya maradhi mbali mbali. Kuna vielelezo vya malaria utakuta ukenda pale kumbukumbu zimetupwa sana, nataka kuona hata Mhe. Said Soud, alipopata maradhi, siyo Mhe. Said Soud huyu aa yule Mfalme, siyo MBM. Kuna kumbukumbu alipata maradhi na ukenda kuzitazama zile alipata wazimu na vielelezo vyake unaweza ukavipata. Hata hayati Baba Karume naye alipata malaria, ukenda Wizara ya Afya watu wa mwanzo, mwanzo waliopata malaria utakumbuka wapo. Sasa hofu yangu kuwa tukizitupa kumbukumbu hizi hatuwezi kufika vizuri na naomba sana, na naomba sana kuna Balozi wa mwanzo wa Uingereza wa Zanzibar, Fatawi bin Issa kumbukumbu zake zipo tunaweza tukazipata lakini tukitupa vitu kama hivi tutakosa urithi wa watoto wetu ili waweze kupata.*(Makofi)*

Sasa nimuombe sana hata maradhi ya kipindupindu yale yaliyotupiga mwaka huu, ukenda ukaangalia taarifa zake pengine huwezi kuzipata. Nitoe mfano, pengine hata OPF ya Mhe. Rais ukenda pale Wizara ya Afya, tupeni OPF yake unaweza ukaikosa, kwa sababu hatutunzi kumbukumbu. Sasa ushauri wa bure niiombe sana Serikali iunde jengo maalum la kuweza kuhifadhi kumbukumbu hizo. Mimi nadhani *Airport* mpya ile *Terminal II* tumeshindwa pengine, sasa tulipeleke basi tukaweke nyaraka zetu kule, tuzihifadhi mle ndani itakuwa aula ni jambo jema sana, kwa sababu tayari tushapata kitu cha kuweza kukitumikia tuzipeleke pale tukatunze kumbukumbu zetu kwa nia njema ya kuzihifadhi vitu hivyo.*(Makofi)*

Lakini nataka nitoe faida gani ambazo tunaweza kuzipata, faida ambazo tunaweza kuzipata kwanza kutoa haki ee kutoa habari za kihistoria, kutoa vielelezo vya muhimu kabisa kiuchumi, kibiashara na kimichezo. Mheshimiwa, niondoke hapo ingawa jengo hili halikutendewa haki, jengo hili sasa hivi limeizuliwa likiwa katika mvua za masika, lilikuwa halivuji na limepoteza nyaraka nyingi sana. Ningemuomba Mhe. Waziri aniliambie hapa.

Lakini niende Ofisi ya Mufti niwapongeze sana kwa kazi ambazo wanazifanya lakini niombe Serikali iwape *vote* yao waweze kuamua mambo mengi zaidi. Mhe. nakwenda haraka nishakuona huko.

Ofisi ya DPP. Mheshimiwa, niipongeze sana kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya Ofisi ya DPP kwa kushirikiana na Mahakama lakini katika hoja yangu ya madawa ya kulevya nilisema, kuna watendaji ambao sio waaminifu wanashirikiana na watendaji wa Mahakama ambao sio waaminifu kuharibu kesi zile za madawa ya kulevya. Niwaombe kwa pamoja tuunde Tume Maalum kuweza kuichunguza ili tuone, ingawaje Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ananisikia juu naye vile vile anahusikana na msiba huu.*(Makofi)*

Vile vile, niende kwenye *E-government* niwapongeze sana kwa kazi zao kubwa wanazozifanya Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nataka nitaje mafanikio ya *e-government* zaidi ya taasisi thamanini ziliunganishwa na Serikali mtandao wa kupata huduma za *internet,* kuwa na mfumo rasmi wa barua pepe wa mawasiliano ya Serikali, kuunganisha Taasisi za Serikali na mfumo wa malipo Serikalini *ifem.* Sasa haya yote ni mafanikio ambayo tumeyapata, katika *e-governmet* lakini bado, bado taasisi thamanini kuna taasisi nyingi sana Mheshimiwa atueleze ametuomba pesa nyingi sana humu mimi nataka hili nisikubaliane naye, nisikubaliane naye kabisa hili nataka nitoe asilimia nne niwe nazo mwenyewe nizishike mpaka atakaponipa jibu sahihi niridhike juu ya mtandao huu, tuna taasisi ngapi leo taasisi thamanini wamefanya kazi nzuri lakini ni pesa nyingi sana.

Lakini Mhe. nimalizie kwa DPP,

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa Mhe. Dimwa nakuomba sana dakika zako zimekwisha.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Waziri wako waliopandishwa madaraja, lakini wale Ma-DPP waliopandishwa madaraja hawajapata posho zao Mheshimiwa, nikushukuru sana lakini Mheshimiwa, aniambie lini watapewa posho zao za madaraja nikushukuru sana *time* ndogo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dimwa, naomba nimwite Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa hii na mimi nitakwenda moja kwa moja katika mada ambayo nakusudia kuizungumza na kuichangia katika wasaa huu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala hili la taasisi hizi za kisheria labda tuanzie katika ngazi ya Polisi, DPP na Mahakama, mara nyingi hupenda kueleza kwamba ili kuweza kutathmini utendaji wa kazi hizi, ni vyema tukazielewa kazi zake ni zipi hasa, kama hatuzielewi basi tunaweza tukalalamika kumbe taasisi zenyewe zinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa na tunaweza tukatoa sifa, kumbe taasisi zenyewe zinafanya vibaya. Kwa hivyo ni vyema sana tukaelewa majukumu ya msingi na taasisi hizo. Suala la uendeshaji wa kesi limeanza mbali linaanza kwenye tokeo, linakuja katika uchunguzi ambazo linahusisha na mashahidi, baadae suala hili likitoka katika kazi ya Polisi linakwenda katika Ofisi ya DPP.

Sasa Ofisi ya DPP moja katika kazi yao ni kujiridhisha kama tukio hili tuloletewa au dai hili tuliloletewa ni kesi au si kesi, hapa panatumika utaalamu, sasa wakati mwengine wanapoona kwamba hapana kesi, kwa maana kwamba ushahidi haupo basi hapo hawana sababu ya kupeleka Mahakamani, kwa sababu hii ni taaluma unapokwenda Mahakamani wakati umejiridhisha hakuna ushahidi unakwenda kuifedhehesha taaluma yako kabisa kabisa. Kwa hivyo, mimi niseme kwamba Ofisi hii inafanya kazi zake kwa uweledi mkubwa isipokuwa sasa kosa la ng'ombe kwa mbele anapigwa nyuma. Maana yangu nakusudia kwamba sisi wananchi ambao tunashuhudia matokeo yale hatuko tayari kushirikiana na taasisi zinazochukuza ukapatikana ushahidi ambao unaotoa shaka kwamba hiyo ndo hali halisi.

kwa hivyo, hapa ningechukua fursa hii kuwaomba wananchi wenzangu ambao pale tunashuhudia mambo yanapotokea tukubali kuwa mashahidi ili kuweza kuendesha kesi hiyo ili mtu aweze kupata haki zake. Lakini mimi naamini kwamba ushahidi unapopatikana ofisi hii hawana sababu ya kuzuia wala hawana sababu ya kucheleweshe, tatizo lipo hapo kwamba watu wengi hatuko tayari kutoa ushahidi na ushahidi unapopatikana na kesi ikapelekwa na pia Mahakama itafanya kazi yake vizuri zaidi.

Sasa mfumo huu wa Kimahakama kwetu sisi unadhohofika kutokana na kosa letu sisi wananchi kushindwa kushirikiana na vyombo vinavyohusika katika kutoa ushahidi. Ili kesi iwe kesi na sifa zake na hawa watu Ofisi ya DPP ndio wanaangalia, hawaangalii tokeo lilipotokea wanaangalia kila kilicholetwa katika Ofisi yao kinastahiki kuwa kesi au la! Ni kweli tunaona matokeo dhahiri yanatokea, lakini wao wanapopelekewa kule wanapelekewa vipi? Hii ni muhimu.

Na msingi wa kuwepo Ofisi hii ya DPP, hii historia yake kwamba ilianza katika miaka 1970, Uingereza kutenganisha baina ya ufanyakazi wa Polisi na kuchanganyisha na hukumu yaani wakati ule ilikuwa Polisi wanachunguza,

Polisi wanashtaki. Ili kutenganisha ndio ikapatikana dhana hii, ambayo tunaitumia leo. Na kwa kweli katika nchi yengine imeleta ufanisi zaidi sana sana katika masuala ya kesi, na kwetu sisi tunatarajia hivyo hivyo, endapo tutatoa ushirikiano katika kutoa ushahidi. Ndugu Mwenyekiti, ni kwamba masuala ya sheria ni sheria, wakati mwengine tunatamani hukumu ziwe kubwa miaka thalathini, arubaini kifungo cha maisha na kadhalika.

Lakini pia, naamini mimi kwenye sheria kuna usheria narejea tena kwenye sheria kuna usheria sasa huu usheria ndio unaoamua kwa tukio fulani kifungo kiwe miaka mingapi, faini iwe miaka mingapi na kadhalika, si kwamba ni fikra tu unasema miaka arubaini, hamsini ata. Sasa huu usheria ndio utaalamu wa sheria yenyewe. Sisi walimu tunasema katika fani ya historia ili jambo liwe historia lazima liwe na *historicity* na hapa lazima liwe na *legality*, sasa kwa kweli mambo hayo ni muhimu sana kuzingatia.

Mwisho kabisa kwamba napenda kusisitiza kwamba wananchi tuwe tayari kutoa ushahidi, ili vyombo hivi viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Kwa kumalizia naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia zote. Ahsante sana*.(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi hii na madhumuni makubwa ni kuchangia kwanza kwa asilimia 100% lakini ni kwa sababu tunazungumzia Wizara hii ya sheria, Wizara hii imebeba mambo mengi imebeba Sheria, imebeba Katiba, imebeba Utumishi na hatimaye Utawala Bora Mheshimiwa, haya makubwa katika nchi. Mambo haya hayawezi kupatikana bure bure, watu wote katika dunia wanahangaika kutafuta mambo haya sasa basi watendaji lazima wajitahidi sana katika kusimamia mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa wazi kwamba utawala wa sheria unakuwa na mambo matatu, kunakuwa na Bunge kama hili kunakuwa na Mahakama na kunakuwa na Rais, sasa Rais anakuwa na wasaidizi wake kama sisi Mawaziri na Watendaji wengine wote wanakuwa ni wasaidizi wa Rais, katika kuliangalia hilo kuna watu wanaoelewa hayo mambo matatu na kuna watu wasioyaelewa hayo mambo matatu na kuna watu wapo wapo tu, hawana habari ya Baraza hawana habari ya Mahakama hawana habari ya Rais wapo wapo tu katika nchi. Lakini kwa sababu tu za lazima katika kutendewa haki watu hawa sheria na utawala bora izingatie haki zao, kwa sababu nchi hii ina Katiba na Katiba zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nasema kila mtu atambuliwe kwa utu wake na kila mtu anastahiki kuheshimiwa kwa utu wake.

Katiba yetu inasema kwamba mambo yote haya, yatasimamiwa kwa nguvu za wananchi wenyewe na maamuzi ya wananchi ndio yatakayoheshimiwa. Mhe. Mwenyekiti mimi nataka niseme kwamba, katika kuzingatia Utawala Bora lazima tuhakikishe sheria inafanya kazi. Mimi nimeshangazwa sana, sana tena na naendelea kusema nashangazwa tena sana na nasema hivi kwa sababu mimi Jimbo langu liko Ikulu, watu kuilaumu Ikulu siko tayari. Sijapata kuona mtu kuwekwa kizuizini rumande miaka, saba hata kama kauwa Mtume basi hawezi kuwekwa miaka saba, rumande na nasema natoa ushahidi huu wapo watu rumande miaka saba, miaka mitano. Rumande yaani hukumu yake yote inamalizia rumande kama ni nusu ya hukumu anamalizia rumande utawala wa sheria hauendi hivyo, tunakaa hapa kutunga sheria lazima sheria zifanye kazi. *(Makofi)*

Haiwezekani kama mtu unamuweka rumande miaka saba, halafu unategemea mtu huyo atoke aje awe tayari kuitetea nchi hii na kuisemea nchi hii hata kuwa tayari mtu huyo. Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba mimi nina mambo makubwa na kuyazungumza lakini leo siyazungumzi. Nilitaka kujua kwa nini mpaka leo mwenye Meli ya *Spice Island* hajashtakiwa mpaka leo sijasema nitakuja kusema makusudi siku hiyo nakusanya vielelezo. Kwa sababu waliokufa Wapemba elfu mbili ndani ya Meli ile wale hawakuwa dagaa wale walikuwa watu, sasa sheria lazima Mheshimiwa, zifanye kazi lazima Mahakama zetu zifanye kazi na tusiwe tayari kumlaumu DPP kumbe kuna mambo ya sheria yanataka kuangaliwa kwa umakini sana. Mheshimiwa, Mwenyekiti najua dakika zako ni nyingi sana tano, lakini nataka niseme kwamba kwa kumalizia hilo ningetaka niseme kwamba sheria ndio roho ya utawala.

Sheria kama haipo, utawala unakuwa unayumba yumba, sasa sisi hatuwezi kuyumbisha utawala wakati tunatunga sheria. Nawaomba watendaji wote wa Wizara hii ya Sheria wajitahidi kufanya kazi zao vizuri vyenginevyo mimi sistosahamili, nitamwambia Rais mmoja mmoja huyu hafai, huyu hafai, huyu hafai, huyu hafai nitaoa moja kwa moja. Mhe. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said kwa mchango wako, Waheshimiwa Wajumbe, nami naomba nichukuwe fursa hii kwa kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia katika Hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma, lakini pia pongezi zangu niwapongeze, Waziri na Jopo lake lote la Wizara hii kwa Hotuba yao sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe niakhirishe kikao mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

(Saa 6.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11: jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwanza halafu atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu, baadaye nitampa Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Waziri wa Fedha karibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwakunipa fursa hii na mimi kupata nafasi ya kutoa mchango wangu, lakini na kutoa ufafanuzi kwenye masuala mawili matatu yaliyozungumzwa ambayo yamegusa kwa namna moja au nyengine Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kutoa pongezi nyingi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Nitoe pongezi hizi kwa kutekeleza ahadi yake ya kuwaongezea mshahara wa kima cha nchini wafanyakazi wa kawaida na wale wafanyakazi wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nimpongeze pia Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Jaji Mkuu, *DPP*, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mufti Mkuu, Kadhii Mkuu, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii na taasisi zake.

Mhe. Spika, niendelee kumpongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kazi kubwa sana aliyoifanya katika Ofisi yake ya kuziweka pamoja Sheria zetu zote, tokea mwaka 1980 mpaka 2015. Sheria zote zimewekwa pamoja na kwa kweli zimeturahisishia sana kufanya rejea katika sheria hizo lakini vile vile kuzitumia sheria hizo katika masuala mbali mbali.

Mhe. Spika, pia Ofisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu imeziorodhesha sheria zote ziliopo za Zanzibar tokea mwaka 1959 mpaka mwaka 2014. Uzuri wake kwamba sheria hizi zimewekwa kwa kila sekta. Kwa hivyo sasa hivi kila sekta inajua sheria zilizokuwepo tokea miaka hiyo na hadi sasa na zinatuwezesha kuweza kujua kama kuna mapungufu na kama ipo haja ya kufanyiwa marekebisho kwa baadhi ya sheria. Hivyo tunamshukuru sana Mhe.

Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri sana uliyoifanya na Ofisi yako ambayo kwa kweli imetusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, katika ufafanuzi kuna suala moja lilizungumzwa la kwamba serikali izingatie pencheni za wenzetu waliokwisha kustaafu. Niseme kwamba serikali inathamini sana mchango mkubwa uliotolewa na wafanyakazi waliofanya kazi kufikia umri wa kustaafu, nikiwemo na mimi mwenyewe kwa sababu tayari nimeshastaafu rasmi. Mhe. Rais kwa kuthamini hilo na serikali yake anayoiongoza, niseme kwamba imeliona hili na imelizingatia mbali ya kuongeza kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi wa kawaida na wale wa vikosi, lakini kutakuwa na zingatio maalum la kuongeza pencheni kwa wastaafu. Pia kutakuwa na zingatio maalum la wale viongozi walioshika nafasi mbali mbali na wakati ulipofika wa kustaafu walistaafu wakiwa na mishahara midogo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa hivyo hilo nalo limezingatiwa na nitamke kwamba tumetenga karibu bilioni 10 kwa ajili ya shughuli hiyo ndani ya mwaka 2017/2018. Kwa bahati kwamba utaratibu wetu mara hii umebadilika, ile bajeti ya serikali inasomwa baada ya mawizara yote lakini kwenye bajeti *highlight* nimetoa kwa waandishi wa habari taarifa hizi tayari tumeshazitoa. Ningemuomba Mhe. Mwakilishi aliyeuliza suala hili akajua kwamba limezingatiwa na serikali imeliona na italifanyia kazi katika mwaka 2017/2018.

Suala la pili Mhe. Spika, lililozungumzwa ilikuwa ni maslahi ya Mhe. Jaji Mkuu na kama nimelipata sahihi Mhe. Mwakilishi alitaka kujua maslahi haya nayo yatoke katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Niseme kwamba ni suala ambalo limejadiliwa sana wakati tunafanya marekebisho ya Katiba mwaka 2010 na wakati huo wenzetu waliona kuna haja ya kwamba fedha hizi au malipo haya ya mishahara ya Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama Kuu yahamishiwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo wakati yanafanyika mabadiliko ya Katiba yetu mwaka 2010 hayo yalizingatiwa.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 111(5) kimewataja au kimewaorodhesha wale wote ambao sasa mishahara yao itatoka moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Ndani ya Katiba imemtaja Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Spika, Jaji Mkuu, Jaji wa Mahakama Kuu, Kadhi Mkuu, Wajumbe wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, *DPP* na *CAG*, hawa wote wameorodheshwa kwamba mishahara yao inatoka kwenye Mfuko wa Serikali au Mfuko Mkuu wa Serikali na hicho ndicho kinachofanyika.

Mhe. Spika, la tatu lilizungumzwa suala la Afisi ya Mufti kuwa na *vote* yake. Hili ni jambo ambalo linazungumzika, ni Afisi muhimu. Mhe. Mjumbe alizungumzia kwamba serikali labda inaiona hii Afisi kama Afisi ndogo. Niseme wazi wazi kwamba serikali inaithamini sana Afisi ya Mufti ni Afisi kubwa sana na ina umuhimu wake mkubwa na ndio maana serikali imeitambua ndani ya mfumo wake wa kiserikali. Ni Afisi iliyopewa hadhi kubwa sana na sote ni mashahidi kwa hali hiyo juu ya hadhi iliyopewa Afisi hii kutokana na umuhimu wake.

Mhe. Spika, pamoja na kufikiria tuwe na *vote* yake. Mhe. Spika, ningependa niseme maneno machache na Waheshimiwa Wajumbe wanielewe kwamba zipo taasisi nyingi ambazo zinaomba kuwa na *vote* yake. Ndani ya Wizara ya Fedha tunakuwa na utaratibu wa kudhibiti kidogo idadi ya *vote.* Sasa hivi tuna *vote* karibu 41 ndani ya serikali, kwa serikali zenye ukubwa kama wa Zanzibar inaonekana kwamba hizo ni idadi kubwa ya *vote* na kuzi- *manage vote* hizo ni kazi kubwa. Pamoja na hilo kutokana na umuhimu wa Ofisi hii, bado serikali inaweza kufanya mazingatio maalum kwa Ofisi hii kuwa na *vote* yake, pamoja na hayo nnayoyazungumza.

Mhe. Spika, kakini yatahitaji kuitizama upya sheria ya Mufti Nam. 9 ya mwaka 2001. Itabidi tuiangalie kwa sababu kuna mambo itabidi yabakie. Tunapokuwa na *vote* kutahitajika kuwa na Muhasibu Mkuu, kuwa na Mkaguzi Mkuu, Mkaguzi wa Ndani thamani lakini pia kuwe na muundo na muundo wake itabidi ubadilike, kwa sababu sasa kutakuwa na Afisa Mas-uul, Mhasibu Mkuu, vile vile pengine kutahitajika kuwa na Idara ambazo zitakuwa chini ya huyo Afisa Mas-uul.

Mhe. Spika, kuwa na *vote* kutahitajika sasa kila mwisho wa mwaka kufungwa kwa mahesabu na kufanyiwa ukaguzi tofauti. Wizara sasa hivi ukaguzi unafanyika kwa Wizara nzima. Sasa hiyo kutenganisha inakuwa ni ukaguzi maalum wa Afisi ya Mufti. Hilo ningeomba nalo tulijue na tulione. Lakini kuna njia nyengine ambayo tunaweza tukaifanya, kama wasi wasi ni kwamba zile fedha zao pengine hazifiki kwa ukamilifu, pengine mara baada ya kujua kwamba bajeti ya Afisi ya Mufti ni kiasi fulani cha fedha kinaweza kikafanyiwa *ring fence* ile *sub-vote* yake ikawa *ring fence,* zikawa fedha zake zinatoka Hazina moja kwa moja zinaingia kwenye Afisi ya Mufti. Lakini bado *Accounting officer* ataendelea kuwa Katibu Mkuu. Kwa namna hiyo fedha hizo zikishakuwa *ring fence* haziwezi kutumika bila ya ridhaa ya Afisi ya Mufti. Kama hilo linaweza likafanyika hata ndani ya mwaka wa fedha wa 2017/18. Tukiweza kukubaliana hilo tunaweza tukalifanya na wao fedha zao wakazipata

kwa ukamilifu bila ya kuwa na *vote separate* ambayo itakuwa na mazingira ambayo kidogo tofauti.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nilitaka kutoa ufafanuzi kwenye baadhi ya maeneo, nitamke kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa mchango wako.,Ssasa naomba nimwite Mhe. Mwanasheria Mkuu ili na yeye aweze kusaidia kidogo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa ya kusema machache katika hoja hii iliyopo mezani ya Ofisi wa Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwa kuwa hii ni Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, nianze na mimi kuchukua fursa hii kwanza kwa kumpongeza mwenye Afisi ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya na ameifanya tokea mwaka 2010 alipokabidhiwa Urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na anayoendelea kuifanya mpaka sasa. Mengi ameyafanya sina haja ya kuyaorodhesha yote hapa, nikiyaorodhesha hapa nadhani dakika zote hizi zitakwisha kwa kueleza yale mazuri ambayo ameyafanya Mhe. Rais.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nimuhakikishie Mhe. Rais, kama sisi, mimi pamoja na wale wote ambao ametuchagua kumsaidia katika kazi hii, tutashirikiana naye, tuko pamoja na naye, tunafahamu *commitment* yake ambayo anayo kwa nchi hii. Sisi tutaendelea kushirikiana na yeye tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu zaidi yeye pamoja na famia yake, ampe uwezo zaidi, ampe subra na uvumilivu mkubwa. Maana kwenye kazi anayoifanya kama hana nguvu, kama hana subra na uvumilivu nadhani kungechafuka. Lakini kwa uvumilivu na subra yake leo, hii sote tunatoka nje tukiwa vifua mbele na tunasherehekea neema ambazo zipo.

Mhe. Spika, hivyo basi niwaombe sana Waheshimiwa Wajume tushirikiane na yeye katika kuhakikisha tunatimiza yale yote ambayo ameyadhamiria. Katika kushirikiana na yeye ni kuhakikisha kwamba tunapitisha bajeti hii kwa nguvu zote, tumuhakikishie kwamba tunampitishia bajeti hii ya mwaka 2017/18 kwa nguvu zote. Kama tunavyojua Baraza la Wawakilishini ni sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni Rais na sehemu ya pili ni Wajumbe wa Baraza. Sote sisi pamoja na yeye, tuna haki ya kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba yale yote mazuri ambayo ameyakusudia katika kipindi hichi kilichobaki cha

uongozi wake, basi tunamsaidia kuyatimiza na anayatimiza kwa kiwango cha hali ya juu kabisa. Kwa hivyo naomba kwa dhati kabisa nimuhakikishie hilo Mhe. Rais kama tupo pamoja na yeye na tutaendelea kumsaidi kwa nguvu zetu zote.(*Makofi*).

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba sasa niingie kwenye maeneo machache ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza na yale ambayo kwa kiasi kikubwa yamegusa Afisi ya *AG* na yale mengine ambayo yametaka ufafanuzi wa kisheria. Moja ni hili ambalo limezungumzwa na Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, nalo la kufungua Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba. Hili nimuhakikishie kwamba tumeshauriwa na Kamati na sisi tumelikubali. Sasa hivi tupo katika kutayarisha mazingira bora ya kutuwezesha kuhamia Pemba.

Mhe. Spika, sasa nimuhakikishie kwamba matayarisho hayo tunayo na tumeanza zamani, wakienda Pemba ile hoteli ya karibu ya *clove* ya zamani, *Archipelagos* kwa wanaofikia huko wanaijua, pembeni yake kuna kiwanja cha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Dhamira hii tunayo muda mrefu lakini hatutosubiri mpaka kiwanja kile kijengwe, tutatayarisha mazingira ili angalau na sisi tuweze kupeleka Mwanasheria mmoja, wawili au hata watatu ili na sisi tuwe na uwakilishi wetu Pemba. Kwa hivyo hilo niwahakikishie Kamati kama hilo tumelipokea na tutalifanyia kazi.(*Makofi*).

Jengine ambalo limezungumzwa ni la Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ambaye na yeye ni Mjumbe wa Kamati. Kwanza Mhe. Nadir ameendelea kusimamia hoja yake ambayo pia aliizungumza wakati wa hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nayo ni kuongeza maeneo ya adhabu ambayo itakuwa ni adhabu ya kifo badala ya adhabu ambazo zipo sasa.

Mhe. Spika, nimjibu Mhe. Naidir kama ambavyo nimemjibu hapo awali. Kwanza jambo hili na hoja hii inajadiliwa sana. Kuna wale ambao wana mawazo kama ya Mhe. Nadir Abdul-latif kwamba bado nchi yetu iendelee kuwa na adhabu ya kifo, lakini kuna wale ambao wana mtazamo tofauti wa kusema sasa adhabu hiyo imeshapitwa na kwa kuwa haki ya kuwa hai ni haki ya Kikatiba, sasa adhabu hiyo iondoshwe.

Sasa mjadala wake ni mkubwa, mjadala wake ni mpana na kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wanakumbuka, moja ya adhabu ambazo zilikuwepo hapa nchini ni adhabu ya viboko. Zamani mtu ilikuwa akihukumiwa na anapewa na adhabu ya viboko, lakini saa hivi sheria zetu imeondosha. Sasa na hili bado lipo kwenye mjadala.

Mhe. Spika, nimuhakikishie Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kama kwa sasa kama akisoma Sheria ya Dhabu kifungu cha 26, ataona adhabu ambazo Mahakama imetakiwa itoe. Moja ya adhabu ambayo Mahakama imetakiwa itowe kwa sheria zetu zilivyo sasa hivi, nayo ni adhabu ya kifo. Lakini adhabu hii inatolewa kwenye makosa maalum na makosa yenyewe ni kama mtu atahukumiwa kwa kosa la uhaini au kosa la mauwaji (*murder and treason*). Ndiyo makosa ambayo sasa hivi yanabeba adhabu ya kifo, lakini makosa mengine yote adhabu yake ama ni kifungo cha maisha ama kifungo cha muda maalum ambao umewekwa na sheria, adhabu na maeneo mengine. Kwa hivyo maeneo haya ya adhabu ya kifo ni kwa maeneo mawili lakini yeye anataka tu-*extend* zaidi ya maeneo haya.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Nadir Abdul-latif karibu Sheria hii itakuja kufanyiwa marekebisho. Sasa hivyo vifungu yeye aviweke tutakapokuja kufanya marekebisho hapa yeye aendelee kusimamia hiyo hoja yake. Kwa vile tunaamua humu kwa kura basi tutaamua, kama wengi watam-*support* Mhe. Nadir au wengi watakuwa na mtazamo wa kusema sasa Sheria ilivyo ibaki kama ilivyo.

Mhe. Spika, sasa hoja yake awe nayo lakini sidhani kama sasa hivi tunaweza tukaitolea ufafanuzi zaidi ambao huo nimeutoa, kama hilo jambo kwa sasa hivi lipo lakini maeneo ambayo adhabu yake na makosa yake yanayotolewa ni hayo mawili. Kosa la *treason* na kosa la *murder* lakini pia nimwambie pamoja na kwamba Mahakama imepewa uwezo wa kutoa adhabu hiyo lakini adhabu hii haitekelezeki mpaka kwa saini ya Mhe. Rais.

Adhabu hii ya kifo pamoja na kama Mahakama imeshatoa amri ya kwamba mtu huyu adhabu yake ni kunyongwa na kunyongwa kwa mujibu wa tafsiri ya Sheria yetu ni kwamba atiwe kitanzi mpaka afe. Lakini zoezi hilo halifanyiki kwa Sheria za sasa mpaka Mhe. Rais atowe agizo, ama anakubaliana na adhabu hiyo ama anasema vyenginevyo na amepewa uwezo huo kwa sababu Kikatiba Mhe. Rais amepewa uwezo na Katiba ya ama kufuta adhabu ama kupunguza adhabu au kufanya adhabu iliyotolewa iwe ndogo zaidi ya ile ambayo imetoka au iwe kubwa zaidi ya ambayo imetoka. Sasa na hili jambo bado mjadala wake ni mpana na nimuombe Mhe. Nadir hiyo hoja yake aikamate tutakapokuja kufanya marekebisho ya Sheria ya Adhabu Sheria Nam.6 ya mwaka 2014.

Hili la Mufti nadhani Mhe. Waziri wa Fedha amelitolea ufafanuzi vizuri na mimi nikubaliane na Mhe. Waziri wa Fedha kama hoja ambayo Mhe. Nadir amekuja nayo inazungumzika. Hoja ni nzuri na sisi tumeipokea lakini kama

alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha, kwa sababu Mufti ni Taasisi ambayo imeundwa kisheria, kwa mujibu wa Sheria Nam. 9 ya mwaka 2001. Na kwa sasa Sheria yenyewe haijatoa uwezo wa kuwepo kwa *vote* au kuwepo kwa msimamizi wa *vote* hiyo.

Mhe. Spika, ili hayo yatendeke itatulazimu kwanza tufanye marekebisho hayo ya Sheria, lakini wazo ambalo amelitoa Mhe. Waziri wa Fedha kama inawezekana ikawa *ring fence,* bajeti ya Mufti na akaipata bajeti yake kama ilivyo mpaka hapo atakapofanya marekebisho ya Sheria, mimi nadhani hilo ni wazo zuri, na ninawaombe waheshimiwa wajumbe tulipokee hilo kama ambavyo amelisema Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.(*Makofi*).

Jengine Mhe. Spika, niende kwenye hoja ya Mhe. Jaku na yeye kwa kiasi kikubwa ameanza hoja yake kwa kutoa sifa nyingi kwa Mahakama. Nadhani wenyewe wamesikia lakini kama hawajasikia Mhe. Waziri atakuwa amepokea sifa hizo kwa niaba yao. Lakini mimi sichangai kwa nini Mhe. Jaku amemwaga sifa hizi zote kwa Mahakama. Na kama asingefanya hivyo ningeshangaa sana, lakini wenyewe wamesikia na Mhe. Waziri atawapelekea salamu zao.(*Makofi*).

Lakini jengine alilosema ni kwamba sasa Ofisi ya *AG* tuwe na *Standard Format* za mikataba. Hili tunakubaliana naye na ndiyo tuko katika hatua ya kutayarisha hizi *format,* atakumbuka kama hivi karibuni tumefanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali. Kwa hivyo ndani ya Sheria ile imeorodhesha maeneo mengi ambayo yanatakiwa kutengenezwa mikataba. Na hivi karibuni nimewaagiza watendaji wangu wa Kitengo hichi cha Mikataba waende kwa wenzetu wa Tanzania Bara ambao tayari wao wameazisha utaratibu huu wakajifunze na wajue na sisi jinsi gani tutaanza na sisi kuwa na *Standard Format* hizi za mikataba.

Lakini niwaambie Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Mhe. Jaku kama kwenye mikataba hakuna kifungu kipya au jambo jipya ambalo utakuja nalo ambalo tayari halipo, mengi ya hii mikataba inaongozwa kama alivyosema yeye na *Standard Format* maalum. Lakini jambo ambalo linatukwaza ni usimamizi wa hiyo mikataba yenyewe. Hili ni jambo kubwa ambalo kwa sasa linatukwanza.

Lakini pia niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kama *Oversight Role* bado inaanza kwa wao pia kama ambavyo ipo kwenye Taasisi husika ambayo imetia saini ule mkataba. Kwa sababu kila miezi mitatu Kamati hizi zinatembea kwenye kila Wizara na kupata taarifa ya utekelezaji wa bajeti. Sasa niwakumbushe sana Waheshimiwa Wajumbe kama wanapokwenda kwenye hizi Kamati ile *Oversight Role* lazima waifanye vizuri. Lazima wahoji, lazima

wakafanye *site visit* na kwenye *site visit* lazima waulize, tusisubiri mkataba umetiwa leo unakuja kuhoji baada ya mwaka, wakati wewe kila mwaka unatembea kwenye hiyo wizara mara nne kwa mwaka. Sasa *Oversight Role* hii lazima tuifanye vizuri na lazima tushirikiana ili kuhakikisha sasa hii mikataba ambayo tunaifunga inasimamiwa na inaleta tija ile ambayo imekusudiwa.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni yale ambayo ameyasema Mhe. Abdalla Maulid Diwani na yeye ametushauri kwanza kuleta marekebisho ya Sheria ya Mikataba ambayo ni Sura ya 149, sheria iliyotungwa tarehe 1 Januari, 1917. Sheria imeshatimiza miaka mia na miezi kadhaa. Kwa hivyo hoja yake ni ya msingi, hoja yake ni ya kweli na nimuhakikishe kama Tume ya Kurekebisha Sheria tayari imeshafanya kazi hii ya kuipitia Sheria hii, na tayari imeshapeleka mapendekezo yake kwa Mhe. Waziri. Sasa Sheria hii pamoja na zile Sheria mbili ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezihoji, Sheria ya Mwenendo wa Jinai (*Criminal Procedure Act)* na Sheria ya Adhabu (*Penal Act).* Sheria zote hizi mbili pamoja na hii ya tatu niwahakikishie tutajitahidi kwenye mwaka huu wa fedha unaoanza ziwe zimefika Barazani. *(Makofi)*

Hakuna sababu ya Sheria hizi kuchelewa kuja Barazani, hakuna sababu na kwa kuwa sisi ni wasimamizi Wizara yetu inaitwa Ofisi ya Rais Katiba na Sheria, tuna wajibu wa kuhakikisha Sheria zote ambazo zinahusu taasisi yetu basi tunazifanyia kazi kwa kasi na tunazileta Barazani mara moja, ili na hizi Wizara nyengine sasa zifuatwe kasi za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Kwa hivyo nawahakikishia Sheria hizi tatu kwenye mwaka huu wa fedha tutahakikisha zinaletwa hapa Barazani na watendaji nadhani huko juu wamenisikia, kama nimeshatoa ahadi ya Sheria hizi kuja Barazani. Sasa wasije kuniangusha, wakiniangusha na mimi nitazifanya kama anavyotaka kufanya Mhe. Said Soud kwenda kwa Mhe. Rais. Kwa hivyo hilo niwajibu hivyo Waheshimiwa Wajumbe kama tutashirikiana na Mhe. Waziri kwa kuhakikisha Sheria hizi tunazileta na zinafanyiwa kazi vizuri. *(Makofi)*

Eneo jengine ambalo linataka ufafanuzi wa kisheria ni hili ambali amelizungumza Mhe. Hassan Hafidh maarufu *DAISPORA*, na yeye kimsingi amezungumzia maeneo ambayo Mahakama imepewa uwezo wa kutoa dhamana na yale maeneo ambayo Mahakama haikupewa uwezo wa kutoa dhamana. Na yeye amezungumzia kwenye haya maeneo ya *Non Bailable Offence* na ame-quo*te* kifungu cha 150. Nimwambie ni kweli kifungu cha 150 kimeorodhesha makosa matano ambayo makosa haya hayatakiwi kupewa dhamana, nayo ni:-

1. Moja ya kosa hilo mtu akishitakiwa nalo ni la mauwaji, kosa hili halitakawi kupewa dhamana,
2. Ni uhaini halitakiwi kupewa dhamana.
3. Wizi kwa kutumia silaha, nalo hili halitakiwi kupewa dhamana
4. Umiliki wa silaha kinyume na utaratibu, nalo hili halitakiwi kupewa dhamana
5. Ni madawa ya kulevya, nalo pia hili usafirishaji wa madawa ya kulevya nalo hili halitakiwi kupewa dhamana.

Lakini nimwambie Mhe. Hassan tutapoleta Sheria hii awe makini kusoma vifungu vilivyokuwemo ndani ya Sheria hii, pamoja na kwamba Sheria imesema haya hayatolewi dhamana. Lakini ukisoma kifungu cha 150 (4), kimetoa uwezo kwa Mahakama kutoa dhamana kwa makosa haya pia. Sasa nimuombe sana Mhe. Hassan azingatie pale ambapo tutakuja kufanya marekebisho. Vifungu hivi visije vikampita halafu akasema aah! hatukuwa makini, azingatie sana na sote ambao tumekuwa tunasimiamia hoja hizi, tuzingatie sana pale ambapo tutakuja kufanya marekebisho ya Sheria. Mengine haya ya kiutawala nitamuachia Mhe. Naibu Waziri na Waziri wazungumzie na wayatolee majibu yao.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa naomba sasa nimwite sasa Mhe. Naibu Waziri (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia leo hii kusimama hapa leo katika kujadili Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, vile vile naomba uniruhusu kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Pangawe kwa kuendelea kuniunga mkono katika harakati mbali mbali za kuimarisha jimbo letu pamoja na taifa letu kwa jumla, pamoja na hayo naomba pia niwape pole wananchi wangu wa Jimbo la Pangawe kwa kupatwa na maafa makubwa ya kubomoka nyumba zao kutokana na upepo mkubwa ambao ulisababisha zaidi ya nyuma 96 kuharibika katika Jimbo hilo la Pangawe na vile vile niwape pole wale wakazi wa Jimbo la jirani yangu, kwa

maana Jimbo la Mwanakwerekwe kwa wale ambao pia wamepata na kadhia hii.

Mhe. Spika, vile vile nishukuru viongozi mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuja kutufariji katika Jimbo letu baada ya kupata maafa haya. Kwa kweli wananchi wa Jimbo la Pangawe tumefarijika sana na sisi hatuna la kuwapa lakini Mwenyezi Mungu Inshaallah atawaongoza zaidi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi sasa nije moja kwa moja katika kuzugusa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wawakilishi walizitoa na ambazo vile vile wanahitaji kupata maelezo ya kina.

Mhe. Spika, miongoni mwa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wawakilishi ni kwamba imeshauriwa Serikali ihakikishe ujenzi wa jengo la Mahakama ya Tunguuu unakuwa wa kisasa ili kukidhi haja inayokusudiwa. Mhe. Spika, ushauri huo tumechukua na Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018, imeshatenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mahakama hiyo.

Mhe. Spika, sambamba na hayo pia hoja nyengine imekuja ya kwamba imeshauriwa majengo ya Mahakama yafanyiwe ukarabati ili kuimarisha mfumo wa utoaji wa haki, ikiwemo Mahakama za Mfenesini, Mwanakwereke, Wete na kadhalika.

Mhe. Spika, hatua za kufanyia ukarabati majengo ya Mahakama zimeanza kuchukuliwa kwa kuanzia na Mahkama ya Mwanakwerekwe kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017. Mahkama ya Mfenesini na Wete zitafanyiwa ukarabati kadri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni ushauri ambao umetolewa kwa Ofisi ya *DPP* kupatiwa kibali cha uwajiri wa Waendesha Mashtaka na kuimarisha Ofisi ya Pemba.

Mhe. Spika, Ofisi ya *DPP* imeshapewa kibali na imefanya usaili kwa waombaji 72 na wanasheria 13 wamechaguliwa na hatua za uchunguzi, yaani *vetting* zinaendelea. Sambamba na hilo kwa upande wa Pemba Ofisi inaendeleza kufanya matengenezo kwa jengo linalotumika hivi sasa ili kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo iliibuliwa na Wajumbe ni kwamba imeshauriwa kuwepo na mashirikiano kati ya Mahakama, *DPP* na Jeshi la

Polisi kuhusu udhalilishaji na madawa ya kulevya. Mhe. Spika, mashirikiano katika Taasisi hizo yataimarishwa zaidi na Ofisi itahakikisha kwamba inasimamia Taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Kuhusu madawa ya kelevya Serikali imeunda Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya ambayo Mwenyekiti wake ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, ushauri mwengine pia ulitolewa kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wapewe mishahara sawa bila ya kuzingatia vigezo vya elimu zao, walipwe kwa kigezo cha kazi zao. Mhe. Spika, ushauri huo umepokelewa na taratibu zinaandaliwa kulifanyia kazi suala hilo. Mhe. Spika, sambamba na hoja hizo pia ilitolewa hoja kupitia kushauriwa Mahakama ya Ardhi kupatiwa jengo linalokidhi haja au mahitaji ya Mahakama hiyo. Mhe. Spika, ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Spika imeshauriwa pia kutolewa maamuzi mapema kesi za mirathi ili waathirika waweze kupata haki zao mapema. Mhe. Spika, Ofisi inaendelea kuchukua juhudi maalum kuhakikisha kwamba kesi zinazohusu mirathi zinafanyiwa maamuzi haraka kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na miongozi iliyopo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo liligusiwa pia ni suala la usafiri. Suala la usafiri ni kitu muhimu sana basi nalo pia tunalichukua na pale ambapo Serikali itakuwa na uwezo wa kuzipatia taasisi zetu gari basi Serikali haitokuwa nyuma kufanya hivyo. Kwa sababu mara zote Serikali inataka kuwarahisishia wananchi wake kuwa katika mazingira mazuri zaidi na sio kupata tabu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache na mimi niseme kwamba naunga mkono hutoba hii ya Mhe. Rais, samahani naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora asilimia kwa mia juu ya mia.

Nashukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri, Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite mtoa hoja ili aje sasa ahitimishe hoja yake Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya wote nichukue nafasi hii kumshukuru Subhana wa Taala Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii kukutana hapa na

kuendelea na shughuli zetu za Kikao chetu cha Baraza katika suala zima la kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala.

Mheshimiwa nashukuru sana lakini pia nichukuwe nafasi hii Mhe. Spika, fursa hii kuwashukuru kwa dhati wenyeviti wa Kamati mbili za Baraza la Wawakilishi, ikiwemo Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum na Kamati ya *PAC* kwa michango yao ambayo ililenga kutoa ushauri, maelekezo kwa Idara na Taasisi zote za ofisi hii. Michango yao imeonesha kwa kiasi gani Kamati hizi zilivyokuwa mahiri katika kutekeleza kazi zao.

Mhe. Spika, kazi zao kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inafikiria malengo na matarajio yake kufikisha huduma kwa wananchi.

Mhe. Spika, pia naomba kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza lako la Wawakilishi hususan wale waliopata fursa ya Baraza la Wawakilishi kuchangia na maelezo na hoja mbali mbali na kuuliza masuala mbali mbali ya kutaka ufafanuzi.

Mhe. Spika, hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2017/2018 imepata bahati ya kuchangiwa na jumla Wajumbe 41, wajumbe 23 wamechangia kwa kusema na Wajumbe 18 wamenileta kwa maandishi.

Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niwataje.

Waliochangia kwa kusema moja kwa moja hapa hapa Barazani ni:

1. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
2. Mhe. Shaib Said Ali
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
5. Mhe. Hidaya Ali Makame
6. Mhe. Abdalla Ali Kombo
7. Mhe. Rashid Makame Shamsi
8. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
9. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
10. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
11. Mhe. Simai Mohammed Said
12. Mhe. Shehe Hamad Mattar
13. Mhe. Ali Suleiman Ali

14. Mhe. Ali Suleiman Bakar
15. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
16. Mhe. Zaina Abdalla Mussa
17. Mhe. Said Omar Said
18. Mhe. Mohammed Said Mohammed
19. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
20. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
21. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali
22. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
23. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
2. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
3. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
5. Mhe. Salma Mussa Bilal
6. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
7. Mhe. Mgeni Hassan Juma
8. Mhe. Asha Abdalla Mussa
9. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
10. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
11. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
12. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
13. Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
14. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
15. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
16. Mhe. Hamza Hassan Juma
17. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote na kama nitalinganisha mwaka jana na mwaka huu, basi *Alhamdulillah* uchangiaji umekuwa ni very *constructive* ukilinganisha na mwaka jana. Mwaka jana kidogo jazba na hii Wizara ilikuwa mpya tulivamiwa vamiwa na mambo mengi. Sasa kidogo tumejirekebisha rekebisha

mwaka huu kidogo inatia moyo. Nashukuru sana wachangiaji wote wamechangia vizuri na nawaahidi wale wote ambao walitupa ushauri kwa njia moja au nyengine tumeuchukua na tutakwenda kuufanyia kazi kilillahi taala.(*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini naomba nichukue nafasi hii kwa ufupi kabisa nieleze kwa muhtasari, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwanasheria Mkuu amenisaidia sana kujibu hoja za kisheria. Natarajia hata nikimaliza miaka yangu mitatu, minne, mitano iliyobakia hii *inshaallah* na mimi nitakuwa Mwanasheria mzuri sana. Nimejifunza mengi na nimeelewa mengi.

Pia nimshukuru sana Naibu Waziri wangu Mhe. Khamis Juma Mwalim kwa kazi nzuri anayoendelea kunisaidia na anayoendelea kuifanya. Pia na yeye amenisaidia maeneo mengi sana ambayo sina haja ya kuyarejea kwa kunusuru wakati. Lakini kuna suala zima nataka nianze nalo suala la Mahujaji, nimeona nianze na hilo.

Mhe. Spika, wengi wamezungumza kwamba wanataka kujua ufafanuzi suala la Mahujaji, miongoni mwao Mhe. Hassan Khamis Hafidh na aliniombea Mungu pengine na mimi kuna siku nitakwenda Hijja vile vile. Lakini napenda nimuhakikishia tayari nishafanya Hijja tokea 1999 huwa najitambulisha kwa mwalimu lakini ningeweza kujitambulisha kwa Al-hajj vile vile. Lakini kwa mpaka sasa hivi najitambulisha kama ni mwalimu wa kawaida tu.

Napenda nikuhakikishie kwamba Zanzibar haidaiwi na taasisi yoyote ya Saudi Arabia. Sisi Zanzibar katika vikundi vyote vya Hijja vile basi Zanzibar haina deni. Tatizo lilotokezea kwa sababu suala hili la Hijja tumeungana na wenzetu wa Tanzania Bara, taasisi inayotambulika ni ile ambayo inafanya kazi chini ya serikali. Kwa hivyo Katibu Mtendaji wetu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana yeye ndiye Mwenyekiti wa hilo jopo lenyewe.

Kwa hivyo mambo yote yanayokwenda kule Saudi Arabia, Katibu Mtendaji wetu ndiye anayekwenda kusimamia masuala yale. Sasa baada ya kutoa fununu hizi kwamba baadhi ya taasisi zetu zinadaiwa, tumelifanyia kazi kwa nguvu zetu zote na tumepata uhakika kwamba hakuna taasisi ya Zanzibar inayodaiwa hata moja. Lakini tumekaa na tumeanza kufikiria kwa nini tusirudi kama ule utaratibu wetu wa zamani tukawa na taasisi yetu wenyewe, kwa sababu sisi tayari serikali ndio inayosimamia suala hili. Kwa hivyo tayari tumeshamwita Katibu Mtendaji na nimeshakaa na watendaji wenzangu wa Wizara yetu ya Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma tunalifanyia kazi *serious* jambo hili ili kuona mwakani tukijaaliwa *in shaa Allah,* basi tunakwenda kwa taasisi kama

Zanzibar bila ya matatizo yoyote. Mhe. Spika, lakini mwaka huu tunakwenda tusiwe na wasi wasi mambo yote yameshakuwa *cleared* hakuna mzozo na Mahujaji wetu watakwenda kufanya ibada ya Hijja kama kawaida.(*Makofi*).

Mhe. Spika, jambo la pili nataka nilizungumze suala la Vyuo na Misikiti. Kumetokea tatizo kubwa sasa hivi watu kugombania Misikiti, limekuja suala wanagombania kitu gani? Tatizo kila mmoja anataka apate hii nafasi ya kuongoza ukubwa. Sasa mengine ni mazito sitaki kuyasema hapa, lakini wakati mwengine Misikiti hii inatumiwa vibaya. Sasa hutokezea watu waliokuwa na nguvu zaidi na ushawishi zaidi, wakawazidi nguvu wale wenzao, wakaanza sasa kuongoza wao. Mimi nakubali Mhe. Abdalla Maulid Diwani alikuja na timu yake ya Jang'ombe pale kuna Msikiti ule wa Kidongo Chekundu na Misikiti mengine na juzi nimepata mwengine Mwanakwerekwe bado kuna matatizo. Lakini suala hili linataka fatwa nzuri na busara nyingi sana. Suala la dini si suala la kuchezea chezea sana, ukitoa maamuzi utoe maamuzi ambayo yatakidhi mahitaji ya watu wote wataridhika ingawa si rahisi. Kwa hivyo tutajitahidi mizozo ile kuitatua kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Spika, kuna Mhe. Hidaya na wengineo walizungumza suala zima la kuwapatia misaada vyuo vya Kur-ani, misahafu. Tumekuwa na utaratibu huo na *in shaa Allah* mimi namuahidi yeye mwenyewe kwanza kama alivyosimama akasema misahafu tutampatia tukijaaliwa. Na utaratibu huu wa kugawa vifaa tende, nyama ya kondoo na mambo mengine yanayohusiana nayo, basi kuna utaratibu wa Kamisheni ya Wakfu ndio wanaosimamia. Sisi Waheshimiwa Wawakilishi tusije tukaingia kwenye jambo kama hili, tuwaachie Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana wana utaratibu wao.

Hivi sasa tayari tumepata bahati tumepata tende tani 100 na tumeshazigawa, yaani kiutaratibu mgao tumeshaufanya na hapa ninayo orodha yote ya tende zote zitakavyogaiwa Kiwilaya, sitaki kusema mmoja mmoja. Sasa Waheshimiwa kama mna *interest* ya kwenda kujua tu na sisi tuone tende zile zinavyogaiwa, basi Mheshimiwa kwa ruhusa yako naomba nitaje kidogo hizi tarehe na mahali penyewe ili Waheshimiwa waende wakashuhudia hizo tende. Najua madhumuni yao ni kitu gani, kwa sababu na wao wakionekana pale si vibaya hata mimi ningependa niende vile vile.

Mgao wenyewe kwa Wilaya ya Magharibi "A", itakuwa siku ya Jumatatu tarehe 22/05/2017, mahali Wilaya Mwera. Wilaya ya Magharibi "B" ni siku ya Jumatatu tarehe 22 Mwanakwerekwe, Jumanne tarehe 23/05/2017 Wilaya ya Mjini, Amani kwa Wazee, Jumatano tarehe 24 Wilaya ya Kaskazini "A", Wilayani Gamba na Jumatano Kaskazini "B" Wilayani Mahonda na tarehe 25

Alhamis Wilaya ya Kati, Wilayani Dunga na Alhamis tarehe 25 Wilaya ya Kusini, Wilayani Makunduchi.

Sasa hizo jumla ya tani zote au maboksi yote yatakayogaiwa Unguja na Pemba ni 5000. Kwa hivyo Waheshimiwa hizo ndio taarifa ili na nyinyi mshiriki kikamilifu katika ugawaji ili mtu asinung'unike nung'unike sana.

Mhe. Spika, tutajitahidi kama itakavyowezekana pale ambapo panahitajia mambo ya kugawana misahafu na mambo mengine, nawashauri Ofisi ya Mufti basi tulizungumze suala hilo kwa makini tusaidiane na tushirikiane.

Kuhusu habari ya Mahakama ya Tunguu na nyenginezo zimezungumzwa na *inshaallah* tukijaaliwa kwa mujibu wa ile ramani na michoro tuliyoiona ya Mahakama ya Tunguu itakuwa ya kisasa kabisa. Mhe. Wanu Hafidh Ameir tunakuahidi kwamba Mahakama yetu itakuwa ya kisasa na tusihangaike hangaike tutakuwa na Mahakama ya kisasa kila kitu kitakuwa humo humo tukijaaliwa wala hawatobanana tena pale. Mambo yatakuwa mazuri tuombe Mwenyezi Mungu tu na bajeti tayari ishatengwa kwa ajili ya kazi hiyo kwa kuanza angalau michoro yake na mambo mengine. Mhe. Mwanasheria Mkuu amenisaidia sana suala la sheria kama nilivyosema tujitahidi na sisi tuwe makini.

Mhe. Spika, kuhusu Chuo cha *IPA,* nataka nizungumzie kidogo kuhusu *IPA* imezungumzwa kwamba wana tatizo la usafiri. Suala hili tunalielewa na Mwenyezi Mungu akipenda tutalifanyia kazi kwa Pemba na Unguja. Tukumbuke kwamba kuanzisha chuo Pemba tumeanzisha kwa makusudi, kwa sababu mnakumbuka hata tulipoanzisha Chuo cha Ualimu kule Pemba cha Benjamin Mkapa, kilianza na matatizo mengi sana. Leo hebu tutizame juhudi alizofanya Dkt. Ali Mohamed Shein tumekihamisha chuo kile cha Wete pale tumekipeleka Mchangamdogo, ni chuo cha kisasa kabisa. Na *Alhamdulillah* Chuo cha Ualimu kiko pale na sasa hivi ni sehemu ya tawi la *SUZA* tumeki-*avail* mpaka kimefika hatua hiyo.

Mhe. Spika, kwa hivyo mwanzo mwanzo tulipata matatizo lakini sasa tunashukuru mambo mengi sana yametatuka katika suala zima la chuo kile na sasa hivi tunaahidi chuo hiki cha *IPA* Pemba tutakiimarisha na ikiwezekana tutajenga hata jengo jengine Pemba kama tulivyojenga hapa Unguja Tunguu kule. Na hilo jengo la Tunguu lenyewe nalo tumeshakamilisha na pale Mizingani pana matatizo, lile jengo ni bovu tutawahamisha tutawapeleka Tunguu kwa lengo la kupata taaluma nzuri, na suala la usafiri tutalishughulikia ipasavyo.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala zima la sheria mbali mbali ambazo *AG* amezitolea ufafanuzi. Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema alifanya juhudi moja kubwa sana kila wizara, kila sekta imepelekewa taarifa ya sheria zake kwamba wazijue sheria hizo na waziangalie, na zile ambazo wanahisi zifanyiwe marekebisho basi zifanyiwe marekebisho. Ni kweli sheria zimekuwa za siku nyingi zinahitajiwa kufanyiwa marekebisho. Namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri aliyoifanya hiyo.

Mhe. Spika, hapa pia pametolewa masuala ya kuimarisha nyaraka. Nataka nizungumze kidogo, limezungumzwa la nyaraka. Mhe. Abdalla Ali Kombo ametaja zumari ya Bazungu na akaigiza hata vile inavyopigwa. Mimi kusema kweli namjua sana huyu mzee namfahamu na ninamkumbuka alivyokuwa anapiga zumari yenyewe. Lakini hapa hatuzungumzii suala la zumari, tunazungumzia suala nyaraka. Mhe. Mohammed Said Mohammed amezungumza na namshukuru sana kaniletea picha nyingi sana za majadala, nyaraka zile ambazo zimewekwa ovyo ovyo. Napenda nimuhakikishie kwamba kazi ile tayari serikali ilikuwa iilikwishakuifanya, imeshaifanya vipi? Imeshapiga picha katika maeneo mbali mbali na tunajua wapi pana hitajia msukumo na sasa hivi timu yetu ya nyaraka inapitia katika Ofisi mbali mbali kuwahimiza ili kuweka kwenye utaratibu unaokubalika.

Lakini pia napenda niwaombe Waheshimiwa wote Mawaziri na Manaibu Mawaziri na watendaji wengine katika sekta mbali mbali Unguja na Pemba katika majengo yetu ya serikali, basi yale majalada yale yanayomaliza muda wake yahifadhiwe vizuri kwa sababu ile ni historia kuna siku yoyote serikali itahitajia kufanya *reference* kwenye maeneo hayo.

Mhe. Spika, pia nataka nikuhakikishieni kwamba jengo la nyaraka lile limefanyiwa ukarabati mkubwa sana sasa hivi, na amezungumzwa yule mtu ambaye anaishi ndani ya eneo lile. Napenda nikuhakikishieni tayari serikali imeshafanya tathmini na bei imeshawekwa na wakati wowote kuanzia sasa hivi tunatarajia yule bwana atapewa haki yake ataondoka na pale eneo lile litakuwa tupu, litakuwa kwa ajili ya makaazi ya nyaraka.

Mhe. Spika, tunashukuru hivi sasa kila kitu kiko katika *line* yake pale nyaraka. Kweli wataalamu wetu wale hasa kwenye *strong room* utaona hivyo lakini tumejitahidi sana kuwapatia fursa mbali mbali na tumejitahidi kuwaangalia vizuri, maposho nyeti na wengineo tutazidi kuwapatia wanaofanya katika maeneo kama yale na maeneo mengi tumefanya hivyo. Kwa hivyo watulie wajue tu mambo yao yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, pia napenda nikuhakikishieni kwamba jengo lile sasa hivi liko salama na kila kinachotendeka pale tunapata taarifa. Na nakuombeni sana mtapopenda kwenda kutembelea maeneo ya pale basi tupeni taarifa ili tushirikiane twende pamoja mkayaone yale mambo yaliyokuwemo ndani *inshaallah*. Wala hakuna matatizo hatumzuii mtu lakini mjue tu kwamba taasisi za serikali ni nyeti na huwezi kwenda tu bila ya kutoa taarifa kwa wahusika ili tushirikiane na wewe. Lakini ni vizuri na mimi nakushaurini Waheshimiwa, nikushaurini sana kwenye Baraza hili nashukuru Mungu mimi nimo ndani mwaka wangu wa 17 sasa hivi humu ndani na *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu akipenda natarajia nitafika 2020 niwe hai, nitaomba tena ridhaa ya wananchi wangu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, makofi hayo kwamba watu wameridhika na wanasema bado niendelee. Madam wananchi wa Jimbo la Makunduchi bado wananipenda, wana imani ya Chama cha Mapinduzi sina mashaka. Wanakipenda Chama cha Mapinduzi, wanampenda Rais wao, wanapenda viongozi wao na nawaahidi tutaendelea kuwatumikia mwisho wa uwezo wetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninachosema hapa suala la nyaraka nitoe ufafanuzi wa hii zumari ya Bazungu kidogo ifahamike. Kweli Mheshimiwa alilizungumza hapa, tumejaribu kutoa ufafanuzi wetu wa kina kabisa jambo lile. Lakini tatizo hili sasa limegusa nchi mbili, mambo ya kidiplomasia, wale watu wa diplomasia wanalijua. Tumeshafika hatua nzuri sana sasa hivi na kuna ujumbe maalum ambao nashukuru Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini alikuwemo katika ujumbe huo amefuatana na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wakati huo walikwenda na wameahidiwa kwamba hizi *documents* zipo na kinachofanyika sasa hivi na tumefika hatua nzuri, tayari mawasiliano wameshafanya mpaka Makamu wa Pili wa Rais keshaandika barua kwa Waziri wa Mambo ya Nje ili tuandae siku twende tukachukue *documents* zetu tuje nazo. Na tunaahidi siku ambayo tutazileta tutakuja kutoa taarifa rasmi Barazani Mhe. Spika, kwamba zile *documents* ni hizi hapa, hatuwezi kuidanganya Serikali, isipokuwa ni taratibu za kiserikali za kidiplomasia lazima twende nazo, tuwe na subra, hakuna jambo lisilowezekana ni wakati tu kufika basi na muda wenyewe utimie. Kwa hivyo naomba sana hilo ikiwezekana tulifikirie.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mishahara tumezungumza tayari limetolewa ufafanuzi mzuri na mimi nalitolea ufafanuzi. Marekebisho haya yaliyofanywa ilikuwa lengo ni kwa ngazi ya kima cha chini, lakini mishahara hii ilikwenda kwenye sekta zote karibu, tulibakisha eneo dogo tu lilobakia linafikiriwa. Eneo ambalo tulilibakisha ni wale wateule wa Rais hao hatukuwafanyia marekebisho

ya mshahara wowote tukasema hapana, hawa wateuliwa wa Rais wana *benefits* nyengine wacha tushughulikie wafanyakazi wengine wa kima cha chini na wengine wote wamefaidika. Tumeweka *formula* maalum pale *Alhamdulillah* tushukuru Mwenyezi Mungu na tumshukuru sana Rais wetu Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, ampe afya njema aendelee na nyinyi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi *Alhamdulillah* mambo si haba na tunaendelea kuyafanyia kazi ili yawe mazuri zaidi tukijaaliwa. Sasa kilichobakia sote tumuombee Mungu Rais wetu aendelee na afya njema yeye na familia yake *inshaallah* aendelee kutuongoza ili kazi ziende katika nchi yetu tufike 2020, *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie mambo yawe mazuri zaidi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza maelezo mengi yameshatolewa na Mwanasheria Mkuu, yameshatolewa na Naibu Waziri na Waziri wa Fedha na Mipango wametoa ufafanuzi mzuri sana kuhusu habari ya *vote* ya Mufti. Ofisi ya Mufti amesema Waziri wa Fedha na Mipango tunaijali sana, na mimi namuheshimu sana Mhe. Mufti, Kadhi Mkuu namuheshimu na vyombo vyangu vyote naviheshimu. Lakini imetoka kauli moja kidogo hapa imetutisha, imetutisha vipi?

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kauli iliyosema kwamba ikiwa Rais haingilii mihimili mengine kuna wasaidizi wa Rais wanaingilia, basi jambo kama hili hebu tuletewe sisi. Mimi aje aninong'oneze yule Mheshimiwa tu, Waziri fulani au mtu fulani, kwa sababu sidhani kama ikiwa Rais wetu anaheshimu. Sasa sisi wasaidizi wake tusiheshimu jambo kama hilo, haiwezekani.

Mhe. Spika, nakuombeni sana kwa mujibu wa utaratibu wetu ni vizuri sana na Kanuni yetu ya 59(6) ukisoma kinaeleza vizuri sana, kumtaja Rais kwa dhihaka au kwa namna nyengine yoyote haipendezi. Hebu tusomeni ile Kanuni jamani tumezipitisha wenyewe. Sasa hapa kila wakati, wakati mwengine Rais kaahidi, Rais kahaahidi, iliyoahidi ni serikali na yeye Rais kama kaahidi itatekelezwa Rais wetu ni mkweli, hakuna kisichowezekana, lakini si vyema kila wakati kumtaja Rais katika masuala ambayo si ya lazima, tutajeni Rais kwa yale mambo ya kumpongeza kama haya ya kuweka mishahara ya wafanyakazi kima chini *Alhamdulillah* tumpongezeni. Lakini kila wakati kutaja Rais, Rais, si vyema na sio Rais tu, nimesema Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais, lakini bahati nzuri Makamu wa Kwanza hatunaye tunae Makamu wa Pili. Sasa tujitahidini, tusome Kanuni ile ya 59.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilisema kuna suala zima ambalo nimesema Mhe. Hamza Hassan Juma kaniletea. Mhe. Hamza anitizame. Mhe. Spika, Mhe. Hamza nina historia naye refu sana huyu, kwa ruhusa yako naweza

nikaisema. Huyu ni mwanafunzi wangu, Skuli ya Haile Selassie zamani nilipokuwa Mwalimu Mkuu pale alikuwa anakaa kule anakokaa Kwamtipura, ilikuwa mbali sana zamani na siku zote huyu Hamza anachelewa. *(Makofi/Kicheko).*

Mhe. Spika, Mhe. Hamza kwa imani yangu yeye na wenzake nikatoa vibali maalum wachelewe na yuko hai yule pale simsingizii. Kwa sababu kawaida skuli saa moja tunaanza yeye mpaka saa moja na nusu au na dakika 40 anaingia pale, akifika pale kibali chake kipo wenye mikwaju yao wanakaa pembeni wanampisha, kapata ruhusa ya Mwalimu Mkuu. Sasa amekuwa mara nyingi sana katika bajeti zangu hata pale ambapo Waheshimiwa wote hawagongi miguu, yeye atagonga mguu, si mara moja, si mara mbili. Mheshimiwa toka ulipokuwa Waziri wa Mawasiliano wakati napitisha Wizara ya Elimu, Wajumbe wote hata wale rafiki zetu walipokuwemo kwenye Baraza bajeti ile ilipokuwa inapitishwa hakuna aliyegonga mguu, lakini yeye akasimama, kutoka nje akanambia eeh! bwana lazima tukutikishe kidogo tutizame uimara wako.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa kaniletea majukumu sasa hivi, kachangia kwa maandishi bado dakika tano nataka nije hapa ananiletea mambo mazito. Mhe. Hamza namuomba sana aniachie kama nilivyokujali mwaka 1979, nitakujali mwaka 2017 na kuendelea usiwe na wasi wasi. Lakini ninachosema Mhe. Hamza yale masuala aliyonieleza ni mazito, tunataka tukae, sio kama alivyosema Mhe. Zulfa Mmaka Omar tukae chini. Mhe. Zulfa Mmaka kwanza sitokuweka chini mimi, tutakaa sambamba mimi na wewe tuyapange yale aliyoyaomba tuyaweke sawa tukijaaliwa.(*Makofi*).

Kwa hivyo na Mhe. Hamza nataka atulie, masuala yake ni mazito, ukitizama nakla za barua zote zile hamna nakala ya Waziri hata moja iliyoletwa, ndio kwanza nayaona hapa, mazito yote sitaki kuyasema ni siri yetu mimi na wewe. Nakuomba sana, bora tunyamaze kwa humu ndani leo, tuje tukutane mimi na wewe tuyaweke sawa. Nadhani amenikubalia, aah! basi.(*Kicheko*).

Mhe. Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote hakika nataka niwahakikishie kwamba nimethamini michango yao, wapo waliotaka mambo mbali mbali tuyachukulie hatua haraka sana tutafanya hivyo. Ofisi hii ni kubwa tujue hivyo, ina idara karibu nane na taasisi nyengine karibu 14 kwa 22.

Mimi niwashukuru sana wafanyakazi wote wa Wizara yangu ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wanafanya kazi nzuri Mheshimiwa, kuanzia Naibu Waziri mpaka mfanyakazi yule wa kawaida. Lakini

Waheshimiwa nikwaambieni kitu kimoja, nasaha nyengine, kwa dhati kabisa Mhe. Spika, mpokuwa na matatizo msingojee vikao vya Baraza mkaja mkatutupia mawe hapa. Kwa nini hamuji maofisini mwetu tukakaa sisi na nyinyi tukalitatua tatizo hilo, kulileta hapa hatulisikii sisi tu, jamii yote ya Zanzibar inasikia. Kuna mambo mengine mazito, si vyema tukayasambaza watu wote wakapata taarifa zile. Ni vizuri tukaambizana kwanza, ukiona umekuja ofisini mara ya kwanza, mara ya pili hujasikilizwa basi njoo upasue. Lakini sidhani kama atatokea kiongozi katika serikali hii atakayedharau kiongozi kama Mwakilishi anakuja pale tusimsikilize.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja wakati umefika ili tupitishe vifungu. Nawaomba sana tupitishe vifungu hivyo bila ya matatizo yoyote hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafuzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji wale wote wanaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wananyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Spika: Waheshimiwa kabla hatujanyanyuka kidogo kwa ajili ya Kamati ya Matumizi nitakuita tena Katibu ili uite Kamati ya Matumizi.

Waheshimiwa tunakwenda kwenye Kamati ya Matumizi na sote ni mashahidi kwamba juzi ile kwa ule utaratibu ambao tulikuwa tumekwenda wakati tunapitisha vifungu vya Wizara ambayo imemaliza kipindi kilichopita tumechukua muda mwingi sana, na wizara hii ni wizara kubwa sana pamoja na kwamba mnaona sasa hivi ni saa 12 lakini tutakuwa na mzigo kama ule wa juzi kwa sababu vifungu ni vingi sana pia.

Sasa nakujulisheni kwanza ule utaratibu kwa sababu Mhe. Waziri amejibu pamoja na Mawaziri wengine ambao wameshirikiana kujibu hapa, hoja nyingi za Waheshimiwa ninafikiria watakuwa wamezigusa.

Sasa itakuwa ni vizuri mtu akikinyanyukia kifungu chochote kile, hoja yake ihusiane na fedha kwenye kile kifungu au sera, sio kwamba hujasikia kujibiwa unataka sasa kutumia nafasi ile ya vifungu upate majibu kwa jambo lako ambalo halihusiani na fedha wala sera. Hilo nina wasi wasi sitaliruhusu ili tuweze kuokoa muda. Hilo la mwanzo.

La pili Waheshimiwa tutavipitisha hivi vifungu kwa utaratibu mpya kidogo, haupo kwenye Kanuni kwa mujibu wa vifungu hivi vya kupitisha bajeti, lakini kwenye Kanuni imo tunapopitisha Miswada. Lakini huo utaratibu ni utaratibu ambao unatumika kwenye Mabunge ya *CPA,* kwa hivyo ni *good practice* ambayo tutakuwa tunaifanya.

Hii wizara ina *vote* kama tisa hivi, kila *vote* moja ina mafungu makubwa kama manne mpaka matano. Kwa hivyo tutakuwa tunalihoji lile fungu kubwa moja halafu watu watavinyanyukia vifungu vidogo vidogo vilivyomo ndani ya lile fungu kubwa, na nitakuwa nakupeni isipokuwa kifungu kidogo kile kimojawapo ambacho kitakuwa kimehojiwa kisihojiwe zaidi ya watu watatu wasikihoji hicho, ni mara tatu tu halafu iwe basi.

Baada ya hapo tutalihoji lile fungu na hatimaye tutakuwa tumekamilisha.

Baada ya maelezo hayo kama nitakuwa nimefahamika vizuri Mhe. Mohammed Said Mohammed nimehisi kama una kitu.

MUONGOZO

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, umetaja neno kuwa Mabunge ya *CPA* yanafuata mfumo kama uliouelezea na leo sisi tunapitisha mafungu na kusema unataja tu, Waheshimiwa Wajumbe sidhani kama watakuwa wana uelewa mkubwa wa hicho unachokitaja.

Sisi wengine tunakijua lakini Wajumbe walio wengi, sidhani kama watakuwa na uelewa huo. Sasa nilikuwa naomba muongozo wako tu nini kifanyike.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mohammed Said Mohammed. Nadhani maelezo yangu mtakumbuka tulipokuwa tukipitisha nafikiri Sheria ya Maafuta. Kuna sheria kama mbili tulifanya kitu kama hicho.

Sasa hili nalifanya kwa sababu hapo mbele tuna Mwezi wa Ramadhani utakapofika tutajikuta tunapindukia ile saa tisa ambayo imepangwa kwa mujibu wa Kanuni, mara nyingi zaidi kuliko kawaida. Kwa hivyo tunataka tulifanye hili ili kama *practice* hii itakuwa imekwenda vizuri hapa baadae tutaichukua tutaiweka kwenye Kanuni ili iwe ni *practice* ambayo inafanya kazi ili kuokoa muda. Kwa sababu huu utaratibu mzima wa programu ni utaratibu mpya kwa ujumla wake.

Waheshimiwa walio wengi kweli hawajafahamu kwa sababu tumepata mafunzo kidogo lakini bado haijakaa vizuri, kwa namna ambavyo inaonekana watu bado wanasimama kuhoji mambo ambayo yalishatolewa maelezo na Waheshimiwa Mawaziri. Ndio maana nimeona tuje kwenye hizi *best practice* ili tuone kama hili mtatuokolea muda basi tutaweza kulirithi baadae halafu kuliingiza kwenye Kanuni ili tuweze kulitumia. Tunalo kwa ajili ya vifungu vya Miswada ya Sheria lakini tulikuwa hatuna kwenye bajeti. Lakini nitawaruhusu watu kwenye fungu husika wasimame hapa wanne, watano lakini akijue kile kifungu.

Kwa mfano, nichukulie mfano wa Mahkama Pemba, lile fungu ambalo litakuwa linahusu Mahakama Pemba litakapokuwa limetajwa, mtu atanyanyuka halafu atalifanyia *reference* lile halafu baadae nitampa Mhe. Waziri atoe maelezo.

Lakini zaidi jielekezeni basi kwenye fedha kama mnahisi kuna upungufu au mnataka kuzihamishia sehemu nyengine kuliko kutaka maelezo ya juma tu; nyumba imevunjwa pahali kwa nini imevunjwa hiyo nyumba, yaani sasa vitu kama hivyo ndio ambavyo kidogo nitakuwa mgumu kuviruhusu kufanyika.

Baada ya maelezo hayo Katibu kwa shughuli inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU G 01 - OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Fungu G01	Ofisi ya Rais, Katiba, Sheri, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	130,084,000
Kifungu PG0103	Programu Kuu ya Usimamizi wa Utawala Bora na Haki za Binadamu	812,975,000
Kifungu PG0104	Programu Kuu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini	1,147,220,000

Mhe. Mwenyekiti: Namuona Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf halafu atafuatia Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi napongeza wote waliochangia na waliotujibu na maswali yangu yote nimejibiwa na nimeyasikia vizuri. Lakini sasa ningeomba anihakikishie kwamba kuhusu *vote* ya Mufti Mkuu lini wanatarajia watamkabidhi na hizi fedha walizoomba watawapatia zote asilimia wanazoziomba au watakuwa wanawakata kama siku zote asilimia 50 kushuka chini.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa sababu anaulizia fedha nafikiri umemuelewa naomba umjibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa anachokiulizia ni suala la *vote* ya Mufti na Mhe. Waziri wa Fedha...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma *microphone* yako iko wazi na unachozungumza tunakisikia huku.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mheshimiwa kama alikuwepo lakini nina wasi wasi labda alikuwa hayupo, lakini kama alikuwepo Mhe. Waziri wa Fedha katoa ufafanuzi mzuri sana, amesema jambo hili linazungumzika na linazungumzika vipi. Kwa sababu kuanzisha *vote* kila wakati kuna matatizo yake Wizara ya Fedha wana mikakati yao vile vile na utaratibu wao. Lakini kwa vile suala hili limefahamika unyeti wake, kuna njia tunaweza kufanya. Pesa zile zikasimamiwa na Katibu Mkuu lakini zikawa zinakwenda moja kwa moja kwenye Ofisi ya Mufti bila ya matatizo yoyote wala kusiwe na mashaka hayo,

atulie hili jambo tumelichukua kwa uzito wake na nimesema Ofisi ya Mufti tunaiheshimu sana na majukumu yake tunayajua.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye lakini kwa nini *vote* yake asipewe. Mimi naomba tu sisemi tena lakini naomba *vote* apewe ina umuhimu wake kwa yeye.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa serikali imesikia. Mhe. Mohammed Said Mohammed sasa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri na Waziri wametujibu vizuri sana.

Mimi nilikuwa tu na *concern* moja tu. Ofisi ya Mufti ni Ofisi kubwa sana ambayo inashughulikia mambo ya Kidini na mambo mengi sasa hivi yameanza kujitokeza. Lakini kubwa ambalo ninaliona fedha ambazo ametengewa kwa Ofisi ya Mufti ni kidogo mno. Ningeomba basi kuna fedha nitazisema baadae ziko wapi ili tumuongezee Mhe. Mufti ili kuweza kuendesha mambo na Ofisi yake kwa ufanisi zaidi, sasa hivi haina ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti: Zimo yaani kwenye fungu la wizara hii.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Liko la wizara hii halafu nitalisema baadae.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nafikiri tusubiri mpaka atapotuainishia hicho kifungu chenyewe cha fedha, halafu tutaamua kama hizo fedha zinaweza zikahamishiwa hapo kwa Mufti au vipi, au kama unataka kujibu jibu. Mhe. Ali Khamis Bakar, Ustadhi.

Mhe. Ali Khamis Bakar : Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, mimi hii wizara naiheshimu kwa sababu ndio wizara ambayo inasafirisha Mahujaji na mimi nimeshatia nia ya kwenda Hijja. Kwa hivyo nataka niulize kitu kimoja kidogo tu.

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri akitoa ufafanuzi wa masuala ya tende jinsi ambavyo zitagawanywa, lakini hapa kuna fedha ambazo zimeelekezwa kwa ajili ya wanufaika. Sasa mimi namuuliza tu, hizi fedha shilingi 270 milioni. Je, zitagawanywa vipi katika majimbo yetu ama katika Wilaya. Nilikuwa nataka kujua hivyo tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa fedha hizo zimehusianaje na tende, maana nimesikia kwanza...

Mhe. Ali Khamis Bakar: Naomba unisikilize kidogo, wakati akitoa majibu alitwambia hivi, kwenye masuala ya zakka na sadaka kwamba kuna tende zitagawanywa kwa ajili ya Mawilaya. Lakini sasa kuna fedha ambazo zimeainishwa katika kitabu hiki ukurasa wa 23 naomba afungue, kuna fedha shilingi 270 milioni zimeainishwa hapo. Sasa nilikuwa nataka kujua je, fedha hizi tutafaidika vipi katika majimbo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hizo fedha unazozungumza ziko kwenye hichi kifungu. Hebu angalia hiki kifungu ulichokizuwia, halafu na hiyo fedha unayozungumza.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Hiki kifungu si kinazungumza masula ya Dini na ndio hapo kwenye hiyo, kwa sababu tukitoka hapo tunaingia kwenye hakimiliki, sasa hapa kwenye Dini ndio pahali pake.

Mhe. Mwenyekiti: Sio hapa basi naomba tuendelee.

Kifungu PG0105	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	5,148,858,000
Kifungu PG0106	Programu Kuu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma	622,309,000
Kifungu PG0107	Programu Kuu ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Mawasiliano ya Serikali	11,132,821,000

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim. Mara tatu Mhe. Hassan Khamis. Mhe. Jaku tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nikushukuru kwa umakini wako, maana jana kiti chako kidogo kiliyumba alipokalia Naibu Spika hapo jana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim, nenda kwenye hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mpaka nikaleta uthibitisho.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku naomba nenda kwenye hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kuhusu mikataba Mwanasheria Mkuu.

Serikali ilianzisha mikataba na serikali hapa mara nyingi niliishauri hapa jana, huwa nasikitika kwenye mikataba huwa inapigwa chini kama inapigwa mwereka huwa wana- *fail* sana katika mikataba. Tumeangalia nafikiri mikataba ya mkonga, *CCTV camera,* serikali hapa inapoteza pesa nyingi kuhusu mikataba.

Je, imejipanga vipi kwenye suala hili kuhusu mikataba pesa nyingi zinapotea kwenye mikataba.

Kwa mfano, uwanja wetu wa ndege, nilichangia jana hili isije ikafika kama jana Waziri mmoja akazidiwa hapa akaja akasema hapana sikuchangia mpaka nilipotoa ushahidi jana hapa ndio nikapona mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Swali la sera hili Mhe. Waziri majibu. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nilimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub na yeye jambo ambalo aliliomba ni tuwe na *standard format* za mikataba.

Mimi nikamwambia hilo ni jambo ambalo sasa hivi tunalifanyia kazi na *of course standard* hizi ilikuwa tuzitowe mapema. Lakini kwa sababu ile sheria yenyewe ya *procurement and disposal* ilifanyiwa marekebisho na Baraza. Kwa hivyo hata ule utaratibu wa ile mikataba yenyewe umebadilika. Zamani ilikuwa maeneo matatu, ni *service, consultancy and goods.*

Sasa hivi kuna maeneo mengine mengi yamezidishwa. Sasa nilichomwambia ni kwamba hii ya kutayarisha *standard format* ni jambo ambalo tunalifanyia kazi na tunalisimamia. Lakini pia nimewaagiza Wanasheria wangu waende wakajifunze kwa wenzetu Tanzania Bara, ambao wao tayari wameshakuwa na utaratibu huu ili tujue na sisi tunaweka utaratibu gani mzuri wa kuweza kusimamia mikataba hii ya serikali.

Lakini pia nikasema kama *over role,* ile *oversight* sio tu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *oversight role* pia inatuhusu sisi Wajumbe wa Baraza, kwa sababu sisi ndio tunaoidhinisha fedha na sisi ndio tunaotembea kwenye taasisi hizi kwa mwaka mara nne. Kwa hivyo ile *oversight role* na sisi lazima tuwe nayo, tusisubiri mpaka jambo linaharibika, halafu ndio tunakuja kuhoji. Kila

tunapokwenda kwenye hizi wizara ni lazima tuhoji mmeingia kwenye mikataba gani, mmefika hatua gani, utekelezaji wake ni nini, twendeni tukaone. Hiyo ni *oversight role* ambayo inabidi Kamati zetu hizi izifanye na izifanye kwa makini. Hayo ndio ambayo niliyajibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Mwanashiria Mkuu na nimwambie tu kwamba maneno mazuri ni sasdaka na maneno mazuri humtoa nyoka pangoni, lakini hili suala ni la muda mrefu, jitahidi Mhe. Mwanasheria Mkuu isiwe maneno tu tunataka na vitendo. *UNDP* walianzisha semina hii.

Nimshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa maneno yake mazuri na ushauri wake tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi pia nilileta maombi yangu au hoja zangu za sheria.

Nilizungumza kwamba *human rights* kwa nchi za wenzetu walioleta kutokana na maadili yetu kuna nyengine nzuri na kuna nyengine zinaharibu maadili. Sasa nikapendekeza kwamba wale wote wanaoleta unga (*drugs)*, wale wote majambazi, wenye jinsia moja wanaojiuza na wanaobaka watoto wanyongwe.

Mhe. Mwanasheria Mkuu kakubali lakini nataka anihakikishie sheria hiyo ataileta lini hapa na katika hayo matano niliyoyapendekeza mimi ni yepi atayaleta.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sijakubali. Nilichosema ni kwamba kwa sasa hivi kama Mhe. Nadir angesoma Sheria ya Adhabu Namba 6 ya mweka 2004.

Moja ya adhabu ambayo Mahakama inatakiwa itowe ni pamoja na adhabu ya kifo, ndio nikasema kwa sasa hivi Sheria ile imeweka adhabu maeneo mawili. Eneo moja ni la *treason* na eneo moja ni la *murder*.

Makosa hayo mtu akihukumiwa na Mahakama na Mahakama ikitamka kwamba ana makosa basi adhabu zake ni hizo. Lakini nilimwambia pia Mhe. Nadir kwamba hiyo hoja yake yeye awe nayo. Sheria hii karibu tutakuja kuifanyia marekebisho, awe nayo tutakapokuja hoja yake ailete. Lakini humu ndani tunaamua kwa wingi wa kura.

Sasa itategemea wale ambao wataitaka hoja yake na wale ambao watataka maeneo haya yabaki kama yalivyo, labda tuongeze adhabu. Kwa sasa hivi adhabu ya maeneo haya imetajwa.

Lakini kwa mfano kosa la *rape* ambalo adhabu yake ni kifungo cha maisha, kama Mahakama haikukufunga kifungo cha maisha basi ikufunge adhabu isiyopungua miaka 30 na maeneo mengine yametajwa. Sasa ama tuzidishe ile adhabu ama Mhe. Nadir Abdul-latif aje asimamie hoja yake, lakini na baadae tutaamua.

Ndivyo nilivyosema Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana kwa majibu ya Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini ninachotaka kusema hata mtu akifungwa miaka 30 saa nyengine hufanyika ujanja hapo mbele baada ya miaka fulani, kama miaka 10, 12 mtu hutoroshwa au hufanya njia vyengine. Lakini...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe usiitumie fursa hii kutaka kutoa hoja.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Haya sawa. Sisi tunachotaka kuokoa taifa. Mimi ningeomba ailete haraka iwezekanavyo ili tupate kujadiliana na Wawakilishi wenzetu tupitishe kwa hawa watu ambao watataka kunyongwa ndani ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifungu PG0301	Programu Kuu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria	923,706,000
Kifungu PG0302	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu	722,404,000
Jumla Kuu		**1,646,109,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU G04 - OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Jumla ya Mapato **104,067,000**

FUNGU G04 - OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu PG0401	Programu Kuu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai	1,248,525,000
Kifungu PG0402	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mkurugenzi	

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza habari ya kisera kuwa kuna utaratibu katika Ofisi ya Muendesha Mashtaka kuwapandisha madaraja wafanyakazi wake, lakini wapo wafanyakazi ambao walipandishwa madaraja lakini mpaka leo walikuwa zile stahiki zao hawajapewa na sikujua lini wanaweza wakapewa. Sasa nilikuwa nataka kukamata mshahara wa *DPP* mpaka nione wanapewa lini hizi stahiki zao.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kuna *restructuring* ambayo inakwenda kwenye ofisi ya *DPP*, kuna mapendekezo mengi ambayo wameyaleta Serikalini na Serikali inayafanyia kazi.

Sasa nimuhakikishie Mhe. Dimwa kwamba kwanza Serikali haimdhulumu mtu haki yake, kila mtu atapata haki yake. Lakini ile *structuring* itakapokamilika ya Ofisi ya *DPP*, nadhani na haya yote ambayo wamesema yatakuwa yamefanyiwa kazi na ile Ofisi itaanza kufanyakazi yake kama ambavyo kuna kazi ambayo tumepewa tukae mimi *DPP* na Katibu Mkuu Kiongozi.

Sasa tutakapomaliza ile kazi basi nadhani haya ambayo Mhe. Dimwa pamoja na Mhe. Zulfa waliyasema, nadhani yatashughulikiwa kwa utaratibu huo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana mdogo wangu Mhe. Mwanasheria Mkuu tuendelee.

Kifungu PG0402	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	1,080,575,000
Jumla Kuu		**2,329,100,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU GO5 - TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu PG0501	Programu Kuu ya Kuzifanyia Mapitio ya Sheria	383,245,000
Kifungu PG0502	Programu Kuu ya Utawala na Uratibu wa Kupitia Sheria	201,115,000
Jumla Kuu		**584,400,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU GO6 - OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

Jumla ya Mapato **84,555,000**

FUNGU GO6 - OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

Kifungu PG0601	Programu Kuu ya Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma	1,218,801,000
Kifungu PG0602	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	1,408,399,000

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ana watu ambao anataka ajenge uwezo nao ma-*professionals* mbali mbali katika Ofisi yake. Lakini hatujaona *strategic* ambayo imeoneshwa kwa sababu wakati mwengine ana *lack* na kutizama vitu kama ma-*engineers*, kuna watu inabidi atowe nje.

Sasa hii pesa iliyojengwa hapa nimeoina ni ndogo sana. Ningeomba pesa hii hapa, ndio kile kitu nilichokuambia kimenipita pia nilitaka niigawe niiongeze kwa hapa. Kwa hivyo fungu hili ni dogo la kuweza kuwaajiri na tunataka ufanisi katika utawala bora na tunataka ufanisi katika udhibiti wa hesabu za serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa hatua tuliyofika sasa hivi nadhani suala suala hilo litakuwa ni gumu. Kwanza utaratibu wa utoaji wa pesa ni hivyo.

Kwa hivyo mimi nashauri sana kwamba tuliangalie kwa kipindi kinachokuja lakini kwa mwaka huu itakuwa sio rahisi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nimemfahamu ni mwalimu wangu sana.

Mhe. Mwenyekiti, labda ni-*declare interest* kuwa mimi ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na tuna uwezo wa kukaa na Serikali kuangalia, tunapeleka pesa wapi na zimezidi wapi. Mimi naona bado hatujachelewa, tukiri tu Mhe. Waziri hili fungu ni dogo mno na tulitake kuliongeza.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, sikumsikia vizuri na labda angerudia, zitoke wapi ziingie wapi. Kwa sababu na huko tunakotaka kuzitoa Mhe. Mwenyekiti, tutakwenda kuna mahitaji na bajeti hii imepangwa kwa kuzingatia mahitaji ya kila eneo na kwa bahati nzuri yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tumepitia tumeona. Sasa tunatoa wapi, tunaweka wapi, hilo ndio suala la msingi.

Tunashauriana kama ni hapa tunahisi kwamba fungu hili ni dogo, wazo lake ni zuri tulizingatie kwa mwaka wa fedha unaokuja kuliko mwaka wa fedha huu, kwa sababu na huko tutakwenda kuondoa vitu ambavyo tayari tumeshavipanga na ni vya muhimu. Sasa hapa sikumsikia vizuri tunazitoa wapi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimemuelewa sana kaka yangu Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ni Mwakilishi wangu wa kijijini kwangu. Bado tunao uwezo kuna *E-government* ina pesa nyingi tu na kuna sehemu nyingi tu ambapo tunaweza tukafanyia *reallocation* tukazitia kwengine, bado tunao uwezo wa kuzisimamia hoja zetu ili tuweze kuitoa kwenye zile pesa ambazo tumeziweka nyingi na wazitizame huku nimeziona ziko nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa labda na mimi niongezee tu, huu utaratibu ambao tunakwenda nao sasa hivi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ni kwamba baadae Serikali inaweza ikakaa sasa na ile Kamati baada ya kumaliza haya masuala yote. Halafu mkatizama bila ya kuathiri bajeti kuu ya serikali, lakini ndani ya hivi vifungu vidogo vidogo kama kuna uwezekano wa kuhamisha hivyo vifungu kama hivyo ambavyo atakuwa amevipendekeza Mhe. Mwenyekiti wa Bajeti, ili kuona. *(Makofi)*

Baadae nadhani mnaweza mkakaa mkalitengeneza hili baada ya kumalizika huu utaratibu mzima. Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, wazo la kukutana tunalikubali, lakini niliuliza pale kwamba Mhe. Mjumbe anataka tuzitowe wapi fedha hizi na kwa babati nzuri amesema kwenye *E-government*.

Sasa mimi nimwambie tu kwamba pamoja na kwa faida ya Wajumbe wengine wote kwamba mradi wa *E-government* ni mradi ambao tumekuwa tukiusubiri kwa muda mrefu, kwanza hilo, hii ni *Phase II. N*a tayari serikali imeshatumia fedha nyingi sana kuwekeza katika miundombinu na ni mradi ambao una *component* ya fedha za nje ambazo zinataka *commitment* ya serikali, dhima ya serikali. Kwa hivyo hizo fedha zilizokuwepo hapa ni *commitment* ya mradi huo kufuatana na misaada wa fedha za kutoka nje, hatungeweza kutoa fedha.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, hoja ya tatu lakini sina nia ya kuzuwia hili fungu lisiende, nina nia ya kuwafahamisha Waheshimiwa Wawakilishi na Serikali kwa pamoja. Kwa sababu hii Kanuni tuliipitisha wenyewe tu, kwa nia nzuri tu ya kuweza baadae kufumua bajeti ya serikali na tukaiweka sawa kwenye vifungu ambavyo tutaona vinafaa.

Lakini sasa tukiwa tuna ukakasi wa kuwa hatuwezi basi tutakuwa maisha hatuwezi. Kwa sababu bado mradi wa *E-government* una ukakasi mkubwa, hauleti tija kwa wananchi. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu PG0602	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	1,408,399,000
Jumla Kuu		**2,627,200,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU G 07 - MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI.

Kifungu PG 0701	Program Kuu ya Kupunguza Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Mhe. Hassan Khamis Khafidh: Mhe. Mwenyekiti, mamlaka hii imekuwa inafanya kazi kwa vikwazo vingi. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa inajitahidi kuwatafuta watafuna rushwa nchi hii lakini hatuoni *outcome* yake, hatuwaoni kupelekwa Mahakamani, na ukifuatilia ukiliuliza mafaili yao yanakwama kwa *DPP* mimi nikasema kwa nini tusitumie kama ya *Drugs*

Bureau ya Marekani tukabadilisha sheria kuipeleka mtu yeyote aliyekamatwa na rushwa nchi hii ikenda moja kwa moja Mahakamani isipitie kwa *DPP*.

Naomba jibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mheshimiwa nimemsikia Mhe. Hassan lakini naomba nimjibu kama ifuatavyo.

Mwenye mamlaka ya kufungua kesi zote za jinai kwa mujibu wa kifungu cha 56(a) cha Katiba ni Mkurugenzi wa Mashtaka. Yeye ndiye amepewa mammlaka ya Kikatiba ya kufungua kesi zote za jinai na kama akiisoma vizuri ile Sheria ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ataona, kama pamoja na kazi zote ambazo rushwa inafanya lakini mwisho lazima ipeleke jalada kwa *DPP*, kama vile ambavyo wanafanya Polisi. Watafanya uchunguzi wote lakini wakishakumaliza lazima wapeleke lile *file* kwa *DPP*, kwa sababu hizo ni nguvu za Kikatiba ambazo amepewa *DPP*.

Natambua inawezekana nchi nyengine utaratibu wao ni tofauti lakini sisi hatuna haja ya kuiga utaratibu wa kila mtu. Sisi utaratibu wetu wa Kikatiba ni huo ambao umeelezwa na Katiba kama Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye mwenye dhamana ya kufungua Mashtaka yote ya jinai kwa hapa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Khafidh: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini Wahenga wamesema, "Zuri huigwa".

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na leo hii tukienda katika wangapi wamekamatwa na wangapi wamefungwa. Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda jela hatujawakuta, tumemkuta mtu mmoja tu aliyekamatwa na hiyo rushwa, tangu Mamlaka ya Kuzuia Rushwa ifunguliwa mpaka leo karibu miaka minne au mitatu lakini tatizo kesi zao zinakwama kwa *DPP* haya mafaili yao.

Sasa nilichokiomba mimi kama ni Katiba, kama ni Sheria, kama ni Sera, sisi ndio wabadilishaji, kama yeye hakubaliani na rushwa na kama yeye anakubaliana na Serikali kuleta hapa tukapitisha Sheria ya kuwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa, naamini sana Mhe. Mwanasheria Mkuu yeye hapendi rushwa, na wala naye hali wala hachukui rushwa.

Sasa kama ni hivyo anaona vigumu gani kuleta mabadiliko ya sheria aidha ya Katiba au Sheria tukaja hapa tukayabadilisha na nchi nyengine zimefanya. Sasa

Mwanasheria Mkuu anaponiambia kwamba hatuwezi kuiga. Mimi najua zuri tumeiga, yeye mangapi kaiga kutoka nchi nyengine, sasa ninamshangaa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea au vipi?

Mhe. Hassan Khamis Khafidh: Jibu kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, rushwa ni tatizo na kesi *outcome* yake hatuzioni sasa anijibu…

Mhe. Mwenyekiti: Basi tushasikia Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Hassan alitaka ule utaratibu na mimi nimemueleza vizuri utaratibu wetu wa Kikaba ambao upo.

Lakini nitamuongezea kama pamoja na uwezo huu ambao *DPP* amepewa Katiba pia haimkatazi kukasimu madaraka yake kwa mtu mwengine yeyote. Kwa hivyo *DPP* akiona kuna haja ya kufanya hivyo basi anaweza akakasimu madaraka yake kwa mtu mwengine. Lakini haiondoi ile nguvu yake ya Kikatiba ya yeye kuwa ndio mtu pekee anayeweza kufungua mashtaka ya jinai hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hassan Khamis Khafidh: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuwa mkaidi lakini nataka tuendelee lakini naamini Mhe. Mwanasheria Mkuu hapandi rushwa. Sasa ninalolisema hapa ni la kuweza kuizuia rushwa Zanzibar, lakini amekuwa mgumu mgumu kidogo lakini naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tunaendelea lakini Mheshimiwa Afisi ya *DPP* imeanzishwa sio zamani sana, kwa sababu mwanzo shughuli zote zilikuwa zinafanywa na Polisi si ndio, halafu tukaona ipo haja ya kuwepo Mkurugenzi wa Mashtaka. Sasa hivi anafanya hizo kazi ameshakuwa yeye sasa ndio yuko *inefficient*, turudi tena kwa kumtafuta mtu mwengine wa kukasimiwa. Nadhani tulitizame vizuri hili kidogo Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Khafidh: Mheshimiwa nafikiri nimeeleweka hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante umefahmika tunaendelea.

Kifungu PC 0701	Program Kuu ya Kupunguza Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	244,220,000
Kifungu PG 0702	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	1,090,480,000
	JUMLA KUU	**1,334,700,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G08 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu PG 0801	Program Kuu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma	462,228,000
Kifungu PG 0802	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma	478,072,000
	JUMLA KUU	**940,300,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU G09 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Mawaziri mnatusumbua kidogo tunataka kusikilizana.(*Makofi*)

Kifungu PG 0901	Program Kuu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini	217,650,000
Kifungu PG 0902	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Utumishi wa Umma	

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema kuna baadhi ya wafanyakazi wa Mkoa wa Kusini ambao walituhumiwa kula pesa za wazee na baadhi ya hao tayari wengine wameonekana hawana hatia, lakini wengine wana hatia. Lakini wale watatu ambao waliokuwa hawana hatia mpaka leo hawajapata haki yao na mmoja ameshastaafu. Sasa nataka kujua ni haki yao ya kurejeshwa au bado tunaendelea kuwashikilia ijapokuwa watu wale hawana hatia yoyote.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mohammed kwamba ni kweli hilo suala ambao analisema lipo na naomba aelewe kwamba Serikali kila siku huwa haimkandamizi mwananchi wake, isipokuwa Serikali inakuwa mstari wa mbele kumtetea mwananchi huyo.

Sasa nimwambie tu Mhe. Mohammed Said Mohammed kwamba sheria itachukua mkondo wake. Lakini kama itaonekana kwamba watu hawa hawana hatia basi mara moja wataachiliwa, lakini ikiwa vyenginevyo basi sheria itachukua mkondo wake. Lakini nimwambie tu kwamba mazungumzo yanaendelea kuhakikisha kwamba hawa watu kama wana hatia au hawana hatia, kama hawana hatia wakati wowote wanaweza wakaachiwa waendelee na wale ambao wanaodai stahiki basi watapewa stahiki zao.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana ndugu yangu Naibu Waziri msomi wa Sheria, lakini nataka nimwambie tayari hao watu wameshajulikana hawa wana hatia, hawa hawana hatia. Sasa sheria gani ichukue mkondo wake, ni uamuzi tu wa haraka wa kuweza kuwapa mafao yao tunawaweka mpaka lini.

Sisi Serikali haiwezi kuwakandamiza watu ni kweli lakini sheria gani ichukue mkondo wake. Mimi naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Said anafahamu taratibu za kisheria na Mhe. Nabu Waziri kajibu vizuri sana.

Lakini mimi nimshauri jambo moja, haya masuala aliyozungumza basi aje Ofisini tukae mimi na yeye, tushauriane. Kwa sababu sheria ni sheria tutafahamishana na tutawaita wanasheria wetu pale tujaliane hili suala mpaka tulipatie ufumbuzi. Kwa sababu hakuna kitu kizuri kuliko kufanya *dialogue* baina ya sisi na yeye na hao wahusika ili tujue na tunawaelimisha wajue kosa lao.

Kwa sababu sheria ikishamtia hatiani au Mahakama ikishamtia hatiani kwamba huyu kafanya kosa, ndio kafanya kosa. Sasa kama anakata rufaa akate rufaa ya juu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nashauri kwamba hili suala tusubiriane tushauriane kwamba aje Ofisini atuletee hili suala, ili tuweze kulifanyia kazi na panapo haki atapewa haki yake na kama hana haki hatoipata haki yake.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana mwalimu wangu na leo amenisomesha tena. Lakini nataka kumwambia kitu kimoja, tunaingiza Serikali kwenye matatizo na tuweze kufunguliwa mashitaka Serikali pasipo manufaa yoyote. Tayari *DPP* amesha-a*gree*, hawa wana makosa, hawa hawana, tunachelea nini kuwapa haki yao.

Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa wale ambao hawana makosa Serikali inafanyaje.

Mhe. Waziri wa Nchi, OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, wale ambao wameshaonekana hawana makosa watapewa haki zao bila ya matatizo yoyote, kama hawana makosa na ushahidi upo na taarifa zao ziletwe tutachukua hatua tutawarejeshea.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, naomba tu tuende pamoja na Mhe. Waziri ili tuweze kulijua suala hili limekwenda je.

Mhe. Mwenyekiti: Asante nafikiri ameshauri hivyo yeye mwanzo tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tupo katika usimamizi wa watumishi. Jana nilizungumza hapa na nikatoa mawazo kuhusu Jaji Mkuu stahiki zake zitoke katika Mfuko Mkuu wa Serikali, baada ya Mrajis kuwa na mrundiko mkubwa wa matumizi, afanye gari *service*, sijui kama mafuta atoe yeye, wino, kompyuta zote za Majaji.

Mhe. Mwenyekiti, nilipendekeza ili hadhi ya Jaji Mkuu ipate kuheshimika zaidi stahiki zake zitoke katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Jaji Mkuu ni kiongozi mkuu moja wa nchi hii. Sasa hivi taratibu zimebadilika tu lakini hapo mwanzo akiondoka Rais, nafikiri alikuwa anakamata nafasi yeye…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hii Tume ya Utumishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tume ya Utumishi akiwemo Jaji Mkuu vile vile ni mtumishi wa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Hamna Mheshimiwa na mimi Spika pia utanipeleka kwenye Tume ya utumishi, Mhe. Rais utampeleka Tume ya Utumishi. Mihimili hii Mhe. Jaji Mkuu, Spika, Rais sijui sio hapa. Tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu PG 09021	Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Utumishi wa Umma	294,150,000
	JUMLA KUU	**511,800,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yetu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Spika: Mhe. Wajumbe naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nashukuru sana lakini kabla sijaahirisha napenda niwakumbushe kwamba kesho siku ya Jumamosi Baraza litakuwako, lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 23 Baraza la Wawakilishi halipo siku ya Jumamosi na Jumapili.

Sasa ningemuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu aweze kuitengua hii Kanuni ili ituwezeshe tuje kesho kwa ajili ya kusikiliza hoja ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ili tuiamue hapa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru na kama ambavyo umeniagiza, naomba kutenga kando Kanuni ya 23(4) ambayo ndio inazungumzia siku na nyakati za vikao na hoja yangu ni kwamba tuitenge kando Kanuni hiyo ili kesho siku ya Jumamosi tuweze kuja na kuendelea na shughuli zetu za Baraza.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante **Wa**heshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono naomba sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nina matangazo.

Tangazo la mwanzo ni kutoka kwa Mwenyekiti wa UWAWAZA anawatangazia Wajumbe wote wanawake wabakie kuna kikao cha dharura baada ya kutoka hapa.

Tangazo la pili Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anawatangazia Waheshimiwa wote kuwa ile shughuli ya kumdhamini Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein katika *Sport* 65 itafanyika kesho Jumamosi tarehe 20/5/2017 Saa 2.00 usiku katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani Kikwajuni, mnaombwa nyote kuhudhuria na kutoa mashirikiano katika kumdhamini Mhe. Rais wetu mpendwa ahsante sana.(*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe baada ya matangazo hayo machache naomba sasa nitoe shukurani zangu za dhati kutokana na namna ambavyo tumeiendesha hii shughuli na imeweza kutuokolea wakati. Tukumbuke kwamba tuna mgeni mwezi mtukufu wa Ramadhani ambao unakuja na hizi shughuli zetu tutakavyokuwa tunaziendesha, tutajitahidi sana kujaribu kufuata utaratibu huu ili kuokoa wakati. Kwa sababu jana tulitumia muda mwingi sana katika kupitisha hivi vifungu, kwa hivyo utaratibu tunaokwenda nao naona ni mzuri sana, baadae itabidi tuuchukue ili uingie kwenye Kanuni zetu, uweze kutusaidia katika uendeshaji wa shughuli zetu za kawaid za kila siku.

Baada ya matangazo hayo machache, sasa naomba kuahirisha shughuli za Baraza mpaka kesho siku ya Jumamosi saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 1.30 usiku Kikao kiliahirishwa hadi
tarehe 20/05/2017 saa 3.00 asubuhi)